

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI**

**Kikao cha Tano – Tarehe 4 Februari, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

***DUA***

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 53

**Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale  
Kupatiwa Watumishi**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA** aliuliza:-

Hospitali ya Karumwa ambayo ni ya Wilaya mpya ya Nyang'hwale haina watumishi wa kutosha kwani ina daktari mmoja, Manesi watatu na mtaalam mmoja wa Maabara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka watumishi wa kutosha katika hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya, Karumwa kilichoko katika Wilaya mpya ya Nyang'hwale kina Daktari mmoja, Manesi watatu na Mtaalam mmoja wa maabara. Kutokana na tatizo la upungufu wa watumishi wa sekta ya afya kuwepo katika hospitali, vituo vya afya na Zahanati zote nchini kikiwemo kituo cha afya Karumwa, Serikali imechukua jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa udhahili wa wanafunzi wanaojiunga na fani za Udaktari na Uuguzi unaongezeka katika vyuo vikuu na vyuo vya ngazi ya Diploma na cheti. Aidha, Serikali imerejesha kada za chini za afya zilizokuwa zimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo, hivi sasa Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inawapanga wahitimu wa fani za afya moja kwa moja katika vituo vya kazi baada ya kibali kutolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hivyo, ili kuondoa upungufu wa watumishi katika Kituo cha Afya, Karumwa, Halmashauri inatakiwa kuomba kibali cha kuajiri watumishi wa afya kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii waweze kupangwa kwa kadri wanavyopatikana katika soko la ajira.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali, kwa kuwa katika hospitali hiyo ya Karumwa, ambayo ni hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale imekuwa na ongezeko kubwa sana la wagonjwa wanaokuja kutibiwa na kulazwa pale na hasa katika wodi za akinamama wanaokuja kujifungua pale, kumekuwa na ongezeko kubwa sana kufikia hatua akinama wawili kulala kitanda kimoja, pengine kulala chini pamoja na vitoto vyao. Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kupanua hospitali hii au kuongeza wodi za akinamama wazazi ili kutatua tatizo hili linalowapata akinamama hao?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tatizo ambalo liko Karumwa, liko pia katika hospitali nyingi, vituo vya afya vyetu na hata zahanati kote nchini na mahitaji ya huduma ni makubwa kutokana na ongezeko kubwa la wagonjwa. Tunazo njia ambazo tunaweza kuzitumia ili kupanua wigo wa huduma hii kwenye hospitali ile pale Karumwa. Kwanza, Halmashauri yenyewe kuona umuhimu wa kupanua hospitali yao kutokana na ongezeko la wagonjwa liko kwa sasa. Hili pia linaweza likafanywa kupitia mipango ya Halmashauri yenyewe ili iweze kupanuliwa na huduma hiyo iweze kutolewa kwa wagonjwa ikiwemo na upanuzi wa wodi yenyewe ambayo inaonekana ina idadi kubwa ya wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili bado tunashauri, Halmashauri ya Nyang'hwale iweze kuingia kwenye mipango yake ya bajeti ya kupanua hospitali yake, lakini

pia kupanua wodi na kuongeza hata wodi nyingine ili sasa Serikali iendelee kutoa huduma ya kuleta Madaktari kadri ambavyo Menejimenti ya Utumishi wa Umma iweze kutoa ajira nyingi kwa hospitali ile kama ambavyo tumeelekeza kwenye jibu la msingi.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKIMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa tatizo la watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ni sawa kabisa na tatizo lililoko katika Wilaya ya Geita hasa katika Vituo vya Afya vya Katoro, pamoja na Bukoli na Chikobe. Ningependa kujua sasa nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba watumishi wanapatikana kule?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema kwenye jibu la msingi, lakini pia hata kwenye jibu la swali la nyongeza la Mheshimiwa Chagulla kwamba, matatizo hayo yaliyozungumzwa kule Karumwa, Wilaya Nyang'hwale yanafanana sana na matatizo yaliyo kwenye hospitali zetu za Wilaya kwenye Halmashauri zote nchini kote, upungufu wa miundombinu, lakini pia huduma zinazotolewa kutokana na uchache wa watumishi wa Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado maelezo tuliyotoa kwenye jibu la msingi ni kwamba, Halmashauri zote zenye upungufu wa watumishi, kwa idadi ya watumishi ambayo wanatakiwa sasa Halmashauri zenyewe ziandike barua Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili iweze kupatiwa kibali cha kuweza kuwaajiri watumishi wengine na

Wizara inaweza kutoa nafasi hiyo kutegemea na idadi ya wasomi walioko kwenye soko la ajira.

Na. 54

## **Usomaji wa Mapato na Matumizi Katika Mikutano Mikuu ya Kijiji**

**MHE. JOSHUA S. NASSARI** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya Wakurugenzi walioshindwa kuwachukulia hatua za kinidhamu Watendaji wa Vijiji kwa kosa la kutosoma taarifa za mapato na matumizi kila baada ya miezi mitatu kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa Namba 7 ya mwaka 1982 kama ilivyorekebisha na Sheria namba 6 ya 1999?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joshua Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kifungu cha 141 cha Sheria Namba 7 ya Mwaka 1982 na Sheria Namba 6 ya Mwaka 1999; Afisa Mtendaji wa Kijiji anapaswa kusoma taarifa ya mapato na matumizi ya kijiji husika kila baada ya miezi mitatu katika Mkutano Mkuu wa Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa ipo changamoto kuhusu Serikali

za Vijiji kutosoma taarifa za mapato na matumizi kama sheria inavyoelekeza. Kutofanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa sheria na kwa mantiki hiyo Mkurugenzi wa Halmashauri husika anapaswa kumchukulia Afisa Mtendaji wa Kijiji hatua stahiki. Wakurugenzi wa Halmashauri wamekuwa wakichukua hatua za kinidhamu kwa wahusika hali hii inapojitokeza, mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ambapo Watendaji wa Vijiji vya Likambana na Marurani walifukuzwa kazi kwa barua zenye Kumb. Na. MM/AR/CS.2/79/22 na MM/AR/CS.S/79/23 zote za tarehe 18 Agosti, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Mulala amesimamishwa kazi kwa barua Kumb. Na. PF15577/22 ya tarehe 9 Machi, 2012 kwa kosa la kutosoma taarifa hizi kwa roho mbili za mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la uwezo mdogo wa baadhi ya Watendaji wa Vijiji wa kuandaa taarifa hizi, jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo. Ili kukabiliana na tatizo hili, Serikali kupitia Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo, imeweka utaratibu wa kuwapa mafunzo watendaji ili kuwajengea uwezo wa kusimamia misingi ya utawala bora ikiwemo usomaji wa taarifa za mapato na matumizi na usimamizi wa fedha. Vile vile Wakurugenzi wa Halmashauri wameagizwa kuhakikisha kuwa bajeti kwa ajili ya mafunzo hayo inatengwa na mafunzo hayo yanatolewa. Aidha, hivi sasa Serikali inamtaka mwajiriwa kuwa na elimu ya kidato cha nne au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitasita kufuatilia utendaji kazi wa Wakurugenzi na Maafisa Watendaji wa Vijiji na kuchukua hatua stahiki kwa atakayebaini kutenda makosa hayo ili kuimarisha uwajibikaji. Aidha, Makatibu Tawala wa Mikoa wameagizwa kusimamia mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutekeleza majukumu yao na kwa kuleta ufanisi. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya upande wa Serikali kwamba imekiri kuwa, tatizo lipo na ni kubwa. Lakini kumbukumbu zangu zinanionesha kwamba, kwa barua ya Mkurugenzi wa Halmashauri yangu wa Meru ya tarehe 28 Agosti, 2012, Mkurugenzi alikiri kwamba watendaji wengi hawasomi taarifa za mapato na matumizi na akasema pengine ni kwa sababu ya uelewa mdogo, kuogopa hadhara au wakati mwingine watendaji hao si waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile nimeiona barua ya Mkurugenzi kwenda kwa Watendaji wa Vijijini ya tarehe 25 na kwenda kwa Watendaji wa Kata ya tarehe 28 Mei, 2012, kuwataka Watendaji wa Kata wahakikishe kwamba Watendaji wa Vijiji wanasoma mapato na matumizi kwenye mikutano mikuu ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kwa barua nyingine ya Mkurugenzi ya tarehe 2 Januari, 2013, anakubali kabisa kwamba Halmashauri haina kumbukumbu ya kwamba ni vijiji vingapi ambavyo vimesoma mapato na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mkristo na nikienda Kanisani huwa tunatoa sadaka na kila Jumapili inayofuata tunapokwenda kwenye sala tunasomewa kwamba ni shilingi ngapi zimekusanywa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa sasa swali.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Maswali mawili, la kwanza, pamoja na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kumwagiza Mkaguzi wa Ndani kuwe kufanywa ukaguzi katika vijiji, huu utaratibu bado haufuatwi. Sasa Serikali au Wizara inachukua hatua gani kwa Wakurugenzi ambao wameshindwa kuwaagiza wataalam wa ndani kufanya ukaguzi kwenye vijiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wakati mwingine wananchi wanaposhinikiza kwa mfano, kwenye Kijiji cha Mkwara na Kijiji cha Mbureni Mwaivaro, wananchi wamefunga ofisi, kwa hiyo Mkurugenzi akalazimika kupeleka Wakaguzi na ubadhirifu ukaonekana lakini cha ajabu wahusika bado wanaendelea na kazi. Je, Serikali inachukua hatua au inatoa kauli gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la utendaji dhaifu la Watendaji wetu wa Vijiji kwenye Serikali za Vijiji kama ambavyo tumeweza kutoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri husika, linaendelea kuchukuliwa hatua kikamilifu, labda kama kuna mahali ambako hakuna utekelezaji wa aina hiyo, nako tutachukua



hatua kwa Wakurugenzi ambao hawajaweza kuchukua hatua hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukaguzi wa ndani unaofanywa kwenye vijiji vyetu ndiyo umepelekea kugundulika kwamba, ubadhirifu umetendwa na Mtendaji wa Kijiji. Pia kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anataka kujua hatua zinazochukuliwa, ni kwamba, Mkaguzi wa Ndani akishagundua tatizo anatoa taarifa kwa Mkurugenzi na Mkurugenzi anapaswa kuchukua hatua za papo kwa papo za kumfikisha kwenye vyombo vya sheria ili Mtendaji huyo aweze kupata hukumu ya vyombo hivyo vya kisheria.

Kwa hiyo basi, kwa kijiji ambacho tayari Mtendaji amebainika amefanya kosa na Mkaguzi wa Ndani amebaini na bado hawajachukuliwa hatua, maeneo hayo sasa tutalazimika kupata maelezo sahihi ya Mkurugenzi ya kwa nini hajachukua hatua baada ya Mkaguzi wa Ndani kuhakikisha kwamba Mtendaji wa Kijiji ametenda kosa, ili tujue kama alishapeleka kwenye vyombo vya sheria ambavyo ndiyo vinatoa hukumu dhidi ya mtendaji huyu na kwa adhabu ambazo zimetolewa. Iko mifano mingi ya Halmashauri kadhaa, tunazo Halmashauri mpaka saba sasa ambazo zimechukua hatua hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge nataka niwajulishe kwamba, wakati mwingine watendaji wetu wa vijiji wanashindwa kutoa mapato na matumizi kwenye vijiji vyetu kutokana na kukosekana kwa *quorum* ya Mikutano Mikuu ya Vijiji, unaweza kuita mkutano wa Kijiji lakini wanaokuja kwenye mkutano ule hawatoshi

kuendesha mkutano wa kijiji ambao kwa masharti yake lazima wawe wamezidi zaidi ya kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili tunalo katika maeneo mengi, lakini bado tutaendelea kuisitiza utendaji kazi na uwajibikaji wa watendaji hawa ili kusiwe na matatizo haya. Kwa kuwa sheria inatoa agizo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri sasa, kuwapeleka watendaji wetu kwa maana ya Wakaguzi wa Ndani kwenye Halmashauri kwa ukaguzi na wakishabaini, Wakurugenzi wote wachukue hatua stahiki za kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria watendaji hawa ambao si waaminifu au kuwachukulia hatua ikiwemo kusimamishwa kazi au kuwafukuza mahali pa kazi.

**MHE. CECILIA D. PARESO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, Watendaji hao wamekuwa na tatizo la kutokusoma mapato na matumizi, lakini Watendaji hao hao wamekuwa wakiwatoza wananchi fedha mbalimbali wanapokwenda kuhitaji huduma mbalimbali mfano, kuandikiwa barua za utambulisho katika taasisi mbalimbali jambo ambalo linawaongezea wananchi mzigo, nini kauli ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna maelezo ambayo yametolewa kwa Watendaji wa Vijiji kutoza tozo ya utoaji huduma mahali pake pa kazi. Mtendaji wa Kijiji ni mtumishi wa Serikali anayepaswa kufanya kazi yake wakati wote kuanzia tarehe moja mpaka mwishoni mwa mwezi na maslahi yake atayapata kutokana na kazi aliyoitenda kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi aliyopatia ajira.

Kwa agizo hili, kama itatokea Mtendaji yeyote kutoa tozo kwa mwananchi anapokuja kuomba huduma kwenye ofisi yake, jambo hili lichukuliwe hatua na yeyote atakayebaini eneo hilo wakiwemo Wakuu wa Vitengo hivyo na Waheshimiwa kama mnapata taarifa hizo hebu tuendelee kusimamia kwamba vijiji vyetu na watendaji wetu wanafanya kazi yao kadri inavyotakiwa. (*Makofi*)

Na. 55

### **Ukaguzi wa Chanjo za Wasafiri Mipakani**

**MHE. HAJI KHATIBU KAI** aliuliza:-

Katika mipaka ya nchi yetu kama vile Horohoro na kwingineko wapo Madaktari ambao hukagua chanjo kwa wasafiri wanaopita katika mipaka hiyo:-

Je, nini lengo la kuangalia chanjo hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatibu Kai, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Homa ya Manjano ni ugonjwa unaosababishwa na *Virus* ambao huenezwa na Mbu anayelitwa *Aedes*. Ugonjwa huu hauna tiba na ni hatari kwa kuwa unaweza kuua zaidi ya asilimia 50 ya wagonjwa. Aidha, ugonjwa wa Homa ya Manjano

unadhibitiwa kwa mtu kupata chanjo ambayo ni salama na inamkinga mtu kwa zaidi ya miaka 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa huu umeathiri sana nchi nyingi za Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa kuwa watu wanaendelea kusafiri kutoka nchi moja kwenda nyingine kupitia mipaka ya nchi yetu, maambukizi ya ugonjwa huu yanaweza kuenea kwa haraka katika jamii yetu endapo hatua za kudhibiti hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanjo ya homa ya manjano hutolewa kwa malengo makuu mawili:-

- (i) Kuchukua tahadhari ili kuzuia ugonjwa wa Homa ya Manjano usiingie nchini; na
- (ii) Kumkinga msafiri asipate ugonjwa huu hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, msafiri anayetakiwa kupata chanjo ya ugonjwa wa Homa ya Manjano ni yule aingiae nchini endapo:-

- (i) Atatoka katika nchi zilizo katika Ukanda wa Homa ya Manjano zilizopo katika nchi za Afrika na Amerika ya Kusini.
- (ii) Atakuwa amepitia na amekaa katika Uwanja wa Ndege wa nchi iliyo katika ukanda wa Homa ya Manjano, kwa kipindi kisichopungua saa kumi na mbili (12) kabla ya kuunganisha safari.

(iii) Atatoka nje ya Uwanja wa Ndege, akiwa anasubiri kuunganisha safari na kukaa muda wa chini ya saa kumi na mbili kabla ya kusafiri tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu imezungukwa na nchi zote ambazo zipo katika ukanda wa maambukizi ya ugonjwa wa Homa ya Manjano, ni vema tuchukue tahadhari ili ugonjwa huu hatari usiingie nchini. Wizara imeweka utaratibu wa kufuatilia magonjwa ya kuambukiza kwa kukagua wasafiri, vyombo vya usafiri na bidhaa zinazoingia na kutoka nchini katika mipaka yetu ukiwamo mpaka wa Horohoro. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa kila msafiri anayeingia nchini amekaguliwa kuona kama amechanjwa chanjo ya Homa ya Manjano kwa kukagua kadi ya Homa ya Manjano.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu wa kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Manjano ni utekelezaji wa Kanuni za Kimataifa za Shirika la Afya Duniani za mwaka 2005 (*International Health Regulations, 2005*) ambazo Tanzania ni moja ya nchi zilizoridhia.

**MHE. HAJI KHATIBU KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wasafiri wanaotumia mpaka wa Horohoro ni wengi, jambo ambalo linasababisha Madaktari waliopo kwenye mpaka huo watafute wasaidizi kwa raia wasio na taaluma hiyo na kwa kuwa raia hawa hupitisha watu kinyemela ambao hawana chanjo hiyo. Ni kwa nini sasa na kwa sababu ya nia njema ya jambo hili, Madaktari waliopo Horohoro, wasiongezwe kutoka wawili hadi wanne ili

kunusuru Taifa hili na kwa usalama wa raia wake kwa ujumla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna watumishi wawili, lakini naamini kabisa kwa utendaji wa kukagua chanjo, watumishi wawili wanatosha kufanya kazi hiyo. Pale ambapo itakuwa inaonekana hawatoshi kwa makusudio ya kuharakisha zoezi la wasafiri kupita, ni vyema na nawashauri na nawataka watoe taarifa Kituo cha Afya kilicho karibu ili waweze kupata mtaalam wa nyongeza kutoka kwa Mganga Mkuu aweze kuwasaidia kufanya kazi ambayo inatakiwa kufanywa.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa tunajua suala la chanjo ni muhimu sana kwa afya ya mwanadamu. Kwa kuwa tunajua kwamba Chanjo ya *tetanus* mara nyingi sana huwa wanapewa akinamama wanapokuwa wajawazito ili mradi kuwa na kinga ya ugonjwa wa *tetanus* na kwa kuwa tunajua kwamba ugonjwa wa *tetanus* unapompata mtu inakuwa ni tatizo kubwa sana. Je, Serikali ina mpango gani kuanzisha kampeni maalum kwa chanjo ya *tetanus* kwa akinababa ili mradi kuzuia tatizo hilo kwa upande wa wanaume.

**NAIBU WAZIRI AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, *Tetanus* kweli ni ugonjwa hatari na unazuilika kwa njia ya kutoa chanjo. Kwa kipindi kirefu tumekuwa tukitoa chanjo hasa kwa akinamama wajawazito kwa kusudio la kumkinga mtoto anayezaliwa kutopata chanjo wakati wa umri wa utoto. Kwa watu wazima, akinababa,

kwa kawaida chanjo hutolewa pale ambapo kunakuwa na hatari ya kupata ugonjwa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja katika njia ambayo mtu anaweza akapata *tetanus* ni pale ambapo atakuwa amepata jeraha, lile jeraha likawa halina usafi, likapata vimelea ambavyo vinaweza vikasababisha mtu kupata *tetanus*. Kwa kawaida chanjo hiyo hutolewa hata kwa akinababa, pale wanapokuwa wamepata majeraha.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza dhahiri athari kubwa za *Yellow Fever* na kwa kuwa hapa Tanzania kuna baadhi ya matapeli ambao wanatoa zile kadi na watu hawachanjwi, je Serikali inalijua hilo? Kama inalijua, inachukua hatua gani kwa sababu nimewahi kuona pale Mnazi Mmoja na hata *Airport* kuna vijana wanauza kadi kwa watu bila kuchanjwa. Je, Serikali inatoa tamko gani?

**NAIBU WAZIRI AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba kuna watu ambao hawana maadili mema, ambao wanavunja kanuni, lakini vile vile wanasababisha wao wenyewe au wanaosafiri kuwa katika hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wewe ni msafiri, unaamua kwa makusudi kupokea kadi ambayo wewe mwenyewe hujapata chanjo, cha kwanza wewe mwenyewe unajiweka katika hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa hatari.

Pili, unaweka hatari ya wewe kwenda kule unakokwenda na baadaye ukapata maambukizi na baadaye ukarudi nchini ukaleta ugonjwa huo nchini ambako hivi sasa hatuna. Kwa maana hiyo, tamko la Serikali ni kuwataka wale wote ambao wanatoa kadi bila mtu kupata chanjo waache mara moja na hatua stahili ziwe zinachukuliwa kwa watu wowote wanaonekana kufanya kitu hicho.

Na. 56

### **Taasisi Zinazosaidia Makundi Mbalimbali Nchini**

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS** aliuliza:-

(a) Je, ni Taasisi ngapi zilizosajiliwa nchini kwa madhumuni ya kusaidia makundi yenye mahitaji maalum kama walemavu, yatima, watoto wa mitaani na kadhalika?

(b) Je, Serikali inazisaidiaje na kuzisimamia vipi Taasisi hizo ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza yale yaliyokusudiwa na si vinginevyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mbunge wa Chonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na majukumu mengine, ina jukumu



la kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma kwa makundi yenye mahitaji maalum katika taasisi na kwenye jamii hapa nchini. Makundi hayo ni pamoja na watu wenye ulemavu, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, wakiwemo yatima, watoto wa mitaani na walio katika mkinzano na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi zinazotoa huduma kwa makundi hayo zinazosimamiwa na Wizara ni pamoja na Makazi ya watu wenye Ulemavu na Wazee wasiojiweza, Vyuvo vya Ufundi Stadi kwa watu wenye Ulemavu, makao ya watoto walio katika mazingira hatarishi, mahabusu za watoto na Shule ya Maandilisho.

Kuna jumla ya Taasisi 153 zilizosajiliwa, kati ya hizo 40 ni makazi ya watu wenye Ulemavu na Wazee wasiojiweza, sita ni Vyuvo vya Mafunzo Stadi kwa watu wenye Ulemavu, 100 ni makao ya watoto walio katika mazingira hatarishi, sita ni mahabusu za watoto na moja ni shule ya Maandilisho. Aidha, kati ya makao 100 yanayolea watoto walio katika mazingira hatarishi na jumla ya makao saba yanalea watoto wa mitaani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusaidia na kusimamia utekelezaji wa utoaji huduma katika Taasisi hizo, Wizara inatekeleza yafuatayo:-

Kuandaa Sheria, Sera, Miongozo na Kanuni zinazohusiana na utoaji huduma kwa makundi ya watu wenye mahitaji maalum; kufanya ufuatiliaji, tathimini na usimamizi elekezi katika utoaji huduma katika Taasisi hizo; kuzijengea uwezo wa kitaalam taasisi zinazotoa huduma

kwa makundi maalum ili kuboresha huduma zitolewazo; kutoa ruzuku kwa ajili ya uendeshaji wa taasisi hizo. Kutoa ushauri wa kitaalam na ushauri elekezi juu ya uendeshaji wa taasisi hizo; kuratibu misaada inayotolewa na wahisani mbalimbali kwa ajili ya makundi maalum; kuchukua hatua stahiki kwa taasisi zilizoshindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo ya Serikali.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dokta Seif Seleman Rashidi, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi juu ya huduma zitolewazo na Taasisi hizi, badala ya kutoa huduma zilizostahiki kwa walengwa, Taasisi nyingi katika hizi zimekuwa ni *income generating institutions* kwa wale wanaoziongoza. Je, Serikali inatathimini gani juu ya hilo?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali imesema kwamba, inachukua hatua stahiki kwa zile Taasisi zinazoshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ni hatua gani zilizochukuliwa, ukiondoa baadhi ya Taasisi chache ambazo zimefungwa, je, ni hatua gani zaidi zimechukuliwa juu ya Taasisi hizo, zinazoshindwa kutekeleza kanuni, sheria na taratibu za kuongoza vituo hivi, ili makusudio ya kuanzisha vituo hivi yaweze kupatikana?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna baadhi ya watu wanaweza wakawa wanatumia utaratibu uliopo kwa

kuanzisha Taasisi kwa madhumuni ya kutaka kuhudumia watoto walio katika mazingira hatarishi kwa kusudio la wao kujinufaisha. Siyo kitu na Serikali inapiga vita hilo, ndiyo sababu tumefanya uamuzi wa kuzisajili Taasisi hizo kwa makusudio. Kwanza, kuziangalia kama zinakidhi vigezo vya uendeshaji wa huduma inayotolewa.

Pili, kuweza kuona kama wanatoa huduma inayokusudiwa kutolewa kwenye eneo hili husika. Hatua ambazo zinatakiwa kuchukuliwa kwa Taasisi ambayo itakuwa inaendeshwa kinyume cha taratibu na kanuni zilizowekwa, ni pamoja na kuifungia, lakini viongozi hao, au mtu huyo ambaye amehusika katika uendeshaji wa Taasisi hiyo, tunaweza tukaendelea kuhakikisha kwamba hawezi kupata ruhusa ya kuanzisha Taasisi yenye makusudio kama hayo tena nchini.

Na. 57

### **Matabaka ya Mifumo ya Kutolea Elimu Nchini**

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE** aliuliza:-

Mfumo wa kutoa elimu hapa nchini una matabaka mbalimbali yanayotishia mustakabali wa umoja wa Taifa:-

(a) Je, kuna umuhimu gani wa Serikali kutenga Shule zake za Sekondari kama shule zenye vipaji maalum na za kawaida na huku sio kuendeleza ubaguzi?

(b) Je, vigezo gani hutumika kuifanya shule iitwe Akademia ya Kimataifa na hadi sasa kuna shule ngapi za aina hiyo za Sekondari na Msingi?

(c) Je, sababu gani hupelekea shule zinazoitwa *English Medium* kutumia vitabu vya kiada/ziada kutoka Kenya?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Shukuru J. Kawambwa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Vipaji Maalum au shule za wanafunzi wenye ufaulu mzuri zaidi ni shule za Serikali ambazo huchukua wanafunzi waliofaulu vizuri zaidi katika mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba na Kidato cha Nne. Nia ya kuwabaini wanafunzi hawa wenye vipaji maalum ni kuwapa fursa ya kujifunza kwa kasi inayolingana na uwezo wao; kuunganisha vipaji vyao kiakili ili kuwawezesha kubuni na kuvumbua mambo mbalimbali yakiwemo ya Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya maendeleo ya Taifa na kuwa shule za mfano katika maendeleo ya taaluma nchini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, vipo vigezo vinavyotumika kuifanya shule iitwe ya Kimataifa ambayo hutambuliwa na Taasisi za Kimataifa kama vile *European Council for International Schools (ECIS)* na *Association of*

*International Schools in Africa (AISA)*. Shule hizi hupewa usajili pale tu zinapotimiza vigezo vyote vilivyowekwa, ikiwa ni pamoja na mazingira stahiki kama vile kuwa na bwawa la kuogelea, mitaala tofauti kwa mfano mtaala wa *Cambridge*, mihula tofauti, wanafunzi na walimu kutoka Mataifa mbalimbali nchi za Nje. Shule za Awali zipo na Shule za Sekondari. Kwa ujumla wake tuna shule 18 katika nchi yetu za mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kufuatwa ili shule isajiliwe kuwa ya Kimataifa kwanza, Shule iwe imesajiliwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mwenye Shule aombe Wizara kimaandishi kutaka shule yake iwe ya Kimataifa. Endapo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itaridhia vigezo vilivyopo, itatoa kibali cha maandishi na mwenye shule ataendelea na hatua za kutuma maombi kwenye Taasisi kama vile *ECIS* na *AISA* zinazosajili shule hizo. Shule itakaposajiliwa kuwa ya Kimataifa, mwenye shule aijulishe Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kimaandishi na kuambatanisha nakala ya usajili huo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi hakuna utaratibu unaozuia vitabu vya ziada kutoka Kenya kutumika ilimradi maudhui hayakinzani na suala zima la utoaji wa elimu bora. Kwa upande wa vitabu vya kiada ni lazima viwe vimeidhinishwa na *EMAC* ya hapa nchini kwetu. Kama kuna shule inatumia mitaala au mihtasari ya Kenya, natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge watusaidie kutupatia taarifa hizo ili tuweze kukagua na tuweze kuchukua hatua stahiki.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa

Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama lengo ni kuendeleza vipaji, katika nchi yetu ya Tanzania, ni kwa nini Serikali isijenge Shule za aina hii kwa kila Mkoa, pamoja na kuifanya Shule ya Tarime kuwa shule ya Vipaji Maalum?

Swali la pili, kwa nini Taasisi ya Elimu isipewe jukumu la kutunga vitabu vya kiada na ziada ambavyo vinatumika katika shule hizi za *English Medium*?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, anaomba hizi shule za vipaji maalum zijengwe kwa kila Mkoa. Ni kweli, hapo zamani shule hizi zimejengwa au zilijengwa Kikanda, ukienda kule Magharibi utakuta kuna Tabora *Boys* na Tabora *Girls*, ukienda Mashariki kule kuna Kilakala na Kibaha, ukienda kule Arusha kuna Ilboru na ukienda Dodoma kuna Msalato.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili labda tuliangalie tena upya ili tuweze kuona namna tunavyopanua shule zetu ngazi ya Kata, kama tunaweza tukalifanya na hili likawa la Kimikoa zaidi. lakini tunashukuru kwa mawazo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, Taasisi ya Elimu Tanzania ndiyo itunge vitabu hivyo pamoja na wadau wengine hapa nchini kuliko labda kuchukua vitabu vya kiada kutoka Kenya. Kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi kwamba, vitabu vya kiada na hasa kwa

masomo ya msingi kama Kiingereza, unaweza bado ukasoma kitabu cha Kenya kilichoandikwa Kiingereza vizuri bado ukafaidika, au unaweza kusoma kitabu cha *Mathematics* au *Physics* au *Chemistry* hata kutoka Marekani ilimradi hoja ni ile ile, lakini vile vya kiada lazima vitungwe na Taasisi ambayo imepewa mamlaka ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, ana kampuni ya kutunga vitabu, tushirikiane kwa pamoja kwa sababu sheria ilisharuhusu na wadau wengine kutunga vitabu, alete nakala za vitabu vyake tuvione kama vinafaa tutamruhusu aweze kutunga vitabu hapa nchini wala hatuna matatizo.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho la nyongeza, nilikuona Mheshimiwa Mchungaji Peter S. Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa hizi shule zinazoitwa za vipaji maalum, wanafunzi wanaokwenda kule wengi wao ni wale ambao wanaonekana wamefanya vizuri kwenye mitihani, lakini dhana nzima ya vipaji inapotea kwa sababu kwa Kingereza, vipaji ni *talent*, ni watu ambao wako *talented*, wako *gifted*, wanaonesha vitu vingine ambavyo watu hawana.

Je, ni tija gani ambayo imeonekana kwa Taifa na ni kwa nini tunatumia vipaji maalum wakati vipimo vinavyotumika kuwaita wenye vipaji maalum haviendani na dhana nzima ya kuitwa watu wenye vipaji maalum?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kukubaliana naye sana moja kwa moja kwamba, shule hizi za vipaji maalum hazina faida kwa Taifa hili na Waheshimiwa wengi Wabunge hapa watakubaliana na wengi wamesoma kwenye shule hizo. Hata Mheshimiwa Julius K. Nyerere alisoma Tabora *Boys* na alikuwa ni mwanafunzi mzuri sana wa vipaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali kuweka shule hizo za vipaji maalum kama nilivyosema, ni kuwaunganisha vijana ambao wako *talented*, ili waweze kuungana kiakili pamoja, waweze kuvumbua mambo fulani na wamevumbua vitu vingi sana ambavyo mpaka sasa hivi tunaendelea kutumia *materials* hayo kwa ajili ya shule nyingine za sekondari kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale vijana tunapowaweka pamoja, mwaka jana hapa tumetoka kuwapa vijana zawadi, vijana 20 ambao wengi wametoka kwenye hizo shule za Msalato, Tabora *Boys*, Ilboru, wanafanya vizuri sana na wengine wakishafanya vizuri wanapelekwa mpaka nchi za nje kwenda kufanya mitihani na wanafaulu vizuri na kulipa heshima Taifa letu.

Na.58

**Michango ya Walimu kwenye Chama  
cha Walimu (CWT)**

**MHE. WARIDE BAKARI JABU** aliuliza:-



Walimu wa Shule za Serikali wamekuwa wakichangia katika Chama cha Walimu (CWT) kila mwezi:-

Je, ni walimu wangapi wapo chini ya CWT na wanachangia kiasi gani kwa mwezi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Walimu Tanzania (CWT) ni Muungano au Umoja wa Walimu Tanzania Bara wanaofanya kazi katika Shule za Awali, Msingi, Sekondari, Vyuvo vya Ualimu, Ofisi za Elimu, *TSD* na Ukaguzi wa Elimu, Wilaya, Mkoa na Wizarani pale Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara yangu za mwaka 2012, jumla ya Walimu katika Shule za Awali, Msingi, Sekondari, Vyuvo vya Ualimu, Ofisi za Elimu, *TSD*, Ukaguzi wa Elimu Wilaya, Mkoa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, jumla ni Walimu 226,176 wanaolipa fedha hizo CWT. Walimu hawa siyo wote wanaochangia asilimia mbili ya mishahara yao katika Chama cha Walimu Tanzania kutokana na sababu mbalimbali, vifo na kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, Walimu wanaochangia asilimia mbili kati ya 226,176 ni walimu 185,102 ambapo kiasi

cha Shilingi bilioni 2.2 hukusanywa kila mwezi kupitia Hazina kutoka kwenye mshahara wa kila mwanachama yaani Mwalimu. Aidha, idadi ya wanachama hubadilika kutokana na sababu mbalimbali kama vile kustaafu, kufariki, kuacha kazi au kufukuzwa.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Walimu hawa wanakuwa wanachangia karibu shilingi bilioni 2.2 alizotueleza kwa mwezi na kwa kuwa kuna Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekuwa inachangiwa na wanachama wake na wanafaidika baada ya kustaafu, nilikuwa nataka kujua, je, Walimu hawa wanafaidika vipi na michango yao hii baada ya kustaafu?

Swali la pili, michango hii ni jasho la Walimu, je fedha hizi zinakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Mbunge ameuliza faida ya hizi fedha zote ambazo Walimu wanachangia CWT, zinawafaidisha vipi na hasa baada ya kustaafu ama kufariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya CWT kama ilivyo, kama nilivyosoma kwenye vitabu vyao na miongozo na sheria zao, sheria namba sita (6) ya mwaka 2004, wanasema, fedha zile zinazokusanywa kazi yake itakuwa ni

kulinda maslahi na kutetea maslahi ya wanachama wenyewe wakati wakiwa kazini. Haijasema baada ya hapo kinachoendelea ni nini.

Vile vile kuna kesi mbalimbali za Walimu, kuna migogoro kama mnayoiona ya CWT, unakuta ndiyo wanatumia fedha hizo *unless otherwise* kama Waheshimiwa Wabunge mnaweza mkafanya *amendment* ya Sheria ya CWT, lakini kiujumla haijaelezea kule mbele Mwalimu mafao yake ni nini baada ya kustaafu ama baada ya kufariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa anataka kujua kama fedha hizi kwa sababu ni fedha za Walimu walioajiriwa na Serikali, je, zinakaguliwa na CAG? Sheria bado ni vilevile, kwamba CWT hawakaguliwi na CAG, bali hesabu zake hukaguliwa na Mtaalam wa masuala ya ukaguzi aliyeteuliwa na CWT na *report* hiyo inapelekwa kwa Msajili wa Vyama.

**NAIBU SPIKA:** Naomba twende mwisho kabisa kule, nadhani nilimwona Mheshimiwa Rita E. Kabati.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa yapo malalamiko makubwa sana kutoka kwa Walimu kukatwa 2% zao mara tu wanapojiriwa na Hazina. Je, ni kwa nini hii inatokea kwa Walimu wetu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningepomba Mheshimiwa Rita E. Kabati aulize tena swali lake, ili niweze kulisikia vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati uliza tena swali lako Mheshimiwa Waziri hajalipata vizuri.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko makubwa sana kwa Walimu kukatwa 2% na Hazina mara tu wanapoajiriwa bila ridhaa yao, naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Suala hili ni kweli linajitokeza mara kwa mara na ni kweli hata Walimu wanapofanya vikao vyao na tunapofanya ziara tunalikuta hilo, najua hata Waziri wa Kazi na Ajira naye tulikuwa tunawasiliana naye pale linatukuta kwamba, Walimu wanapoajiriwa *first appointment*, mwezi wa kwanza ule ule unakuta asilimia mbili imeshakatwa na Hazina hata bila ya ridhaa yao na hata wengine wanakuwa hata hawajajaza fomu hata hawajui CWT ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala ni kweli lakini nimejaribu sana kujitahidi kutafuta sheria ile ile, tena Sheria namba sita (6) ya mwaka 2004, kule mbele mwishoni inamalizia kwamba, Chama cha Walimu kwa sababu kimeshavuka asilimia 50 ya wanachama wake, kwa hiyo, *automatically*, mwanachama yeyote anapokuwa tu ni Mwalimu, basi anapoanza kazi *automatically* anakatwa ile asilimia mbili, ndivyo sheria ilivyo.

Ndiyo maana nimesema Waheshimiwa Wabunge kidogo sheria hizi zinakinzana, *unless otherwise* kama bado tunaweza kuzifanyia *amendments* lakini wanacholalamika walimu ni kweli, lakini vile vile sheria inabana hivyo hivyo

kwamba, lazima iendelee kukatwa kwa sababu wameshazidi asilimia 50 ya wanachama wote Tanzania Bara kwa sababu ndiyo chama kikubwa chenye watumishi wengi hata ukienda kule Halmashauri.

Na. 59

### **Kukiboresha Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chala**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chala kinakabiliwa na matatizo mengi ikiwemo kuchakaa kwa majengo, ukosefu wa walimu, ukosefu wa vifaa vya kufundishia pamoja na kukosa kabisa chombo cha usafiri:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiboresha Chuo hiki kwa kukikarabati na kukipatia gari?

(b) Kwa kuwa Wilaya ya Nkasi haina Chuo chochote cha Ufundi, je, ni lini Chuo hiki kitapandishwa hadhi na kuwa Chuo cha Ufundi (*VETA*)?

**NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kuviboresha Vyu vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*) kwa kuvikarabati, kuvipatia watumishi na vyombo vya usafiri kwa awamu kutokana na bajeti ndogo itolewayo kwa Wizara. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Chala kilifanyiwa ukarabati mdogo wa majengo ya utawala na madarasa mwaka 2002/2003 na kiliwekewa mfumo wa umeme wa jua mwaka 2010/2011.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 iliagiza kuwa, kila Wilaya iwe na Chuo cha Ufundi Stadi ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana. Katika kutekeleza hili Serikali iliamua kwamba Wilaya ambazo hazina Vyu vya Ufundi Stadi, Vyu vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*) viimarishwe ili viweze kutoa mafunzo ya ufundi stadi sanjari na elimu ya wananchi inayotolewa kwa sasa.

Kutokana na hilo, Wizara yangu imeshaanza kutoa mafunzo ya Ufundi Stadi katika Vyu vya Maendeleo ya Wananchi 25, kikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Chala. Mafunzo haya yameanza kutolewa rasmi mwezi Januari, 2013 na tayari Wizara yangu imewapatia Wakufunzi wa Vyu hivi, mafunzo ya kufundisha kozi za ufundi stadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara yangu imetuma kiasi cha sh. 25,261,972/= kwa ajili ya chakula cha wanachuo Chala na sh. 6,000,000/= kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kila chuo. Vile vile kiasi cha sh. 8,000,000/= zimepelekwa chuoni kwa ajili ya kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia, pia tumeweza kupata vitanda 50

na magodoro 50 ambayo Mzabuni ameshaanza kusambaza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza niipongeze Serikali kwa majibu mazuri kuhusu chuo hiki, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Chuo cha Chala kimezalisha vijana wengi ambao wametusaidia sana hata katika ujenzi wa Sekondari na Shule za Msingi na kwa hakika ni kusaidia katika kupunguza tatizo la ajira nchini, lakini sasa hivi kina Mwalimu mmoja tu na Mwalimu huyo anastaafu mwezi wa sita. Naiomba Serikali ifanye jitihada za haraka kuhakikisha kwamba chuo hiki hakifungwi na tunapata Walimu wa kutosha ili kuendeleza nia njema ambayo ilikusudiwa kwa Chuo hicho.

Swali la pili, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri, inaonesha kwamba katika suala la kushughulikia usafiri litatolewa kwa awamu, naiomba Serikali, kutokana na umuhimu wa chuo hiki na ukizingatia Wilaya ya Nkasi yote haina chuo chochote cha ufundi, tuwe wa kwanza kufikiriwa katika suala zima la usafiri ili kuweza kutoa huduma kwa upana Wilaya nzima. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba, tuko katika maboresho ya Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo 25 viko katika mpango huo, kwa hiyo, moja wapo ya kitu ambacho kinafanyika ni kupeleka Walimu wenye ujuzi na uwezo wa kuweza kutoa mafunzo

ya *VETA*, kwa hiyo, nina hakika kabisa tukienda chuoni sasa hivi tutakuta suala hilo limetatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usafiri, ni kweli nikiri kwamba, tuna matatizo, lakini pia ni katika mpango huo huo wa maboresho ambapo tumepata pesa kutoka *SIDA* Canada. Tunaamini pia suala la kutatua usafiri katika vyuo vyetu tutalimaliza kadri bajeti itakavyoweza kuruhusu na tutakufikiria kama ulivyosema katika zile *priority areas*. Ahsante sana.

Na.60

### **Kukomesha Mauaji ya Watu wenye Ulemavu wa Ngozi**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR** aliuliza:-

Watu wenye ulemavu wa ngozi (*Albino*) wameripotiwa kuuawa tangu mwaka 2007:-

(a) Je, hadi leo ni watu wangapi wenye ulemavu wa ngozi wameuawa na wangapi wamejeruhiwa?

(b) Je, mauaji haya hutokea kwenye Mikoa gani zaidi?

(c) Je, Serikali ina mipango gani endelevu ya kukomesha uonevu huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo haramu vya mauaji ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi (*Albino*) kwa imani za kishirikina vilianza kushamiri kuanzia mwaka 2007. Vitendo hivi kwa kiasi kikubwa vinaendelea kudhibitiwa na kupungua mwaka hadi mwaka. Takwimu zinaonesha kuwa jumla ya walemavu wa ngozi 36 wameuawa na nane kujeruhiwa katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Tabora na Geita.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji hayo yalitokea zaidi katika Mikoa ya Mwanza, Kigoma na Shinyanga.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na mikakati mbalimbali ya kukomesha tatizo hili kwa kuwachukulia hatua za kisheria na kuwakamata watuhumiwa na kuwafikisha Mahakamani. Aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuondokana na imani potofu zinazochangia mauaji hayo kwa kushirikiana na Taasisi za Kidini na Asasi za Kiraia katika jitihada hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi wa Polisi Jamii na vikundi vya ulinzi shirikishi katika Mitaa, Vitongoji na Vijiji vyenye walemavu hao, ulinzi umeimarishwa kwa kusaidiana na wadau wengine wakiwemo Makampuni ya Simu za Mkononi ambayo yamekuwa yakitoa simu kwa walemavu ili

kurahisha mawasiliano wanapokuwa katika mazingira ya kuhatarisha maisha yao.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake na naishukuru Serikali kwa jitihada zake kubwa za kulishughulikia tatizo hili, lakini naomba kuuliza yafuatayo:-

Kwa kuwa mbali na Serikali kuchukua hatua za kisheria za kuwakamata wahalifu hawa, lakini wanawakamata, hukumu huwa hazitolewi kiharaka na hasa wengine wanaonekana wana vifaa vya kuulia, damu zimewachirizikia, wanakamatwa na wanakutwa mpaka na maumbile ya binadamu, mfano vichwa, mikono na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakikamatwa kinachoshangaza ni kwamba, hukumu hazitolewi kwa haraka, kitu ambacho kinatumiza sana sisi wananchi na kinatuvunja moyo. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa wakati umefika wa Serikali kuchukua hatua ya haraka ya kutoa hukumu kwa wahalifu hawa?

Swali la pili, kwa kuwa ni hivi juzi tu tumekiona kichanga kisichokuwa na hatia kimeuliwa, nafikiri itakuwa ni Mkoa wa Tabora nimeona kwenye TV na wamekamatwa wahusika, naomba kujua Serikali imefikia hatua gani ya kufanya uchunguzi wa haraka ili wahalifu wale wafikishwe Mahakamani na kuchukuliwa hatua? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria na Waziri wa Mambo ya Ndani, ninapendakujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida Bakar, ambaye ametaka kujua kwamba Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hukumu zinatolewa haraka.

Serikali haicheleweshi kutoa hukumu kwa makusudi, kesi inapokuwa imechelewa kunakuwa na sababu za msingi. Unakuta wakati mwingine labda shahidi hajajitokeza au wapelelezi na kila mara Serikali imekuwa ikijitahidi kwa kadri inavyowezezana kuharakisha upelelezi na usikilizaji wa kesi. Lakini kama kuna sababu za msingi na ana ushahidi wa kesi ambayo labda ameona imekuwa ikicheleweshwa kwa makusudi basi atupatie taarifa ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Lakini pili, kuhusiana na upelelezi wa muuaji wa mtoto huyu kichanga wa Tabora, utawala wa sheria upo na unafuatwa na hata siku moja Serikali haijaka kimya kumwacha mtu ambaye amefanya makosa ya jinai kutembea bila kuchukuliwa hatua.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sambamba na mauaji ya Albino, kumetokea na mauaji ya kutisha katika Mkoa wa Mara akina Mama wamekuwa wakikatwa vichwa hasa katika Wilaya ya Butiama na Musoma Mjini. Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa imeonyesha kushindwa kudhibiti hali hii kwa sababu inaendelea, na ni majuzi tu ameuawa Mama mmoja kwa kunyongwa na kutupwa kisimani katika Kata ya Boari.

Ni nini kauli ya Serikali kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mara?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Vincent Nyerere wa Musoma Mjini kama ifuatavyo:-

Tatizo hili la mauaji tumeshalipata na mbali na kuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama inaendelea kulifanyia kazi lakini linapotokea kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama ikielelemewa na Jambo taifa huwa linateua Kamati ya Kitaifa ili kulishughulikia. Suala hili lipo miongoni mwa mambo ambayo Kamati ya Taifa yaani *Task Force* inashughulikia na majibu tutayapata karibuni.

Na. 61

### **Muda wa Askari Kustaafu**

**MHE. VINCENT J. NYERERE** aliuliza:-

Je, ni kigezo gani kinatumika kuongeza muda wa Askari Polisi kustaafu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali moja la

Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 14 Julai, 2010 Bunge lako Tukufu lilifanya mabadiliko ya kifungu Na. 9 na 10 cha Sheria ya hitimisho la ajira kwa watumishi wa Umma sura Na. 371 (*The Public Service Retirement Benefit Act, Cap. 371*) na kuongeza umri wa kustaafu kwa Askari wa Vyeo vya Konsebo, Koplo na Sajini wa Polisi. Vigezo vifuatavyo vilizingatiwa katika kuongeza muda wa Askari kustaafu:-

(a) Wabunge wengi walisema sana humu Bungeni kwamba umri wa kustaafu usogezwe mbele. Aidha, Askari wengi walikuwa wanatoa maombi ya namna hiyo.

(b) Ilibainika kwamba kuwabakisha Jeshini Askari wa Vyeo vya chini wenye uzoefu na weledi ingeleta na kuongeza ufanisi.

(c) Kupunguza pengo la upungufu wa Askari kwa kuzingatia uwiano wa Polisi na wananchi waliokuwepo (*Police - Population Ratio*).

(d) Ongezeko la umri wa kuishi (*Life Expectancy*) ambalo limefanya baadhi ya Askari wanaostaafau waonekane bado wana nguvu ya kutosha kuendelea kulitumikia taifa.

(e) Kubadilika kwa mbinu za utendaji wa Polisi ambapo kwa sasa ushirikishwaji wa Jamii unahitajika zaidi kazi ambayo inahitaji Askari wenye uzoefu, motisha, weledi na waliokomaa katika huduma ya Polisi.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla ya mabadiliko ya tarehe 14 Julai, 2010 wapo Askari ambao walistaafu lakini bado wana uwezo. Je, Serikali ipo tayari kuwarudisha kazini kwa sababu tayari Waziri amekiri kwamba kuna upungufu kwa kuzingatia uwiano wa Polisi na wananchi yaani *Police Population Ratio*, sambamba na kuwaajiri vijana wengine?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Nyerere, kama ifuatavyo:-

Wazo lake nafikiri ni moja katika *options* ambazo tunaziangalia katika kuondoa tatizo la upungufu au kurekebisha ratio ambao ipo kati ya Askari na Raia. Hata hivyo, bado ni mambo ambayo yapo kwenye meza ya mazungumzo na majadiliano nafikiri tukikubali baada ya kutazama faida na hasara yake tunaweza tukalichukua na moja ikawa na yeye ameshachangia mawazo katika kuboresha ulinzi wa wananchi.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa vile kwenye jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba moja ya sababu zilizofanya umri wa Askari kustaafu uongezwe ni pamoja na ongezeko la umri wa kuishi yaani *life expectancy*.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akalieleza Bunge hili kwamba hii *life expectancy* imeongezeka kwa kiasi gani? Ongezeko la umri wa kustaafu ni kiasi gani ili tuweze kulinganisha?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tundu Lissu kama ifuatavyo:-

*Life expectancy* au umri wa kuishi kwa Tanzania umeongezeka kutoka miaka 51 mpaka hivi sasa kwa takwimu tulizokuwa nazo za mwaka 2012 kuwa ni miaka 55.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Mwijage, kwa niaba yake.

Na. 62

### **Ununuzi wa Mazao ya Wakulima Nchini**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (K.n.y. MHE. MARY P. CHATANDA)** aliuliza:-

Wakulima nchini wamekumbwa na matatizo makubwa katika ununuzi wa mazao yao kama Mahindi, Korosho, Pamba na kadhalika:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha mazao ya wakulima yananunuliwa bila ya wananchi kufikia uamuzi wa kuandamana kuchoma moto vituo vya Polisi na kukosa imani na Serikali yao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka uwiano wa Kilimo na Viwanda kwa ajili ya kuwanusuru wakulima

husunani kundi la vijana na wanawake kama sehemu ya kujiinua kiuchumi na ajira rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha mazao ya wakulima yananunuliwa kwa utaratibu maalum na hivyo kuwanufaisha wakulima nchini. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kununua mazao hususan Mahindi na Mtama na mazao mengine ya nafaka kupitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*).

(ii) Kuanzisha Bodi ya Nafaka na mazao mchanganyiko yenye jukumu la kununua mazao ya nafaka (Mahindi, Mtama na Mchele) kwa bei ya ushindani/soko.

(iii) Kuruhusu wafanyabiashara kununua na kuuza mazao ya wakulima katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali vilevile inasimamia mifumo na taratibu mbalimbali za ununuzi wa mazao ya



wakulima. Kwa mfano zao la Korosho, linatumia mfumo wa Stakabadhi za mazao ghalani ambao umeanza kutumika tangu msimu wa mwaka 2007/2008 hadi sasa. Utaratibu uliopo katika zao la Pamba ni kutumia wafanyabiashara binafsi kwa usimamizi wa Serikali ambapo wadau wote hukubaliana kuhusu bei dira ya Pamba kwa msimu husika.

Aidha, utaratibu uliopo katika zao la Kahawa ni wakulima kupitia vyama vya ushirika na vyama vya wakulima kuuza kupitia mnada wa kimataifa wa Moshi pamoja na mauzo ya moja kwa moja (*Direct Sales*) kwa Kahawa ya kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni kupitia utaratibu wa kilimo cha mkataba na utaratibu wa kuwashirikisha wakulima wadogo na mwekezaji mkubwa (*Outgrower Schemes*) ambapo kupitia utaratibu huo mkulima anahakikishiwa soko la mazao yake na kuwezesha kupata pembejeo kama mbegu bora, mbolea, zana bora za kulimia na kuvunia, madawa ya kuulia wadudu waharibifu na utaalum wa kilimo cha kisasa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao yenye kuongeza tija, unaoambaana na uongezajiwa thamani ili kuleta uwiano wa kilimo na viwanda kwani usindikaji wa mazao una uwezo wa kuwa na mchango mkubwa kwa kuongeza mapato ya wakulima na utachangia ajira na ustawi wa jamii yua wananchi wetu na kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo kwa kuboresha, miundombinu ya usafiri, mfumo wa kodi na kuongeza upatikanaji wa nishati ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya viwanda vya mazao ya na kutoa elimu kwa umma hususani kwa makundi ya vijana na wanawake juu ya mfumo huu wenye tija zaidi ya uzalishaji. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Tumekuwa na tatizo la muda mrefu la uendeshaji wa sekta ya Korosho na hasa hasa upande wa masoko na Serikali kwa makusudi mazima iliamua kujitoa kwenye shughuli.

Kwa kuwa, soko la Korosho lipo Amerika na Ulaya, kwa nini sasa baada ya Serikali kugue kwa makusudi kurudi katika shughuli ili iendeshe uchakataji na uuzaji wa zao la Korosho Amerika na Ulaya walipo wateja badala ya kuwatumia hao watu wanaopeleka Korosho Bara Hindi?

Pili, ni jukumu la Serikali kusimamia Taasisi ambazo zimesajiliwa ndani ya nchi hii au kuendesha shughuli. Kwa kuwa, *Tanzania Coffee Board* na *KNU* ya Kagera zimekuwa zikiendesha shughuli zake katika hali ambayo inawaumiza wananchi kufikia katika hali ya kuandamana kama alivyoeleza mwuliza swali la msingi. Kwa nini sasa Serikali isitamke kwa mambo yanayojulikana bayana kwenye *KNCU* na *Tanzania Coffee Board (TCB)* kwamba matatizo hayo itayaondoa mara moja na haraka badala ya kuingia kwenye mchakato usioisha?

## **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwijage kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la soko la Korosho lina *complications* kidogo kwa sababu mtuamiaji mkuu wa Korosho duniani ni Marekani, China na kadhalika na kwa soko la Korosho ambazo zimeshabanguliwa soko kuu ambalo manunuzi makubwa yote yanakwenda ni kupitia India, kidogo kuna ubanguaji unaofanyika Brazil kwa Korosho inayozalishwa Brazil na Korosho inayotoka Ivory Coast na kanda ile ya Senegal na nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado Korosho kwa kiasi kikubwa inabanguliwa India.

Sasa tatizo tulilokuwa nalo ni kwamba Korosho ya Tanzania ndiyo Korosho *premium* duniani, lakini hatujaifanyia *branding* na hatujaifanyia *branding* kwa sababu kwenye hali ya kukandamiza hii hali ya Korosho kuna maslahi kwa watu wengi ambayo inawakandamiza wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka jana tumeiagiza *Board* kwa makusudi kabisa kwamba kwa kupitia mfumo huu wa stakabadhi ghalani, mkulima anaweza akapata bei inayofanana na bei ya soko kwa kulingana na Korosho zinavyokwenda duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini humohumo kuna vikwazo vimetokea na matatizo yaliyojitokeza. Kwa hiyo, tunasema Serikali imejipanga kwa kupitia Bodi na kwa

kupitia Mfuko wa Maendeleo ya zao la Korosho kukabiliana na tatizo hili. Lakini tatizo la Korosho halitamalizika mpaka tupate ufumbuzi wa kubangua na hivyo tumejielekeza kwenye Serikali kutengeneza mkakati wa makusudi wa kuwawezesha na kuwapa vivutio wabanguaji ili waweze kubangua korosho nchini. Hapo tutapata nafasi ya kubangua, kuongeza thamani na kupeleka moja kwa moja kwenye masoko makuu ya dunia ya Korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la Korosho kwamba kuna migogoro kati ya *Coffee Board* na *KCU*, *KCU* ni Chama cha Ushirika cha Kagera, tatizo lililokuwepo lilitokana na masuala ya uchaguzi na uongozi na kuna matatizo kidogo ambayo yamekuja kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na yamekuja kwangu pia, tumeyafanyia kazi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amekwenda Bukoba amekutana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tatizo ni kubwa na kusema kweli inabidi tulifanyie kazi ikiwa ni pamoja na kuangalia kama uongozi pia wa Bodi ya Korosho unaweza ukasimamia vizuri suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa hili naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna haja ya kuandamana na kufanya vitendo vingine vya ajabuajabu kwani Serikali tunalifanyia kazi na tutapata ufumbuzi wa suala hili haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kwa kuwa, swali limejikita kwenye Korosho, basi niwape Wabunge Wawili Mheshimiwa Mbunge wa Liwale na Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru. sasa tuanze na wa Liwale!

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, wakulima wa Mkoa wa Mtwara, Lindi na Wilaya ya Tunduru mpaka sasa hivi wameshindwa kuuza Korosho zao na Korosho hizi zimejaa kwenye Maghala.

Serikali inatamka nini juu ya wakulima hawa wa Mkoa wa Mtwara na Lindi na Wilaya ya Tunduru juu ya Suala hili la ununuzi wa Korosho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Faith Mtambo, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba zao la Korosho mwaka huu limekabiliana na tatizo kidogo kubwa na tatizo lenyewe wote tunafahamu kwamba limeanzia kwenye mgogoro ulioingia kwenye usimamizi wa Vyama vya Ushirika na mfumo mzima wa stakabadhi ghalani mwaka jana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa maana kwamba mwaka huu vyama vya ushirika vilishindwa kudhaminika kupata pesa kutoka kwenye benki ili kununua Korosho mapema. Tulichofanya kama Serikali tumeongea na benki, zimejaribu kuchagua kutenga vyama vya ushirika ambavyo vimeonekana vinaweza kukopesheka. Lakini pia tumeingia mgogoro kwenye wanunuzi wa zao hilo la Korosho, tulikuwa

tumekubaliana bei dira lakini baadaye wenyewe wakatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda tukubaliane tu kwamba kwa sasa hivi tumeiagiza Bodi kwamba ipitie upya watu wote waliopewa leseni ambao wanaonekana kwamba wanafanya mchezo na hili soko ili hizi leseni tuziondoe.

Halafu ikibidi tutoe leseni mpya kwa watu watakaofuata utaratibu huu wa kununua Korosho kwa maagizo kama ya Serikali kwa sababu haiwezekani tunakupa leseni halafu wewe unampa leseni mtu mwingine anakwenda kununua Korosho Mkuranga, Rufiji au Liwale kwa shilingi 400/= badala ya shilingi 1200/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wadau wenzangu wote wa Korosho kwamba jambo hili linafanyiwa kazi kwa uti na uvumba ili tupate namna ya ufumbuzi wa haraka ambao utakuwa na maslahi kwa wakulima. *(Makofi)*

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 ilieleza bayana kabisa kwamba moja ya mambo ambayo Serikali itaifanyia Wilaya ya Tunduru ni kutafuta masoko ya uhakika na bei ya uhakika ya zao la Korosho. Bahati nzuri, sera hii au ilani hii ya Uchaguzi ni endelevu tofauti na kujenga daraja kwani ukishajenga Ilani imeshakamilika. *(Makofi)*

Je, Serikali ina habari kwamba Korosho za wananchi wa Tunduru ambapo Serikali iliahidi wananchi wa Tunduru kwamba itawatafutia soko la uhakika na bei ya uhakika leo hii Korosho zile zinauzwa shilingi 500/= mpaka shilingi 1000/= wakati bei elekezi ni shilingi 1200/=?

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Tunduru?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdalloah Mtutura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati najibu swali la Mheshimiwa Faith Mohamed Mtambo, nilisema kwamba bei elekezo ni shilingi 1200/= na hii bei elekezi haitolewi kienyejenyeji tu bali imefanyiwa kazi na wanunuzi tumeshirikiana nao katika kupata hii bei elekezi na tumekaa kwa pamoja tumekubaliana kwamba bei elekezi itakuwa hii.

Hao wanaokwenda kununua Korosho kwa shilingi 500/= wanafanya hivyo Tunduru, Liwale, Rufiji na kadhalika. Lakini wanachofanya kusema kweli hii ni dhuluma, hakuna sehemu ambayo Serikali inasema tunakubaliana na bei hii. Hii ni dhuluma na ni wizi unaofanywa kiujanjaujanja na baadhi ya wafanyabiashara kutumia mawakala ambao ni watu sehemu ya wananchi wetu katika maeneo ya Tunduru na huko kwinghine nilikokutaja. *(Makofi)*

Sasa naomba niseme, nimelisema awali, naomba niliseme tena kwamba tatizo la bei ya uhakika ya korosho

linaanzia kwenye mfumo wa sisi wenyewe kule chini kwenye Vyama vya Ushirika mpaka huku juu kwenye wanunuzi.

Tumeiagiza Bodi, sisi Serikali, watu wote, wadau na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa maeneo yanayolima Korosho tusimamie jambo hili ili tufikie hatua ambayo sasa wanunuzi hawa na mawakala wao wanaokwenda kununua Korosho kwa Tsh. 500 huko vijijini kwetu wasipate nafasi kwa sababu wanawakandamiza wananchi wote wa zao la korosho ikiwa ni pamoja na hawa wananchi wa Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie wadau wenzangu wa Korosho kwamba tunalifanyia kazi na tutalipatia ufumbuzi wa kukomesha tabia hii.

Na. 63

### **Sheria ya Tumbaku Nchini**

**MHE. JUMA S. NKUMBA (K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Mwaka 2008 nchi iliridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kudhibiti matumizi ya bidhaa zinazotokana na zao la Tumbaku na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nazo zimeridhia Mkataba huo:-



Je, ni kwanini sheria ya Tumbaku ya mwaka 2003 haifanyiwi mabadiliko kulingana na Mkataba huo wa Umoja wa Mataifa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa sasa wa Serikali kuhusu matumizi ya Tumbaku ni: Zalisha tumbaku lakini usitumie (*produce but don't use*). Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2001 pamoja na marekebisho ya mwaka 2009 (*Cap. 202, RE*) inahimiza uzalishaji kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira na afya ya binadamu ambayo inasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Aidha, sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku na Bidhaa zake ya mwaka 2003 inapiga marufuku matumizi ya tumbaku au bidhaa zake katika maeneo ya umma (*public places*) pamoja na kuzuia watoto kujihusisha na matumizi na kutumika katika matangazo ya aina yoyote ya bidhaa za tumbaku. Sheria hii inasimamiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maazimio ya Mkutano wa mwezi Novemba, 2012 uliofanyika nchini Korea kujadili suala

la matumizi ya bidhaa zinazotokana na tumbaku na mazao mbadala kwa tumbaku yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuwepo kwa muda wa kutosha kwa kila nchi kutafuta namna ya kutekeleza mkataba huo (*FCTC*).

(ii) Kufanyike utafiti wa kutosha wa mazao mbadala kwa zao la tumbaku.

(iii) Kuwepo kwa uwezeshwaji (*financial support*) kwa wakulima na wadau wengine watakaoacha shughuli za tumbaku na kuhamia kwenye kilimo cha kitu kingine au shughuli nyingine ya kiuchumi.

(iv) Uwepo uhuru kwa kila nchi kupanga matumizi ya fedha zitokanazo na mapato ya tumbaku bila kulazimisha kuwa fedha zote zitumike kwa shughuli za afya zinazotokana na madhara ya shughuli za tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu inatekeleza Mkataba huu wa Kimataifa wa Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku (*Framework Convention for Tobacco Control (FCTC)*) kupitia sheria zilizotajwa. Hata hivyo, nchi zinazozalisha tumbaku duniani zinaendelea kujadili namna ya kudhibiti matumizi ya tumbaku. Hadi sasa makubaliano ya nchi zinazozalisha tumbaku hayajafikiwa hususan katika masuala yanayogusa uhuru wa maamuzi ya kila nchi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Nkumba, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA S. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa zao hili la tumbaku ndilo zao linaloingiza fedha nyingi za kigeni hapa nchini na kwa uchumi wa Tanzania ambao kwa namna moja au nyingine unategemea sana zao hili.

Je, Serikali inatoa tamko gani la kuwatia moyo wakulima badala ya maneno ya kuwakatisha tamaa wakulima wa tumbaku nchini?

(ii) Kwa kuwa yapo mazao nchini yanayopata ruzuku kama korosho na pamba, lakini kwa muda mrefu sana wakulima wa tumbaku wamekuwa wanaomba na wao ruzuku kwa ajili ya pembejeo ambapo wakipata ruzuku wataendesha kilimo hiki cha tumbaku kwa gharama nafuu.

Ni lini Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi (CCM) itaamua sasa kutoa ruzuku kwa wakulima wa tumbaku nchini ili waweze kuzalisha tumbaku kwa gharama nafuu na waweze kuliingizia taifa fedha nyingi sana za kigeni?  
(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Nkumba, kama ifuatavyo:-

Naomba nikubali kabisa ni kweli, ila naomba tu Mheshimiwa Said Nkumba hili neno la kwamba uchumi wa Tanzania unategemea zao la tumbaku siyo kweli, isipokuwa zao la tumbaku katika mazao ya kilimo ndiyo linaloongoza katika kuingiza fedha za kigeni nchini, hiyo ni kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika mazingira haya ya sasa hivi kuna ndugu zangu kule wa Namtumbo, Chunya, Urambo, Sikonge, Mpanda, ni wazalishaji wakubwa wa zao la tumbaku. Maisha yao yanategemea uzalishaji wa zao la tumbaku. Kwa hiyo, ndiyo maana nikasema msimamo wa Serikali kwa sasa hivi kwa sababu huko duniani watu hawajaacha kutumia tumbaku, wamepunguza *per capita*. Lakini sisi kama Tanzania matumizi yetu ya sigara ni 110 kwa kila mtu mzima, ndiyo takwimu zinavyoonesha. Lakini kuna nchi kama China huko na wapi, Japani, Spain, Ugiriki, wanatumia zaidi ya sigara 2000 kwa wastani kwa kila mtu mzima. Kwa hiyo utaona sisi ni kama nchi ya 120 kwa matumizi ya Sigara duniani.

Mheshimiwa Spika, sasa soko halitoacha, sisi tukiacha kuzalisha tumbaku haimaanishi kwamba soko litaacha kupokea tumbaku. Kwa kuzingatia kwamba tumbaku yetu ni nzuri na ina soko huko duniani, sisi tunahimiza kwamba kwa hivi sasa ambako hatujafikia hatua ya kuwa na zao mbadala la tumbaku tunaendelea kuzalisha tumbaku lakini tunaendelea na fikra ya kuwa na zao mbadala kwa wakulima wa tumbaku ambalo siyo zoezi la siku moja au siku mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sheria inasema tunaendelea kuzingatia vigezo vya kimazingira na kadhalika na nini, linafanyiwa kazi. Lakini kwa sasa hivi tunaendelea kuwahimiza wakulima wa tumbaku wazalishe tumbaku kwani ina maslahi makubwa kwenye masoko ya dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la ruzuku kwa ajili ya zao la tumbaku tumeishalizungumzia humu ndani na mimi mwenyewe nimeishalijibu kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ruzuku kwa tumbaku kusema kweli ni uchache tu katika ufinyu wa Bajeti, lakini pia mazingira ya uzalishaji wa zao la tumbaku ni tofauti kidogo na mazao mengine. Kuna uwezekano mkubwa wa kupata utaratibu wa bodi ya tumbaku kwa kushirikiana na wafanyabiashara wakubwa kutengeneza mazingira ambayo yatawawezesha wakulima wa zao la tumbaku kuwa na uzalishaji wenye maslahi zaidi. Huo ndiyo tunaouhimiza kupitia kilimo cha mkataba na mazingira mengine ya kiuchumi ambayo yatawawezesha wakulima kuwa na maslahi makubwa zaidi katika zao la tumbaku.  
*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mkitazama muda wetu bado nina maswali manne na muda umeisha kabisa. Wizara ya Katiba na Sheria swali la Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila!

Na. 64

**Marekebisho ya Sheria ya Ndoa na Mirathi**

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA** aliuliza:-

Kuna sheria nyingi zinazohitaji kufanyiwa marekebisho ikiwa ni pamoja na Sheria ya Ndoa na Mirathi:-

Je, ni lini Serikali itazifanyia marekebisho Sheria hizo ili Wanawake wa Mkoa wa Rukwa na hasa wa vijijini waweze kunufaika na Sheria hizi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuzipitia na kuzifanyia marekebisho Sheria mbalimbali za nchi ili kuendana na kasi ya maendeleo mbalimbali ya kiuchumi, Kijamii, kisiasa, kimila, kiteknolojia na kisayansi. Hii ikiwemo na kuzifanyia marekebisho sheria za ndoa na mirathi. Ni azma ya Serikali kuzifanyia marekebisho sheria hizi ili kuhakikisha kwamba wanawake wote wa Tanzania, ikiwemo wa mkoa wa Rukwa wananufaika na sheria hizi ili kukuza na kulinda haki na maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa pia ikichukua jitihada mbalimbali kwa kurekebisha sheria mbalimbali za nchi ili kukidhi haja na matakwa ya wakati huo kwa kadri Bajeti na fedha inavyoruhusu, kama vile, mnamo mwaka 1999 Serikali kupitia Bunge hili Tukufu ilitunga Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, ili kuruhusu

pamoja na mambo mengine wanawake kumiliki ardhi sawa na wanaume na kupata fursa za kushiriki kwenye nafasi mbalimbali.

Mnamo mwaka 2005, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanyiwa marekebisho ili kuongeza nafasi za uwakilishi wa wanawake kwenye ulingo wa kisiasa kutoka asilimia 15 mpaka asilimia isiyopungua 30. Hatua nyingine ni pamoja na Bunge kutunga Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 ambayo iliifanyia marekebisho sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 ili kuhakikisha kwamba, pamoja na masuala mengine wasichana na wanawake wanalindwa dhidi ya vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kutunga sheria hizi mpya na kufanya marekebisho mbalimbali kama ambavyo nimeeleza Serikali bado inayo dhamira ya kuzitazama tena upya sheria za ndoa na mirathi kwa lengo la kuzifanyia marekebisho. Kwa kutambua unyeti wa sheria hizi ambazo zina mchanganyiko wa masuala ya kimila na kidini, Serikali ina nia ya dhati ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Ndoa na Mirathi kwa kukusanya maoni yatakayoweza kuboresha sheria hizo ili kukidhi mahitaji. *(Makofi)*

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini naomba kuongeza maswali madogo mawili tu kwamba:-

(i) Sheria hizi zinazomlinda mwanamke zimekuwepo muda mrefu na nyingi zimekuwa zikifanyiwa marekebisho,

lakini pamoja na marekebisho hayo wanawake wengi hawazijui kwa hivyo wamekuwa hawanufaiki na sheria hizo kwa sababu zimebaki tu kwenye makabati na ma-*shelves*. Sasa Serikali iko mbioni kurekebisha hii sheria ya ndoa na mirathi ikiwa ni pamoja na haki nyingine za binadamu.

Je, Serikali inaahidi nini au ina mkakati gani sasa baada ya marekebisho sheria hiyo isibaki kwenye *shelves* ila wapelekewe wanawake wa mkoa wa Rukwa na hasa wale wa vijijini ambao ni vigumu sana kufikiwa? (*Makofi*)

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Afya kwa sababu ina watumishi mpaka ngazi ya Kata ambao wanaelimisha wananchi kuhusu masuala mbalimbali.

Je, Wizara ya Sheria na Katiba haioni kwamba sasa ni muda mwafaka kupata wanasheria kwenye Kata mbalimbali ili hao wanasheria waendeleo kuwaelimisha wananchi kwenye ngazi za Kata, Vijiji na Vitongoji ili wazifahamu sheria mbalimbali kwa kina ili ile dhana ya kutii sheria bila shuruti iweze kufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rosweeter Kasikila kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la kwanza ametaka kujua Serikali inao mkakati gani wa kuwapelekea wanawake sheria hizi ambazo zimekuwa zikitungwa.

Kwanza kabisa napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imekuwa ikijitahidi kila inavyoweza kuchapisha sheria hizi, lakini pia sheria hizi zinapatikana na zinazuzwa katika maduka mbalimbali ya Serikali ambayo yako mikoani. Pia ziko taasisi mbalimbali zisizokuwa za kiserikali ambazo zimekuwa zikijitahidi kutoa vijarida mbalimbali vyenye kuelimisha sheria hizi zinazohusiana na masuala ya wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili ametaka kujua endapo Wizara ya Katiba na Sheria haioni sasa ni muda mwafaka wa kupata Wanasheria ambao wataelimisha akina mama na makundi mengine maalum katika sehemu mbalimbali za Kata zetu nchini.

Ni kweli Wizara ya Katiba na Sheria inalitambua hili na inaliona ni suala kubwa na muhimu, hata katika mpango mkakati wetu tunatarajia kuleta Bungeni kabla ya mwezi wa Kumi na Mbili mwaka huu sheria kuhusiana na wasaidizi wa kisheria pamoja na huduma za msaada wa kisheria. Lakini pia Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark imeanzisha mfuko wa huduma za msaada wa kisheria (*legal services facility*) na inajitahidi kupeleka huduma hizi katika sehemu ambazo hazijafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata la Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, swali la Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, Mbunge wa Busega.

Na. 65

### **Kuboresha Mnada wa Mifugo wa Mwasamba – Lutubiga**

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI** aliuliza:-

Mnada wa mifugo wa Mwasamba katika Kata ya Lutubiga umepata umaarufu sana kutokana na wachuuzi wanaonunua Mbuzi na Kondoo na kusafirisha kwenda nchi jirani ya Kenya:-

Je, Serikali ina mpango wa kuboresha Mnada huo ili uwe na hadhi ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba uniruhusu nitumie fursa hii kwa niaba ya familia kushukuru Ofisi ya Bunge, Ofisi ya Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Wapiga kura wa Kiteto, Jamaa, Marafiki na Majirani wote kwa ushiriki, misaada ya hali na mali na kufariji ambako mmetufariji wakati wa msiba na mazishi ya Marehemu Baba yangu. Nawashukuru sana kwa niaba ya familia yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini ipo minada ya aina tatu ambayo ni Awali (*Primary Market*), Minada ya Upili (*Secondary Market*) na minada ya Mpakani. Kutokana na utaratibu wa uhawilishaji wa madaraka minada yote ya Awali hujengwa na kuendeshwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo; minada ya Upili na Mpakani huendeshwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mnada wa Mwasamba ni moja ya minada 300 iliyopo katika daraja la Awali hapa nchini. Iwapo Halmashauri ya Wilaya ya Magu inaona mnada huo wa Mwasamba unavyo vigezo vya kupandishwa daraja na kuwa mnada wa Upili au Mpakani.

Basi ni vyema ikaleta rasmi mapendekezo yao ambapo tathmini itakayofanyika ikithibitisha haja ya kupandishwa daraja basi utaweza kuboreshwa na kuingizwa kwenye daraja husika. Hata hivyo, Wafugaji na Wafanyabiashara wanashauriwa kutumia mnada wa Mhunze ambao ni wa Upili na unaweza kutumika kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imejenga jumla ya minada 12 ya Upili na 10 ya Mpakani kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania kufanya biashara na nchi jirani ikiwemo Kenya. (*Makofi*)

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza na mimi niungane na wenzangu kumpa pole Mheshimiwa Naibu Waziri kwa msiba alioupata.

Pamoja na majibu aliyoyatoa kidogo nimetatizika na ushauri ambao wanapendekeza kwamba wananchi watumie mnada wa Mhunze kwa shughuli hizo. Kimsingi mnada wa Mhunze uko mkoa mwingine wa Simiyu na ni mbali kabisa kiutawala na kijiografia na mnada wa Mwasamba anaopendekeza. Mnada wa Mwasamba uko katika barabara kuu inayounganisha nchi yetu na nchi jirani ya Kenya. *(Makofi)*

Hivi karibuni Serikali imejenga barabara ya kuunganisha kijiji hiki cha Mwasamba na barabara kuu inayoenda nchi jirani ya Kenya. Sasa ningependa kumwuliza Naibu Waziri.

Je, ni lini Serikali sasa itafanya utafiti wa kina ili kupendekeza mnada wa Mwasamba kupanda hadhi?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali inapoteza mapato mengi kwa kutopima mnada huu na kuvutia wawekezaji, ni lini Serikali itapima eneo hili na kuligawa kwa wawekezaji kwa viwanja ili liweze kuingiza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi naomba kujibu maswali

mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, mnada wa Mwasamba ni mdogo kiasi, unauza jumla ya mbuzi kati ya 240 hadi 320 kwa mwezi na kwa kweli mbuzi wengi wanaoonekana wakipitishwa hapo kupelekwa Kenya wanatoka katika mnada wa Bariadi kiasi cha wastani wa mbuzi 2559 na mnada wa Dutwa unaouza jumla ya mbuzi 1193 na hao mbuzi wanapitishwa katika eneo analosema Mheshimiwa Mbunge.

Kwa hiyo, ni vizuri tukaacha mamlaka husika wenyewe waje na mapendekezo ama ya kushauri kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema, utafiti wa kina ufanyike ili kuona uhalali wa mnada huo kupandishwa hadhi ama moja kati ya minada hiyo iliyoko katika mkoa huo huo kupandishwa hadhi maana inaonekana kwamba ndiyo inayouza mifugo mingi zaidi kwa nchi jirani.

Kuhusu kugawa na kupanga maeneo hili pia ni suala ambalo liko katika mamlaka husika ya Halmashauri husika. Lakini watakapokuwa wameleta kwetu kiwizara tutakuwa radhi kushiriki na kuhakikisha kwamba mnada huo utatumika kwa manufaa ya wananchi wa eneo lile.  
*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda hauko upande wetu na nyie wenyewe ni mashahidi. Sasa swali la Mheshimiwa Halima James Mdee.

## **Miradi ya kuendeleza Uvuvi nchini**

**MHE. HALIMA JAMES MDEE** aliuliza:-

Serikali imekuwa na miradi mingi ya kuendeleza uvuvi sehemu ya Pwani ya Mwambao wa Bahari ya Hindi:-

(a) Je, Serikali imetoa fedha kiasi gani katika mradi husika?

(b) Katika Mkoa wa Dar es Salaam ni vikundi vingapi vimefaidika na miradi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mradi wa Usimamizi wa Bahari na Mazingira ya Pwani, (*Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP)*) chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia ilifadhili miradi midogo ya uzalishaji mali 470 kwenye Halmashauri 16 za Mwambao wa Bahari ya Hindi katika Mikoa ya Dar es Salaam ambayo miradi 33 ilitekelezwa, Mkoa wa Pwani miradi 187, Mkoa wa Tanga miradi, 93, Mkoa wa Lindi miradi 100 na Mkoa wa Mtwara miradi 57. Ufadhili huo uliwanufaisha wananchi 8,082 wanaume 4,900 na wanawake 3,182

waliojiunga katika vikundi na kuanzisha miradi miradi mbalimbali ambapo jumla ya shilingi 6,702,865,484/= zilitumika katika kutekeleza mradi hiyo. Kati ya miradi 470 iliyoibuliwa na wananchi, miradi 240 ni ya uvuvi. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Dar es Salaam vikundi vya uvuvi vilivyonufaika na mradi wa *MACEMP* ni 20 vyenye wanavikundi 269, ambapo wanaume walikuwa 234 na wanawake ni 35. Jumla ya fedha zilizotumika kufadhili miradi ya uvuvi katika Mkoa wa Dar es Salaam ni shilingi 356,464,760/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa mamlaka za Serikali za mitaa kuendelea kuvisimamia vikundi hivyo kwa kuvipatia elimu ya usimamizi wa miradi hiyo ili iweze endelevu. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Miaka 16 iliyopita Sekta ya Uvuvi ilikuwa inachangia asilimia 10 ya pato la Taifa, wakati huo ilikuwa imeajiri watu 80 tu, lakini sasa miaka 16 baadaye pato la Taifa kwa Sekta ya Uvuvi imeshuka kutoka asilimia 10 mpaka asilimia 1.3, na moja kati ya changamoto ambazo zilielezwa katika miaka 16 iliyopita ni kwamba utegemezi wa wafadhili kutoka nje ndiyo kikwazo cha kukwamisha sekta hii. Leo, Naibu Waziri anajibu anatoa majibu yale yale ya utegemezi ya miaka 16 baadaye.

Sasa kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta hii; na kwa kuzingatia wavuvi walivyochoka kwa kutelekezwa na Serikali. Serikali ina mkakati gani makini wa kutumia fedha

za ndani kuweza kuinua Sekta hii muhimu kwa Uchumi wa Taifa? (*Makofi*)

Swali la pili, imekuwa ni kawaida kwa hizi nyavu ama wavuvi kukamatwa kwa kuambiwa kwamba wanatumia hizi nyavu ambazo zipo chini ya kiwango, lakini wavuvi hawa wanachukua hizi nyavu kutoka viwandani, hakuna *effort* zozote za Serikali kwenda kukamata wenye viwanda.

Sasa nilitaka Serikali iniambie ina mpango gani kuanzia sasa kwenda kukamata na kuvifungia viwanda vyote ambavyo vinazalisha nyavu wanapelekewa wavuvi, wavuvi ndiyo wanakuja kuathirika? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni kweli uchangiaji wa Sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa imeshuka, lakini kushuka kule ni kwa sababu ya michango inayotolewa katika Sekta nyingine kama vile Madini, Utalii na Ujenzi. Kwa hiyo, ni vizuri kutafuta na kutazama *factors* zingine ambazo zinaonyesha kushuka huko kwa mchango kwa sekta ya uvuvi.

Lakini tayari, maana anaulizia katika (a) yake juu ya mkakati. Kama Wizara na kama Sekta tumeishajipanga na tayari tumeandaa kukamilisha mkakati pamoja na Mpango wa kuendeleza sekta ya uvuvi ambao utazinduliwa wakati wote hivi sasa na mkazo sana katika mkakati huo ni kujenga uwezo kwa watu wetu waweze kujenga uwezo wa kuvua kutoka kwenye maji ya kina kirefu yaani kwenda kwenye bahari kuu zaidi kuliko kutegemea mito kama tulivyozoea. Lakini pamoja na mkakati huo ni kukazania pia kilimo



kinachokuza samaki au kwa *culture* ili katika maeneo yetu tunayoishi tuweze kufuga na kuvua samaki.

Lakini swali la (b) yake uchomaji wa nyavu unafanyika, lakini Serikali kama ilivyosisitizwa katika barua aliyoandika Mheshimiwa Waziri Mkuu ya tarehe 18 Januari, 2010 kwa Wakuu wote wa Mikoa kusimamia utengenezaji, usafirishaji, uuzaji na matumizi ya nyavu hizo haramu na hapa mkazo umewekwa si kwa watumiaji tu, lakini pia kwa wauzaji na kwa watengenezaji.

Kwa hiyo, hapa Serikali inabana viwanda husika ili visitengeneze nyavu hizo kwa sababu sheria inaharamisha utengenezaji, usafirishaji, uuzaji na matumizi ya nyavu alizoziongelea Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho katika siku ya leo, Wizara ya Nishati na Madini, Swali la Mheshimiwa Herbert Mtangi.

Na. 67

### **Mfumo wa Usambazaji wa Gesi Nchini**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kutokana na kuongezeka kwa ugunduzi mpya wa visima vya gesi, uzalishaji na usambazaji wa gesi asilia nchini na hujuma za kampuni binafsi ya usambazaji wa mafuta ya petroli nchini kama ilivyojitokeza hivi karibuni:-

Je, kwa nini Serikali isirejeshe Kampuni ya Taifa ya *Gasco* iliyoundwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) ili kusimamia mfumo wa usambazaji wa gesi nchini badala ya kutegemea kampuni ya nje ya *Pan African Energy*?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *GASCO* ni kampuni tanzu iliyoundwa na Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (*TPDC*) chini ya sheria ya Kampuni na kupewa Cheti cha usajili Nambari 11280 tarehe 13 Agosti, 1985. *GASCO* iliundwa kwa madhumuni ya kujihusisha na usambazaji gesi asili nchini.

Jukumu la msingi la *GASCO* lilikuwa kuiuzia gesi asili Kamuni ya Kilwa *Amonia Company Ltd. (KILAMCO)* iliyoundwa kwa ajili ya uzalishaji mbolea kutokana na gesi asili. Shughuli za *KILAMCO* zilisitishwa kutekelezwa kutokana na sababu kadhaa ikiwemo, kutumia muda mwingi kutafuta fedha za kuendeleza mradi, badiliko la wafadhili wa mradi na kuahirishwa kwa mpango wa utekelezaji mradi kutokana na kushuka kwa bei ya mbolea kwenye soko la Dunia kati ya miaka ya 1980 na 1990.

Mheshimiwa Naibu Spika, *GASCO* ilihuishwa upya mwaka 1998 ili kujihusisha na uuzaji gesi asili ya Songo Songo kwenye mitambo ya umeme na kuhusika na usambazaji wa gesi asili hapa nchini na nje ya nchi. Hata hivyo, shughuli za *GASCO* zilisitishwa rasmi mwaka 2001 baada ya *TPDC* kuathirika kifedha kufuatia mabadiliko katika mfumo wa uagizaji mafuta nchini ambapo Serikali ilibadili mfumo wa uagizaji mafuta kwa kuruhusu mfumo wa ushindani wa soko huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeliagiza Shirika la *TPDC* kufanya mapitio ya muundo wake ili kuendana na hali halisi ya sasa katika shughuli za utafiti, uchimbaji, uzalishaji na usambazaji wa mafuta ya gesi asili. Mchakato huu umelenga kutenganisha baadhi ya shughuli za Shirika ikiwemo usimamiaji wa mfumo wa usambazaji gesi asili hapa nchini.

Pindi mchakato utakapokamilika, kampuni ya *GASCO* itahuishwa rasmi ili kushughulikia uendelezaji wa kazi ya kusimamia mfumo wa usafirishaji na usambazaji gesi asili hapa nchini pamoja na miundombinu yake. (*Makofi*)

**MHE. HERBET J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa, lakini napenda kusema ndani ya Bunge lako Tukufu wapo Waheshimiwa Wabunge wanne ambao walitoa mawazo ya kuanzishwa kwa Kampuni *KILAMCO*, *GASCO* pamoja na *COPEX* ili kusimamia usambazaji wa mafuta na gesi. Lakini kikubwa ni kwamba utekelezaji haukufanyika na laiti ungefanyika hata

mgogoro uliotokea kule Mtwara wala usingetokea.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, jukumu la *GASCO* ni kusimamia usambazaji wa gesi, lakini vilevile ni kutoa elimu kuhusu mikakati ya usambazaji wa gesi na matumizi ya gesi nchini kwa wananchi wa Tanzania.

Je, kwa nini Serikali isijitolee sasa na kutoa fedha ya kuwezesha *GASCO* kuanza mara moja ili jukumu liweze kuwa ndani ya mikono ya wananchi na vilevile kuongeza ajira kwa wananchi?

(b) *GASCO* imechelewa kuanzishwa kutokana na *TPDC* kudhoofika kifedha. Lakini taarifa zinaonyesha hapa hata Kamati ya Nishati ya Madini iliyopita kwamba Kampuni inayosambaza gesi sasa ya kutoka nje ya nchi imehodhi fedha zaidi ya dolla milioni 20 mali ya *TPDC* kwa muda mrefu bila kuwalipa. Naibu Waziri anasema nini kuhusu hali hiyo na kama kweli *TPDC* wameishalipwa fedha hizo?  
(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kama ingekuwepo Kampuni hii ambayo hivi tunavyozungumza bado haijaanza ingawa dhamira ya Serikali kuhakikisha Kampuni hii inakuwepo ili ifanye kazi kwa niaba ya Watanzania, tatizo lake kubwa ni fedha. Lakini pia mkakati wetu wa uharaka ule uliathiriwa sana na

makubaliano yetu kwamba hatukuwa na sera ya gesi na baadaye sheria ya gesi. Sasa tukadhani pengine mambo haya yakianza yaweza yakaathiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nichukue nafasi hii kusema kwamba katika mapendekezo mengi yaliyotolewa na Watanzania kuhusiana na suala la sera ya gesi. Moja kati ya mambo ya msingi ni eneo hili katika umiliki wa miundombinu na kusimamia usambazaji wake.

Kwa, hiyo, niseme tu kwamba sera ya gesi ipo karibu kutoka ni wakati wowote kuanzia sasa itakuwa tayari inamalizia hatua zake za mwisho na baadaye tutaleta sheria hapa Bungeni katika kutunga sheria hiyo. Waheshimiwa Wabunge mtapata fursa nzuri zaidi ya kueleza namna tunavyoweza tukaweka hata hizi kampuni za kusimamia sekta ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwamba kampuni hii inayofanya kazi hiyo kwa sasa ya *Pan African* inadaiwa na *TPDC* ni kweli na Wabunge walikwishaagiza ingawa ndani humo kuna mambo mengi yaliyoingiliana katika mahusiano ya kibiashara kati ya kampuni hii ya *Pan African* na *TPDC* na wadau wengine bado uchambuzi wake unaendelea. Lakini mazungumzo yanaendelea na si mabaya.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umeisha na maswali yetu yameisha na muda wetu

kama mnavyouona hauko upande wetu. Naomba niwataje wageni wetu kwa haraka haraka waliopo kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika kuwa ni Engineer Chiza Sayi, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, karibu, ahsante na Engineer Basil Mrindoko Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji. (*Makofi*)

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni Wakurugenzi wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Maji, lakini pia Wakurugenzi wa *Life Fitness Centre* ya Arusha ambayo ni wafadhili wa Timu ya *Bunge Sports Club* iliyokuwa Kambini Arusha kwa maandalizi ya Michezo ya Bunge la Afrika Mashariki hawa ni Bwana George Lyimo, Bwana Dudley Mawalla na Bwana Paul Were. Karibuni sana popote mlipo. (*Makofi*)

Tatu, ni wageni kutoka *Flight link Limited* wakiongozwa *Managing Director* wa *Flight Link Limited* Captain Munawer Dhirani, karibu sana.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni watano wa Mheshimiwa Sylvester Mabumba, ambao ni wastaafu kutoka Ujerumani kijiji cha Newsasen ambayo ni Ndugu Dieter Bertisch, Ndugu Bruno Golder, Ndugu Meter Hofer, Ndugu George Otto Ruf na Padri Mosha, karibuni sana wageni wetu kutoka Ujerumani.

Wageni wa Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira, ni pamoja na Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine ambao ni Mheshimiwa Peter Mwera Nyanguru, Diwani wa CCM Kata ya Mriba Tarime na ni Kaimu Mwenyekiti wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la

Tarime. Karibu sana Mheshimiwa Diwani Nyanguru. Pia yupo Mwalimu Nyerere Jakson, Mwalimu wa Nkende *Secondary School* Tarime, Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Goodluck Ole Madeye, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ni Ndugu Priscilla Phelemen, Ndugu Flora Amos, Ndugu Maria Lazaro, Ndugu Eliamani Joseph, karibuni sana. (*Makofi*)

Lakini pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Tundu Lissu - Mnadhimu Mkuu wa Upinzani, ni mzee Samson Munkinya kutoka kijiji cha Isuna Jimbo la Singida Mashariki. Yupo pamoja na Fanuel Muna ambaye ni Katibu wa Mbunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya vikao. Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba Kamati ya Ulinzi na Usalama ikutane leo saa 7.00 Mchana Ukumbi wa Msekwa (b). (*Makofi*)

Kikao cha kazi pia Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo Mheshimiwa Sylvester Mabumba, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Sheria Ndogo kukutana katika Ukumbi Namba 227 ghorofa ya pili jengo la utawala saa 7.00 mchana.

Mheshimiwa Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii anaomba Kamati ya Huduma za Jamii ikutane leo saa 7.00 mchana Ukumbi wa Pius Msekwa (C).

Tanzia nimepewa taarifa na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani anatoa taarifa ya kifo cha aliyekuwa Mbunge wa zamani wa Jimbo la Ziwani katika mwaka 1995 – 2000 Maalim Hashur Nassor, ambaye amefariki katika usiku wa kuamkia leo, mazishi yatakuwa leo saa 10.00 jioni huko Zanzibar.

Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, bwana alitoa na bwana ametwaa, jina la Bwana lihidimiwe. Tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, amin.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na uzoefu tuliopata siku ya Ijumaa katika uendeshaji wa Shughuli za Bunge, ningependa kuwakumbusha Wabunge baadhi ya mambo muhimu ya kuzingatia.

Moja ni kwamba Mbunge unapoamua kutumia kanuni ya 68(7) ya kuomba mwongozo kumbukeni kwamba unapoomba mwongozo anayekuwa kwenye kiti hapa anaweza katoa mwongozo huo hapo hapo au akautoa baadaye kanuni zinampa madaraka ya kufanya hivyo.

Kwa hiyo, unapoomba mwongozo na unalazimisha mwongozo utolewe saa hiyo hiyo unakuwa siyo uendeshaji mzuri wa Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, unapotaka kuitumia hiyo Kanuni uwe unajua jambo hilo, usitake kutumia Kanuni na kutaka kulazimisha mambo saa hiyo hiyo yafanyike vile unavyotaka. Kwa



sababu kila Mbunge hapa akilazimisha mambo yaende anavyotaka yeye kwa kweli kwa ujumla wake hatutaweza kufika popote.

Kwa mfano, baada ya hapa tuna hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla na baada ya Mheshimiwa Kigwangalla kuna hoja ya Mheshimiwa John Mnyika. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla akishika hapa akitaka tufanye ya kwake yeye na muda utakwisha na wengine hawawezi kupata nafasi. Mimi nipo hapa kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata nafasi kwa kadri ya muda uliopangwa hapa. Hilo la kwanza.

Pili, lakini vilevile kwamba hoja iliyopo mezani ni hoja gani, siyo vizuri hoja iliyopo mezani ni nyingine, halafu unapachika hoja nyingine juu yake na wakati mwingine mwongozo unaishia kuomba hoja na hoja hiyo inaungwa mkono kwenye mwongozo inafika mahali fulani inakuwa ni fujo hivi.

Tatu, jukumu la kuagiza *document* yoyote iwekwe mezani ni jukumu la Kiti siyo jukumu la Mbunge wewe kulazimisha kwamba lazima kitu hicho kiwe hivyo. Wajibu wako wewe ni kushawishi na kujenga hoja. Kiti ndicho kitakachoamua ni wakati gani na kwa namna gani *document* yoyote ya Serikali iwekwe mezani. (*Makofi*)

Nne, kwamba Kiti kina upendeleo, ni hoja ambayo imekuwa ikitolewa mara kwa mara, lakini niseme tu ndugu zangu na nawaomba kwa sababu tunaenda kwenye kuandika Kanuni zetu vizuri zaidi siku zijazo, humu ndani Wabunge wa CCM tuko robo tatu, robo ndiyo Wabunge

wa Upinzani. Chukua *Hansard* yoyote ya kipindi cha maswali toka hili Bunge la Kumi lianze, *Hansard* yoyote ya uchangiaji wowote ule, ya siku yoyote ile, tazama idadi ya Wabunge wa CCM waliochangia na Wabunge wa Upinzani waliochangia, utaona Wabunge wa Upinzani ni wengi ukilinganisha na idadi hiyo ya uwiano wa robo na robo tatu.

Katika mazingira ya kawaida, tukitaka twende kwa usawa huo, tugawe kabisa kwamba kwa kila maswali manne litakuwepo swali moja la Upinzani. Kwamba, kila wachangiaji wanne atakuwepo mchangiaji mmoja wa Upinzani, kila wachangiaji wanane watakuwepo sita wa CCM, wawili wa Upinzani. Tukubaliane kwa utaratibu huo, mtaona kwamba hali mliyonayo sasa ya Upinzani ya kupata uchangiaji mkubwa zaidi mtaipoteza. Mimi niko tayari twende kwenye mgawanyo huo, nitamshawishi Mheshimiwa Spika na nyinyi Waheshimiwa Wabunge mkikubali huo ndiyo uwiano wa haki na uwiano huo utatuondolea malalamiko ya kusema kwamba kuna upande fulani unaonewa. Mimi kwa uhakika, kwa sasa Wabunge ambao hawapati muda wa haki ni wa CCM. *(Makofi)*

Mwisho, kuhusu Waandishi wa Habari; Waandishi wa Habari katika kuwaatarifu Wananchi, rafiki zangu Waandishi wa Habari ninyi ni watu muhimu, lakini nataka kuwakumbusha jambo moja; wakati Bunge linapoendelea hapa ndani mkiona Mbunge yeyote au kikundi cha Wabunge chochote kikitoka hapo nje, hapo kantini, Ukumbi wa Msekwa, kwenye Jengo la Utawala au mahali pengine popote, mjue wanakunywa chai tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mkitaka kuripoti kwamba Wabunge wametoka nje ya Ukumbi wa Bunge ni nje ya geti. Kwa hiyo, Mbunge yeyote anaruhusiwa kutoka nje mmoja mmoja, watano watano, kundi, yaani hapa sisi tunaendelea na shughuli zetu kama kawaida. Kwa hiyo, msiwaambie Watanzania kwamba kuna Wabunge wametoka nje ya Bunge, nje ya Bunge ni nje ya Ukumbi kule nje ya geti kabisa. Muwe mnaripoti sawasawa ndugu zangu Waandishi ili tuelewane. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo!

### **HOJA BINAFSI ZA WABUNGE**

**Hoja ya Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangala ya Kuitaka Serikalilanzishe Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana kwa Kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza Kwenye Kilimo na Viwanda Vyenye Uhusiano wa Moja kwa Moja na Kilimo**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Nawaomba Waheshimiwa tuendelee na majadiliano, miongozo nitaipa nafasi mwishoni kidogo, kwa sababu ya muda ambao ni mdogo sana nilionao.

Katika uchangiaji wetu nitamwita Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, hapo hapo ulipo.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru kwa

kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala, inayohusu ukosefu wa ajira kwa vijana na hivyo kulitaka Bunge kupitisha Azimio la Kuitaka Serikali Kuanzisha Mfuko Maalum wa Kukopesha Vijana wanaowekeza kwenye kilimo na viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, kwa kuleta hoja hii muhimu na kuwa na Mpango Maalum wa kukuza ajira kwa vijana na Maazimio yanayolenga umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana Wanaowekeza moja kwa moja katika masuala ya kilimo. Namshukuru pia Mheshimiwa Gaudencia Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira, kwa mawasilisho ya kina kuhusu hoja ya Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla na mapendekezo ya Serikali kuhusu hoja hiyo. Kwa namna ya pekee kabisa, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge Kijana kwa Tiketi ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuwasilisha Marekebisho ya Mapendekezo ya Serikali. Nitumie nafasi hii pia kusema kwamba, naunga mkono Marekebisho ya Mheshimiwa Ester Bulaya katika hayo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, michango mingi imepitishwa na wakati wa kuchangia kuna hoja moja iliendelea hapa ya kusema kwamba, Waziri wa Vijana ameulizwa swali kuhusu takwimu za ukosefu wa ajira za vijana akashindwa kujibu. Mimi nataka ijulikane wazi kabisa sijawahi kuulizwa swali hilo na sina kumbukumbu kama hicho kitu kimewahi kuulizwa Waziri wa Vijana.

Kwa nafasi yangu kama Waziri mwenye dhamana ya kushughulikia maendeleo ya Vijana nchini, nawapongeza walioleta hoja; Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mheshimiwa Ester Bulaya na wachangiaji mbalimbali, kwa kutusaidia na kuisaidia Wizara na Serikali kuweza kuwavuta Vijana kuona umuhimu wa KILIMO KWANZA na nafasi yao kama Vijana katika kuhakikisha tunatekeleza hili jukumu la KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali, tumejipanga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 81(b) – (i) lakini pia Ibara ya 79, ambayo kimsingi inaelekeza Serikali kuibua na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuwatayarisha Vijana kuweza kujitambua, kujiajiri na kuweza kuajirika ikiwa ni pamoja na kuajiri Vijana wenzao. Kama nilivyosema, tumepokea michango mingi ya kuboresha na mingi inahimiza Serikali kuona kero mbalimbali zinazowakabili Vijana na kuzichukulia kama fursa za kuweza kuwapatia kazi. Sasa napenda niseme tu kwamba, Serikali imesikia kilio hiki kwa kipindi kirefu na imeweka Idara inayoshughulika na Maendeleo ya Vijana kuweza kufanyia kazi masuala mbalimbali yanayowakabili Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Idara hii ya Maendeleo ya Vijana ina majukumu ya moja kwa moja ambayo yanalenga moja kwa moja mchakato ambao hoja hii kubwa tunayoizungumzia inashughulikia. Ina Kitengo cha Maendeleo ya Uchumi na Uhamasishaji kwa Vijana (*Youth Economic Development and Mobilisation Section*) na jukumu la msingi la Kitengo hiki ni kuhamasisha uundwaji wa Vikundi vya Vijana vya kuzalisha mali, kuvitambua na kutoa

mikopo chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kupitia TAMISEMI.

Kimsingi, upo Mfuko wa Maendeleo ya Vijana uliopitishwa kwa Sheria ya Bunge, tatizo ni kwamba haupati fedha za kutosha. Pia kipo Kitengo cha Makuzi, Ushauri Nasaha na Maongozi kwa Vijana (*Youth up Bringing, Guidance and Counselling*). Jukumu kubwa la msingi la Kitengo hiki ni kuandaa vijana kimakuzi, kimaadili na kiuzalendo, kupitia stadi za maisha, stadi za kazi na ushauri nasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wabunge, napenda niliseme wazi hili kwamba, limekuwa linafanyika kwa bidii zote na kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita kumekuwa na hamasa kubwa sana na michakato mbalimbali ya kujitahidi kuweza kuunganisha haya masuala ya vijana kule katika ngazi ya Halmashauri na tumekuwa tunashirikiana kwa karibu kabisa kuzungumza na Halmashauri.

Katika kufanya hili, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana katika *level* ya Halmashauri, Watu wa TAMISEMI wametupatia nafasi kama Wizara chini ya Idara ya Maendeleo ya Vijana kuweza kuwa na mtu pale ambaye anashughulikia masuala ya Vijana moja kwa moja; hivyo basi, Kitengo hiki cha Idara kinakuwa ni rahisi kabisa kuweza kutekeleza masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la msingi la Kitengo cha Mafunzo ya Maendeleo na Ujuzi (*Youth Training and Skills Development*) ni kuandaa, kuratibu na kutoa mafunzo

ya ujasiriamali na stadi za kazi kupitia Vituo vya Mafunzo vya Vijana. Naona niliseme hili kusudi mwone wazi kabisa kwamba masuala mbalimbali yanayohusu Vijana kwa maana ya kuwatayarisha ili waweze kujajiri, kuajirika, lakini pia kuweza kuwaajiri wengine pamoja na kuwapatia maarifa ya biashara na masuala mbalimbali ya mitaji, yako tayari yanafanyiwa kazi katika ngazi mbalimbali, ndani ya Serikali kwa kupitia kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri zetu na Wizara ya Kazi na Ajira. TAMISEMI kwa ujumla wamekuwa tunashirikiana nao kufanya kazi hizi ili kuhakikisha tunawasaidia hawa Vijana waweze kujitambua na kuweza kujitayarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu, suala la maendeleo ya Vijana ni suala mtambuka, utekelezaji wake wa kukuza ajira kwa Vijana ni mmojawapo ambao unawagusa wadau wote ikiwa ni pamoja na Sekta zote za Serikali. Nachukua nafasi hii kuwaomba kwamba, kila mdau aguswe na changamoto hii. Tujitahidi kuhakikisha kwamba tunawatayarisha Vijana katika sekta mbalimbali ambapo kazi zozote zinazotayarishwa katika sekta hizo umuhimu uwe katika kuwafuatilia hao Vijana ambao tayari wanakuwa wamekwishatayarishwa kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana pamoja na Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo wa Vijana kimsingi upo tangu mwaka 1993/1994. Kwa kipindi cha mwaka 2007/2008, Mfuko wa Vijana umeweza kukopesha Vijana jumla ya shilingi ya bilioni 1.2 kupitia SACCOS 242 kutoka katika Halmashauri 121 nchini. Mfuko huu uko chini ya Sekta ya Maendeleo ya Vijana; kimsingi,

ninachotaka kusema hapo, mahitaji ya Vijana ni makubwa mno na uwezo wa Mfuko ni mdogo. Mkakati wa kuboresha huu Mfuko umeandaliwa na umekwishawasilishwa katika ngazi mbalimbali za mipango Serikalini. Mpango wa Serikali ni kwamba, watakaowezeshwa katika Mfuko huu wataweza kuwa wateja wazuri wa Benki ya Vijana hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii, suala la Benki ya Vijana liliibuka na kuna *statements* zilijitokeza kama kweli hili suala la Benki ya Vijana ni muhimu au kama itaweza kuwepo au imekuwa ni *story* tu. Nataka nichukue nafasi hii niseme kwamba, suala la Benki ya Vijana siyo *story* tu, suala la Benki ya Vijana liko katika ngazi mbalimbali ya matayarisho. Mpaka sasa tumekwishafikia kuzungumza na tuko katika nafasi ya kutafuta mtaalam mwelekezi wa kuweza kutushauri, lakini kimsingi tumeshafikiria Makao Makuu yatakuwa wapi, tumeshaamua nani atakuwa msimamizi, lakini pia kwamba itakuwa ni benki ya namna gani.

Tumekwishapanga kwamba, itakuwa ni Benki ya Biashara ya masharti nafuu kwa maana ya kwamba, tayari vijana mbalimbali kupitia makundi yatakayojitokeza katika Baraza la Vijana, yale makundi yatakayounda Baraza la Vijana watakuwa tayari ni Vijana wenye kujitambua, ambao tayari wamekwishapitishwa katika mafunzo mbalimbali pamoja na uwezo wa kujua masuala ya kushughulikia masuala ya pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii niseme kwamba, katika utekelezaji wa haya masuala



mbalimbali hasa ya Benki ya Vijana, tuko katika ngazi ya kuhakikisha kwa mwaka huu ikiwezekana kabla ya Juni, tuwe tunatambua wazi kabisa hiyo benki itafanya kazi namna gani na itakuwa vipi na uwezekano wa kutafuta hela kiasi cha shilingi bilioni 15. Hizi shilingi bilioni 15 tulizungumza na BoT, ndiyo waliotueleza kwamba kuweza kuanzisha Benki ya namna hii basi ni muhimu kuwe na mtaji wa shilingi bilioni 15. Kwa hiyo, nataka niseme tu ile *story* kwamba, Benki ya Vijana labda ni hadithi tu, hapana ni kitu ambacho tunakichukulia umuhimu na tunategemea kwamba ni muhimu Vijana wawe na hiyo Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia niseme tu Vijana wawe na matumaini, wajitume, wawajibike kwa malengo chanya, Serikali inawatambua, Serikali inawafanyia majukumu mbalimbali. Tukigusa Wizara mbalimbali hapa utakuta zote kuna mikakati ambayo ni ya msingi kabisa ambayo zimefanya juhudi mbalimbali wakati wa kuajiri au wakati viwanda mbalimbali vinaanzishwa, Vijana wanapewa nafasi zaidi na hii haitokei *automatically* tu, inatokea kwa jitihada za makusudi kabisa zinazofanyika na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono marekebisho ya hoja yaliyotolewa na Mheshimiwa Ester Bulaya. Ahsanteni. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Sasa naomba nimwite Waziri wa Kazi, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka. Mtoa hoja jandae maana utafuata sasa hivi.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Naomba niende moja kwa moja. Hoja hii ni yetu wote, sisi wote ni wadau, tunapozungumzia suala la ajira hasa ajira kwa Vijana na utakumbuka ulivyotumba tukae pamoja Serikali, mtoa hoja chini ya Mwenyekiti wa Maendeleo ya Jamii pamoja na wachangiaji akiwemo Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na sisi Serikali, kwa pamoja tunasema kuundwa kwa Mfuko Maalum kwa ajili ya kushughulikia masuala ya ajira na hasa ajira kwa Vijana ni kitu ambacho hakikwepeki.

Programu nzuri inaweza kuwepo, lakini kama haina uwezesho, haina pesa ya utekelezaji, programu hiyo itakuwa ni kazi bure. Kwa hiyo, hoja hiyo naiunga mkono, kwa maana hiyo kwamba mpango huu utakuwa na Mfuko Maalum. Tofauti na Mifuko ambayo nilitaja katika maelezo yangu ile ni Mifuko ya Ujasiriamali ambayo imekuwa ikiwasaidia Watanzania kwa ujumla kupata ajira na kujiajiri na kuajiri wengine; ni Mfuko wa Maendeleo wa Vijana kama alivyozungumzia Mheshimiwa Waziri anayehusika, lakini Mfuko huu pia ulikuwa unapata fedha kutokana na OC ya Wizara ambayo ilikuwa haitoshelezi, maana Wizara isipopata OC ya kutosha basi na Mfuko huu pia unatetereka. Kwa hiyo, haja ya kuwa na Mfuko mahususi kwa ajili ya Vijana na Programu Mahususi kwa ajili ya Vijana, hili ni jambo zuri na wote tunapaswa kuliunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu hii na Mfuko wake vitasaidia kuongeza ajira ya Vijana na hasahasa ajira yenye staha. Sitasema sana kuhusiana na ajira yenye staha, lakini kipengele kimojawapo cha ajira yenye staha ni kwamba, Vijana watajiwekea akiba, watajiunga kwenye vikundi na

wataweza kujiwekea pia akiba katika Hifadhi ya Jamii kwa mafao ya wakati huo na mafao ya baadaye, kuliko sasa hivi wanavyoendesha maisha yao hawawezi kujiwekea akiba katika Hifadhi ya Jamii ambayo tunasema ni muhimu kwa sasa hivi na wakati wamechoka hawawezi tena kujiendesha na ajira zao.

Hii ni kutokana na kwamba, kwa kweli katika uchumi wetu, uchumi umekua, lakini kukua kwa uchumi wetu kumeshindwa kukabili wimbi la mahitaji ya wahitimu wa ngazi zote za elimu kuanzia shule ya msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu, ambao wanaingia katika soko la ajira kila mwaka. Haya ni matokeo mazuri ya maendeleo mazuri ya elimu yetu, Sera yetu ya Elimu ambayo chini ya mipango miwili ya MEM na MMES ambapo MEM ilianza mwaka 2001 baadaye kidogo MMES, matokeo yake yalianza kuonekana mwaka 2007. Kwa hiyo, soko la ajira likafurika na hii yote ni nguvu kazi.

Mtoto anapomaliza Darasa la Saba anataka afanye kazi kama hakuenda sekondari, lakini huyo wa Kidato cha Nne pia kama hakuendelea na elimu ya Kidato cha Sita na baadaye Elimu ya Juu angependa ajajiri. Sasa na wa Vyuo Vikuu kulingana na *Liberalisation* ya Elimu ambayo kutokana na Sera ya 1995 tuliruhusu watu binafsi kuanzisha Shule za Sekondari na baadaye za Msingi na baadaye Vyuo Vikuu, wahitimu wamefurika katika soko la ajira na hii ndiyo imesababisha kwa kweli uchumi wetu hata pamoja na ukuaji wake, umeshindwa kuhimili ukubwa wa soko hili la ajira.

Nikitoa tu mfano, mwaka 2005 wahitimu katika soko la ajira katika ngazi zote za elimu walikuwa 324,983 kabla ya matokeo ya MEM na MES. Mwaka 2010 baada ya matokeo ya MEM na MES, soko letu la ajira kwa wahitimu wote waliomaliza na ambao walikuwa sasa ni nguvu kazi ya Taifa walikuwa 1,008,225. Hili ni ongezeko la asilimia mbili ya wahitimu wanaokuja katika soko la ajira kila mwaka.

Kwa hiyo, nasema Mfuko huu na Programu hii mkishaipitisha, Serikali tutajua jinsi ya ku-*harmonise* mambo yetu, itasaidia sana kupunguza kiwango cha ukosefu wa ajira ambacho naomba kwa kweli nitumie nafasi hii kutoa taarifa kama nilivyosikia juzi wakati mchangiaji mmoja akichangia kwamba ni asilimia 30. Takwimu rasmi ya kiwango cha ukosefu wa ajira Tanzania kwa takwimu za utafiti wa nguvu kazi wa mwaka 2006 ni asilimia 11.7 na utafiti huu wa nguvukazi hufanyika kila baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa mwisho ulifanyika mwaka 2006 na hatujafanya utafiti mwingine, tulikuwa tufanye 2011 lakini kutokana na maandalizi ya Sensa hatukuweza, tunategemea kufanya sasa hivi. Kwa hiyo, kiwango kipa cha *unemployment* kitatoka 2014, mwakani, kwa sababu sasa hivi ndiyo tunatakiwa kuifanya na utafiti huu unatumia mwaka mzima. Una-*include public* na sekta iliyo rasmi na sekta isiyo rasmi. Kwa hiyo ni utafiti ambao ni wa kisayansi. Sasa ukianza kusema asilimia 30 na nilishawahi kusikia mwanasiasa mmoja anasema asilimia 36, sijui taarifa hizi siyo rasmi kwa sababu ni takwimu ambayo inatokana na utafiti.

Kwa hiyo, naomba tukubaliane kwamba, kwa utafiti wa mwisho, *unemployment rate* sasa hivi ni asilimia 11.7; ni afadhali hata ukisema inawezekana ikafika asilimia 12. Kwa hiyo, Mfuko huu utasaidia sana kupunguza hiyo *unemployment rate* na juzi Wizara ya Kazi kwa kushirikiana na Ofisi yetu ya Takwimu, tumetoa hali ya ajira nchini. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge kabla hamjaondoka, taarifa hii itakuja hapa Bungeni, muweze kuona hali ya ajira nchini katika *Public Sector*.

Katika Sekta ambayo siyo rasmi, hii inategemea sasa huu utafiti unaozungumzwa. Katika Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, *employment rate* imeongezeka. Sasa *employment rate* imeongezeka, ina maana *unemployment rate* inapungua. Kwa hiyo, mimi nafikiri tusebiri hizo takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi mimi naunga mkono hiyo lakini kabla sijamaliza, naomba pia nitoe taarifa kulingana na majadiliano yaliyofanyika hapo Siku ya Ijumaa; moja ikiwa ni hii fedha ya *ILO* ambayo nafikiri Mheshimiwa Mnyika pia alizungumza kwamba, Serikali nafikiri kupitia Wizara yangu, ilipata fedha kutoka *ILO* kwa ajili ya kukuza ajira ya Vijana. Anauliza fedha hii iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niseme kwamba, Wizara haikupata fedha kutoka *ILO*, lakini mwaka 2005 Wizara ilichofanya iliandaa *document* ya Mpango wa Taifa wa Kukuza Ajira au *National Employment Creation Programme*.

Sasa katika kuandaa Mpango huu kulikuwa na gharama ilikuwa kumwajiri Mtaalam Mwelekezi (*Consultant*), pamoja na gharama nyingine. Sasa gharama hizi ndiyo zilizotolewa na *ILO*. Kwa hiyo, *ILO* haikuleta pesa katika Wizara ambazo tunatakiwa kuzitolea taarifa na Mpango huu utekelezaji wake bado. Kwa hiyo, hatujapata fedha ya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mara nyingine kwa kweli tuwe tunatafuta hizi taarifa sahihi kwa sababu unapozungumza kwamba Wizara imepata pesa, *in fact* hata *ILO* wenyewe walishangaa wakaniuliza *what type of money is this? What was the MP talking about?* Kwa hiyo, ni vizuri tukaulizana na kama unatafuta ukweli kwa ajili ya nia nzuri mimi nitakupatia tu. Kwa hiyo, naomba tuwe tunawasiliana.

Naomba pia nizungumzie suala la ajira nje ya nchi. Serikali kupitia Wakala wetu wa Huduma ya Ajira (*TAESA*), imeweza kwa kweli kuwatafutia Watanzania ajira zaidi ya 2000 nje ya nchi, ikiwemo Nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, Oman, Saudi Arabia lakini pia na Denmark. Sasa hivi tunasubiri kusaini Mkataba na Nchi ya Qatar kwa ajili ya kupeleka Watanzania kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutafuta kazi kwenye *internet* kama yule msichana aliyekuwa ana-*serve* kile kiti cha One A (1A), mimi sikatai. Watanzania naomba wawe *aggressive* pia watafute kazi kwenye *internet* kwa sababu hii ni ruksa ya kila mtu. Serikali kwa upande wetu tunafanya hizo juhudi na sasa hivi tunapoongea, Wizara ya Kazi imeshaandika *document* ambayo imeipeleka Wizara ya Mambo ya Nje na nafikiri wao wamepeleka kwa Mwanasheria Mkuu kwa

ajili ya ku-*seduce* ajira zaidi Nchi ya Oman na jana nilipokuwa naulizia nimeambiwa mwezi huu wa Februari, Serikali ya Oman itakuja Tanzania, wataongea na Serikali yetu kwa ajili ya mpango huu mzuri wa kutafutia Watanzania kazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua Wakenya ni *very aggressive* na nilivyokuwa namsikiliza mmoja wa wagombea Urais anasema, *unemployment* yao ni asilimia 40. Wako milioni 41, *unemployment* ni asilimia 40. Kwa hiyo, kwa kweli lazima wawe *aggressive* na sisi tunaomba tuwe *aggressive*. Serikali ipo *aggressive* na Wananchi naomba muwe *aggressive*, Vijana muwe *aggressive* kusudi wote twende sambamba. Kwa hiyo, hii ni kazi ya kila mdau na sisi wenyewe Wabunge tuwe *aggressive* na makampuni tuwe *aggressive*, Sekta Binafsi tuwe *aggressive*, kwa ajili ya kusaidia Vijana wetu kutafuta kazi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na swali lilijitokeza wakati wa kuchangia kuhusu dereva Mkenya katika Ubalozi wetu wa Uswisi. Taratibu za kidiplomasia kulingana na *Vienna Convention*, kazi hizi ambazo ni za chini, sisemi za chini sana lakini katika *level* hiyo ya udereva na mambo mengine, Balozi zetu zinaajiri *local staff*. Sasa kule Geneva walitangaza hii kazi ya dereva na katika *applicants* walioleta maombi mmojawapo ni huyu bwana, ambaye anaitwa Bwana Omoro ambaye anatoka Kenya na Waswisi na Bwana Omoro ana kibali cha kukaa kule kwa sababu mke wake pia anafanya kazi *UN*.

Sasa unapopata *applicant* Uswisi ambaye ni *local* au unapata *applicant* Mkenya ambaye katika *terms* hizo

anaweza kuajirika kama *local* hivi utamchukua nani? Si afadhali uchukue Mkenya mnaweza kuongea Kiswahili wakati mnaenda kwenye mizunguko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *this is what happened* na ni sahihi na wakati Mheshimiwa Mbilinyi amekwenda, kwa kweli alitusaidia sana kwa sababu aliweza kumwambia kanitafutie vocha, anaongea Kiswahili na hii ndiyo maana huyu bwana ameajiriwa kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nirudie kusema kwamba, naunga mkono hoja na nawashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa naomba nimwite kwa ufupi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji na Uwezeshaji baada ya hapo mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu sana na kupitia Baraza la Uwezeshaji, Serikali imefanya mambo makubwa sana ambayo pengine kupitia Bunge lako, itakuwa jambo zuri wakilisikia ili tukiunganisha na jitihada za mtoa hoja, tunaweza tukaenda mbali zaidi kuliko tulikofika.

Nianze kwa kumshukuru sana na kumpongeza na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala, Mbunge wa Nzega, kwa kuileta hoja hii na hasa kwa jinsi alivyoguswa na matatizo yanayowakabili Vijana pamoja na ubunifu wake. Namshukuru sana Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudensia Kabaka, kwa kuleta marekebisho kwenye hoja



ya msingi ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, ametolea ufafanuzi Mfuko wa Vijana. Nawashukuru na kuwapongeza Wabunge wote, kwa kusema yale ambayo wameyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mapendekezo ya hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ni utekelezaji wa maelekezo ya Ibara ya 79 na 81 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010 na kwa hiyo ni kazi ya Serikali kuona kwamba, maelekezo ya Chama chetu yanatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, hela nyingi sana zimetolewa, siyo nyingi ukilinganisha na mahitaji ya vijana, lakini takriban shilingi bilioni 1.094 zimetolewa kupitia Mfuko ule. Siyo Mfuko huo tu; ila kuna changamoto kwenye huo Mfuko kwamba tunapaswa kuongeza fedha zaidi na baada ya hii hoja nina hakika wote wanaohusika wataliona hilo. Pia Serikali inawawezesha Vijana kupitia Mfuko wa Uwezeshaji ambao upo chini ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mfuko huo nao una hela nyingi sana, hela zilizopitishwa kwenye Mfuko huo zinafikia shilingi bilioni 8.47.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo tu ...

## **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kanuni ya 68(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 60(8):-

*“Mbunge hatasoma maelezo isipokuwa kwa madhumuni ya kutilia nguvu maelezo yake anaweza kusoma dondoo kutoka kwenye kumbukumbu zilizoandikwa au kuchapishwa na anaweza pia kujikumbusha kwa kuangalia kwenye kumbukumbu alizoandika.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anasoma maelezo, nafikiri siyo sahihi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, unaweza ukaendelea. Ahsante Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasoma takwimu ambazo zinaonesha jitihada za Serikali ili Waheshimiwa Wabunge waone kwamba, Serikali imefanya lakini bado jitihada nyingi zaidi zinahitajika na kwa hiyo, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kuonesha ni kwamba, kuna Mifuko mingi sana na kila Mfuko una hela. Kama nilivyosema ile iliyotangulia, lakini kuna Mfuko wa Wanawake ambao vilevile umefikia shilingi bilioni 4.04. Mfuko mwingine ni ule ambao unapitishwa *SIDO* nao una

bilioni 26 na Mifuko mingine mingi. Kwa mfano, *SELF* wana shilingi bilioni 36.6 na wajasiriamali zaidi ya 80,000 wamenufaika. Mfuko wa *TASAF* una shilingi bilioni 428 na Vijana wananufaika nao na Mifuko mingine mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, Mifuko yote niliyoitaja kwa pamoja ilitoa mikopo na dhamana zenye jumla ya shilingi bilioni 690.5. Kwa hiyo, Serikali inafanya jambo kubwa. Jambo muhimu hapa ni kujipanga vizuri na kuona Mifuko hii inaratabiwa na ikiwezekana ile inayohusu Vijana inawekwa pamoja na hoja hii ya Mheshimiwa Kigwangala pengine inaweza kutufikisha kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba, Vijana lazima wajipange na nchi zinashindana kwa namna ambavyo zinajipanga. Vijana wakijipanga na inajulikana kwamba Vijana wengi wametokana na wazazi maskini na kwa hiyo wao hawana mali isiyohamishika, kwa hiyo, hawana dhamana kwenda Benki.

Namna pekee ya Vijana ya kuweza kunufaika na hii Mifuko ni kuwa kwenye vikundi na kuwa kwenye *SACCOS* na ushirika wao, lakini Vijana wengi hawako. Ninawaasa Vijana wangu kwamba, wakubali kuwa kwenye *SACCOS*, wakubali kuwa kwenye Ushirika, wakubali kuwa kwenye Vikundi na wakubali kuwa kwenye *VICOBA* ili waweze kunufaika na fedha hizi ambazo zinatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa vilevile ...

## **T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mimi napenda kuungana na Mheshimiwa Nagu, kwa kutambua jitihada ambazo zinafanywa na Serikali kwa ajili ya Vijana. Wakati tunapitisha bajeti mwaka jana, Mheshimiwa Mary Nagu alikiri kwamba, kulikuwa kuna changamoto zilizojitokeza katika zile fedha za mabilioni ya JK na akasema kwenye awamu ya pili kutakuwa na fedha maalum ambazo zitatengwa kwa vijana. Sasa baada ya hii hoja kupita, vijana walikuwa wanaulizia ndiyo maana nikasema ni vyema nimweleze aji-*commit* kwamba katika awamu hiyo hizo fedha zipo na je kutakuwa na uwezekano wa kuziweka katika huo mfuko utakaoanzishwa ambao utakuja kuwa benki. Ni hilo tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, tukumbuke kwamba Mheshimiwa Waziri anachofanya ni kuchangia hoja. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mmoja wa watu ambao napenda kuwapongeza sana ni pamoja na Mheshimiwa Ester Bulaya, ambaye pamoja na Mheshimiwa Kigwangalla, wamekuwa wakipigania haki za Vijana na wanajaribu kutoa mawazo yenye busara ya kuweza kuendeleza vijana.

Nataka nimhakikishie kwamba, fedha zile za Mheshimiwa JK, zilifanya kazi kubwa sana na mchanganuo

wake ninao kama nilivyo na michanganuo ya Mifuko mingine. Pengine cha kukiri hapa ni kuelezea kazi gani ambayo imefanyika kutokana na mabilioni ya JK na kwamba kwa kweli yaliwawezesha Vijana wengi na Wananchi wengine wengi.

Nataka nimhakikishie kwamba, tutajitahidi sana kuona vyanzo mbalimbali ambavyo vinaweza vikatunisha Mfuko ambao utasaidia kuongeza ajira za Vijana, lakini nisingependa kukubali kwamba ni Serikali peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Binafsi ina nafasi pekee katika kuchangia ajira ya vijana. Vijana ndiyo nguvu kazi ya nchi, Vijana ndiyo watoto wetu, Vijana ndiyo tegemeo letu na tutahakikisha kutokana na utajiri wa madini, kutokana na utalii wa utalii na kutokana na utajiri wa gesi ambao Mwenyezi Mungu ametupa, sehemu kubwa ya faida ya wale wawekezaji watakaonufaika na rasilimali hii itaelekezwa kwa Vijana na kwenye kilimo na maeneo mengine ambayo vijana wanaweza wakapata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza tena Mheshimiwa Kigwangala na nampongeza zaidi kwa kukubali marekebisho ya Mheshimiwa Waziri, ambayo yameboreshwa na Mheshimiwa Ester Bulaya. Nakiri kwamba, ikiwa Serikali na Wadau wengine wote tutafanya kazi kwa pamoja, kutambua *plight* ya Vijana au adha ya Vijana kutambua kwamba ni sehemu kubwa ya jamii ambayo kama itawajibika na tukiwasaidia, wanaweza kusukuma mbele maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ambayo karibu ungenisahau. Utaona kwamba, kama shilingi bilioni 690 zimetolewa kwa ajili ya uwezeshaji na uwezeshaji huu, unapelekwa kwenye nguvu kazi ambayo ni Vijana kama tutajipanga vizuri. Vijana wakikubali wajibu wao, wasipocheza *pool table* saa nne, nina hakika nchi yetu tutaikwamua kutokana na huu umaskini ambao umekithiri na adha ya Vijana kukosa ajira itapungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa naomba kumwita Mheshimiwa Mnyika. Ni nini tena?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mtoa hoja anakwenda kuhitimisha hoja ili Bunge liweze kuamua, hili ninalotaka kuomba Mwongozo wako litapoteza umaana kama hoja itahitimishwa na hoja itaamuliwa. Kwa hiyo, ningepomba unipe fursa ya kuomba mwongozo wa utaratibu wa hatua ambazo tunakwenda nazo mbele kutoka hapa baada ya Mawaziri kumaliza kuchangia kabla ya mtoa hoja kuhitimisha hoja.

**NAIBU SPIKA:** Endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 57(1) na 58(1). Kanuni zote hizi mbili zinahusu utaratibu wa kufanya mabadiliko ya hoja katika hatua mbalimbali kabla uamuzi haujafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii, mtoa hoja alitoa hoja yake, Serikali ikapendekeza marekebisho kupitia kwa Waziri mwenye dhamana. Mheshimiwa Ester Bulaya, akapendekeza mabadiliko ya mabadiliko yaliyowasilishwa na Serikali, kukawa na mjadala katika hatua hiyo kuhusu mabadiliko hayo yaliyowasilishwa. Sasa hivi mtoa hoja anakwenda kuhitimisha na hatimaye Bunge kuweza kufanya uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza michango ya Waheshimiwa Mawaziri, michango yote inadhihirisha kwamba; moja, Mfuko wa Vijana tayari ulishakuwepo kwa mujibu wa Sheria, tatizo ni kutengewa fedha kwa ajili ya utekelezaji. Pili, nchi yetu ina Sheria nyingi za Uwezeshaji, za Ajira na nyinginezo, tatizo ni kwamba fedha zinazotumika kwanza haziko bayana; lakini pili, hakuna maeneo maalum yanayohusiana na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nimewasilisha kwa awamu mbili tofauti kwenye hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na baadaye kwenye marekebisho ya Mheshimiwa Ester Bulaya, mapendekezo ya mabadiliko ya hoja ili tushughulikie msingi wa tatizo ambao ni kushindikana kwa utekelezaji wa Sheria na utekelezaji wa Mipango, lakini mabadiliko haya hayajaingia humu ndani.

Kwa hiyo, napenda kupata mwongozo kabla hoja haijaamuliwa ili niweze kupewa fursa ya kuwasilisha hayo mabadiliko tuweze kuunda Mifuko na tuweze kujenga misingi ya utekelezaji wa Mipango na Sheria ili tuweze kupata ufumbuzi wa kudumu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, ahsante sana. Nilipewa taarifa kwamba, uliwasilisha marekebisho ya hoja ofisini lakini ukiwa umechelewa. Marekebisho hayapo hapa Mezani kwa Makatibu wangu na mimi mwenyewe hayakuwepo na kwa sababu hiyo hayakuingia katika utaratibu wa kawaida kama marekebisho mengine yalivyokuwa wakati ule tulipokuwa tunafanya marekebisho ya mjadala huu wa hoja iliyopo mbele yetu kuhusu masuala ya Vijana. Kwa jinsi hiyo, kwa sababu hayakuingia kutokana na wewe mwenyewe kuchelewa kuyaleta, basi kwa hiyo ni bahati mbaya.

Mheshimiwa Kigwangala, naomba uendelee. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa siku ya leo ili niweze kufanya majumuisho ya hoja ambayo niliwasilisha hapa Siku ya Ijumaa wiki iliyopita.

Baada shukrani hizo kwako, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kuchangia kwenye hoja ambayo niliwasilisha hapa Bungeni; wale waliopata fursa ya kusema; na wale waliotoa michango yao kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kuwatambua wale wote ambao wamechangia kwa kusema hapa Bungeni, nikianza na Mheshimiwa Gaudentia



Kabaka, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwatambua wale ambao walipata fursa ya kutoa michango yao kwa njia ya maandishi na nianze kwa kumtambua Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari, Mheshimiwa Namelock Edward Moringe Sokoine, Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Joshua Nassari, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge; michango yao nimeisoma, nimeisikiliza na nimesoma *Hansard* za michango, kwa kiasi kikubwa Wabunge wote wameonesha kukubaliana na hoja niliyoitoa hapa Bungeni. Mara chache sana tumetofautiana namna ya kimawazo kuwa ni jinsi gani tunaweza kutatua

tatizo la ajira kwa Vijana wa Kitanzania. Mchango ambao niliona ulikuwa *radical* sana *to the extreme left* ulikuwa ni mchango wa kaka yangu, Mheshimiwa Tundu Lissu.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa ana haki ya kuongea, nitajitahidi kuchukua fursa hii uliyonipa ya kufanya majumuisho ya hoja yangu walau kumpa elimu kidogo ili aweze naye kurudi kundini na kuelewa kwenye huu mpango tunangelea nini. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mawaziri wote, waliochangia hapa Bungeni na nimshukuru zaidi na kumpongeza dada yangu, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, ambaye pia naye alipata fursa ya kutoa mapendekezo ya kufanyia mabadiliko hoja iliyoletwa hapa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, Mama Gaudentia Kabaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nilishakubaliana na mapendekezo yale, sasa nichambue tu hizi hoja ambazo zimeletwa na Wabunge na nianze kwa kueleza kuwa, Wabunge wote kwa ujumla wamekubaliana kitu kimoja kwamba, tuna tatizo la fikra, tatizo la *mindset*, katika nchi yetu, ambapo Vijana wengi wanadhani kuwa ajira ni kuajiriwa katika mfumo rasmi wa ajira, kwa maana ya kuajiriwa katika mfumo wa Serikali au Mashirika ya Umma na kupewa hizi *white collar jobs* ama *blue collar jobs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo fikra iliyopo miongoni mwa Vijana wengi wanapohitimu masomo yao na hata miongoni mwa Vijana ambao wapo katika masomo, wanapohitimu masomo yao wanawaza kuwa watakapopata shahada zao, watakapohitimu masomo basi watapata ajira nzuri, watafanya kazi na kuendesha

maisha yao na kuhudumia familia zao. Ajira katika Dunia ya leo na katika ile Dunia ya kesho ambayo ndiyo tunayoitarajia kwa Vijana hawa, imebadilika sana.

Dhana ya ajira sasa hivi ni pamoja na kujiajiri, ni pamoja na kufanya shughuli ambazo zitakuongezea kipato wewe binafsi na ukaajiri wengine ambao hawakupata fursa ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kama nchi ambayo kwa sasa inafuata mfumo ninaoweza kusema ni wa *Mixed Economy*, wa Uchumi Mchanganyiko, wa masoko zaidi, ina fursa nyingi sana za biashara, za kilimo, ambazo zinaweza kutumiwa vizuri kwa Vijana wetu kujiari wao wenyewe na kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao. Fursa hizo kwa bahati mbaya sana zimekuwa hazitumiki ipasavyo.

Lingine ni suala la *mindset* pia, ninakumbuka hata Mheshimiwa Samuel Sitta, aliwahi kulizungumzia mwaka jana hili suala la watu kutaka ajira ambazo ni rasmi na kukwepa kufanya baadhi ya kazi na uvivu kuwa, watu hawataki kutafuta fursa. Alizungumza sana kwa uwazi hapa na sitaki kurudia haya lakini huo ni ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimewahi kufanya kazi za aina nyingi sana, mtu akiniona leo anaweza kudhani kuwa kazi niliyoifanya ni hii ya Ubunge tu na niliibuka ghafla na kuwa Mbunge la hasha! Ninafahamu pia kuwa hata Wabunge wengi hapa walishapitia kazi nyingi sana katika maisha yao mpaka kufika hapo walipofika leo. Sasa Kijana wa Kitanzania anatakiwa kubadilisha fikra yake *aji-tune* kukamata kila *opportunity* inapopatikana ya ajira

ilimradi tu apate kipato chake na tukifikia hapo tutaona Vijana wetu wanakuwa *aggressive*, tutaona vijana wetu wanajituma zaidi katika kulivamia soko la ajira kama wanavyofanya wenzetu Wakenya na nchi zingine.

Mimi binafsi nimewahi kufanya kazi ambazo unaweza kusema ni za deiwaka ama za wasaka tonge kama vile kazi za kibarua, za udereva, za ukuli, za uchuuzi wa bidhaa mbalimbali, za kusambaza magazeti wakati nikitafuta elimu yangu huko nje ya nchi ni ajira hizo nimefanya na zimeniwezesha kupata kipato ambacho kiliniwezesha kujikimu maisha yangu mpaka nikamaliza masomo.

Vijana wa Kitanzania wanatakiwa wafanye kazi za namna hiyo. Ninafahamu Mheshimiwa Juma Nkamia, naye alipokuwa akisoma kule Uingereza, alikuwa akifanya kazi ya u-*waiter* kwenye baa, alikuwa akifanya kazi ya kusambaza magazeti ilimradi tu apate pesa ya kumuwezesha kujikimu katika shughuli zake za kimaisha wakati akitafuta elimu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetembea sana katika nchi mbalimbali hapa Duniani na nimewaona kule siyo Vijana wa Kitanzania, nimeona Vijana wa Kikenya, Wakinijeri, wa Kighana, wa Kichina, wa Kihindi, wakifanya kazi ambazo sisi Vijana wa Kitanzania tunasema pengine ni za hovyonyo na hazina hadhi inayofaa kwa Kijana wa Kitanzania lakini wenzetu wanazifanya.

Huwezi kuibuka ukawa Mbunge siku moja ama ukawa Daktari siku moja eti Daktari uliyesoma nje ya nchi una maisha mazuri ama ukaibuka ukawa Felista Dada, *Air*

*Hostess*, ambaye tulipata hadithi hapa Siku ya Ijumaa kutoka kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, huwezi ukaibuka hivyo tu kama umekaa nyumbani umelala unacheza bao, unacheza *pool table* mchana kutwa bila kutoka na kwenda kutafuta riziki; haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale Waislamu, wanafahamu Hadithi ya Mtume inasema kuwa, mguu uliotoka Mtume kauombea. Kutoka maana yake ni kutoka kwenda kutafuta siyo kutoka tu unatoka nje. Ninategemea Vijana wa Kitanzania wanaonisikiliza sasa hivi, wataanza kutoka wataenda kuvamia masoko ya ajira; na hapa ninaelezea tu dhana moja ya *mind-set change*, kubadilisha fikra.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaeleza kwa mifano mbalimbali ya kazi ambazo watu mbalimbali wamewahi kuzifanya, nikasema mimi binafsi nimefanya kazi ya kuuza mchele mashineni wakati nikisoma ili niweze kupata pesa niweze kulipa hela ya *tuition* kwa mwalimu. Maana nimesoma *High School* ambayo haikuwa na mwalimu hata mmoja katika masomo yangu matatu ya *physics, chemistry and biology* niliyokuwa ninasoma, lakini tuliweza kufaulu kwa sababu tulikuwa tunatafuta pesa tunalipa walimu wa *tuition* ili waje watufundishe shuleni kwetu kwa sababu tutakwenda wapi shule ndiyo hiyo hiyo hakuna nyingine, siku hizi kuna ma-*saint* nini huko watoto wanasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, zama tulizosoma sisi zilikuwa ni hizi hizi Shule za Serikali na matatizo ya walimu yalikuwepo, lakini tuliweza kujisomesha kwa kufanya biashara mbalimbali. Mimi binafsi niliwahi kuuza mchele,

sasa leo mtu anashangaa nimefika kuwa Mbunge, sijui kesho watashangaa nini nikiwa Rais kama hii ndiyo *mindset* niliyonayo kwamba hakuna kisichowezekana, kila kitu kinawezekana tukiamua kubadilika na kuji-*tune* kuwa inawezekana kuwa siku moja mimi nikawa Mbunge, inawezekana kuwa siku moja nikawa Reginald Mengi, siku moja nikawa Bhakhresa, utaona kuwa inawezekana.

Vijana wa Kitanzania wa-*unlock brain* zao ili waweze kuzikamata fursa mbalimbali ambazo zipo katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangalla mpaka hapo uko ndani ya utaratibu ilimradi hujautaka Unaibu Spika tu, endelea kuchangia Mheshimiwa.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengine ambayo wameongea Waheshimiwa Wabunge, ninajaribu kuunganisha kwa pamoja ili nisichukue muda mrefu sana na hili ni suala la uwepo wa watu kutoka nchi mbalimbali wanaoingia katika nchi yetu kufanya kazi kinyume cha utaratibu. Ninaomba Serikali ichukue hilo kama changamoto ilifanyie kazi kwa sababu ni kweli kuna Wakenya wengi wanafanya kazi katika hoteli mbalimbali hapa nchini kwetu, wanalipwa mishahara mizuri kama *expatriates* wakati kazi hizo zingeweza kufanywa na Vijana wa Kitanzania ambao wapo katika soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile mimi sitaki kuchukulia hii dhana ya watu kutoka nje kuja katika nchi yetu *negatively*, inaweza ikawa ni *positive*, kwa maana ya kwamba Vijana wa Kitanzania wajifunze kutokana na

*experience* hiyo, wajue wenzao wanafanyaje kuja kwetu ili na wa kwetu sasa waende wakavamie soko lao la ajira kwa sababu tunaongelea mambo haya ya utengamano wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Hatuwezi kuwa kama kisiwa, ni lazima kuwe na mwingiliano wa watu ili tujifunze kutoka kwa watu lakini pia na sisi tuweze kuzitumia fursa zilizopo katika nchi zao.

Jambo lingine ambalo nimeona limechangiwa kwa maandishi na watu wengi ni uwepo wa rasilimali nyingi katika Taifa letu na namna ambavyo zinatumika kuwafaidisha Watanzania. Hili mimi ninalichangia katika sura tofauti, nikisema kuwa kuna ubeberu ambao unaingia katika nchi yetu na ubeberu huu siyo mzuri sana kwa mustakabali wa Taifa na siyo mzuri sana kwa mshikamano wa Kitaifa.

Ninasema hivyo kwa maana ya kwamba, ubeberu ni sawasawa na mwanafunzi mtukutu, ambaye akipewa adhabu ya kutoka nje ya darasa ama akipewa mtihani na akafeli, anaendelea kurudi siku hadi siku, anarudi darasani na kesho yake tena atakosea atatolewa tena nje na atarudi tena darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninaongelea namna ambavyo ubepari na ubeberu vimekuwa vikirudi katika Nchi za Kiafrika siku hadi siku hata kama utaangushwa na mfumo lakini uta-*keep on returning on back and back*; na hapa ninasema kwa maana ya kwamba, tunaona sasa hivi katika nchi yetu ujio wa Mashirika makubwa ya Kimataifa, ninaongelea *Multinational Corporations*. Mashirika haya ya Kimataifa yanapokuja nchini yanakuja na nyimbo nzuri sana

hadi Mashirika ya Kibeberu yanakuja kihalali, yanakuja Kisheria na mengine yanachukua ardhi kubwa sana na baada ya kuchukua ardhi hizo, visingizio ni viwili tu; cha kwanza ni kwamba, mabeberu hawa wanasema kuwa wakiwekeza watazalisha ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema wakiwekeza watakuza uchumi wetu na nchi yetu itaendelea na wanawekeza katika sekta nyeti na sasa hivi wanaingia kwenye Kilimo, walikuwa kwenye Nishati na Madini wanazalisha umeme, wanakuja wanavuna dhahabu, wanavuna almasi wanapeleka nje, kisingizio ni kimoja kikubwa kwamba watazalisha ajira. Kwetu Nzega waliwadanganya Wananchi wa Nzega kwa namna hiyo hiyo kwamba, Watu wa Nzega watafaidika watapata ajira.

Matokeo yake, wakitoa ajira kwa mwaka mmoja, wa pili na wa tatu, wanapunguza idadi ya wafanyakazi, wanaanza kuleta *theory* zao za kiuchumi na kibiashara. Wanaoajiri wanapungua siku hadi siku na mwisho wa siku ajira zinazoongezeka ni chache mno kiasi kwamba unaweza kusema hazihesabiki katika uhitaji wa ajira tulionao katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamekuwa wakijirudia kuingia katika mifumo mbalimbali na jinsi mabeberu hawa wanapokuja na ahadi hizo tamu, sisi tunawakaribisha kwa kuwajengea mazingira mazuri, kuwarahisishia namna wanavyoweza kupata ardhi, kupata viwanja na namna ya kupata hati, masharti ya kibenki tunawarahisishia tunawaambia kuwa mnaweza kuondoka na faida yoyote



mnayoweza kuvuna hapa. Tunawaambia mambo mengi mazuri ambayo yanawavutia waje, lakini wakishafika hapa faida tunayoipata ni ndogo sana ukilinganisha na namna wanavyokuja.

Ninalisema hili kwa maana ya kwamba, kama tunatengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya makapuni ya kibeberu kuja kuwekeza katika nchi yetu, sasa hivi tunaingia na kwenye kilimo, tunawaruhusu na huu Mpango wa *SAGCOT* ambao mimi ninauunga mkono, siwezi kusema ni mbaya ni mzuri lakini kama tunatengeneza mazingira ya *SAGCOT* kufanikiwa, tunawaleta Mabeberu wanakuja kuchukua ardhi na kuwekeza kwenye kilimo. Kwa nini sasa ninauliza swali hapo? Ni kwa nini sasa sisi kama Taifa tusiwekeze kwa Vijana wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunaweza kutengeneza mazingira mazuri ya kuwapatia ardhi Mabeberu ni kwa nini tusitengeneze mazingira mazuri namna hiyo hiyo kwa kuwapa Vijana ardhi kwa masharti nafuu katika mazingira nafuu yanayoeleweka lakini pia hawa Mabeberu wanakuja kutoka kwao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, sina uhakika kama maneno hayo unayotumia ni sahihi sana, uwe makini kidogo. Sina uhakika kama kuna Mabeberu wanaotoa ardhi Tanzania.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nikisema kwa Kiingereza nitaeleweka;

Beberu ninamaanisha *imperialists*, labda hili linaweza kuwa rahisi.

Haya Makampuni ya Kimataifa yanayokuja kuwekeza hapa, yamejengewa mazingira mazuri sana, kwa lugha nzuri, ambayo imebadilika siku hizi inaitwa uwekezaji na yanawezeshwa kwa mifumo ambayo tumeitengeneza kwa Sheria za Bunge kupata ardhi, kulindwa kila aina na namna ambayo itawafanya wafanye kazi zao vizuri. Baada ya kuwezesha, wanaendelea, wanafanya mambo yao, wanavuna wanachokitaka na wanaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inabaki palepale, leo hii Mgodhi wa *Resolute* kule Nzega, umefungwa na ajira walizozitoa hazifiki hata 3,000 toka wameingia mpaka leo. Sasa kama wameajiri watu ambao ni *less than 3,000*, walikuwa na faida gani pale na wakati wanaingia tulisema kwamba hawa wataongeza ajira na ajira walizoongeza ndiyo hizo lakini kabla ya hapo watu zaidi ya 10,000 walikuwa kwenye maeneo mbalimbali ya ile *belt* ya dhahabu wakichimba maana walikuwa wakipata faida kutoka kwenye ardhi ya nchi yao.

Ninachokisema hapa ni kwamba, kama tunatengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya watu wa nje ambao wao wanapata mikopo kutoka katika nchi zao, wamejengewa mazingira mazuri kwenye nchi zao wapate pesa waje wawekeze Afrika, wazalishe, wavune na warudishe faida kwao.

Kwa nini sisi kama Taifa tusiwekeze kwa Vijana wa nchi hii?

Hoja hii nimeileta kwa sababu hiyo kwamba, tutengeneze mpango kabambe ambao utakuwa mpya, utaleta nguvu, utaleta mazingira mazuri ya kuwapa Vijana ardhi, mazingira mazuri ya kuwatambua Vijana wawekezaji na kuwawezesha kwa kuwapa mikopo nafuu ili waweze kufanya shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja nia nzuri ambayo nilikuwa nayo katika kuleta hoja hii, nimesikitishwa na michango mingine, sanasana mchango wa Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba, yeye haoni faida ya uwepo wa mpango huu.

Nimeshangaa sana jana, wakati ninatoka Nzega nimepita pale Isuna nimekuta Vijana, wanahangaika hawana ajira wako kijiweni, wengine wanacheza *pool*, kuna mmoja tu ambaye amejajiri ameweka meza ya *pool* pale, kwa hiyo, yeye anachukua michango kutoka kwa wenzake, maana yeye ndiyo amejajiri anapata faida wale wengine wote ni wazembe hawafanyi kazi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge badala ya kushughulika na masuala kama haya ya Isuna, anakuja kushughulika na hoja ya kupinga mpango ambao utawawezesha Vijana wapewe maeneo kwenye vijiji vyao. Anapinga Maazimio yasipitishwe na Bunge ya mpango ambao utawawezesha Vijana wapewe mikopo ili waweze kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mtu wa namna hii anawawakilisha wale Vijana niliowakuta Isuna wanahangaika hawana ajira, walivyojua

tu kuwa mimi ni Mbunge, wakaanza kuniomba pesa ya matumizi wakale; ni mtu wa kuogopwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Nzega nilipata fursa ya kuhutubia jana kwenye Mkutano wa Kusherehekea Chama cha Mapinduzi kufikisha umri wa miaka 36, niliwaambia vijana wa Nzega ambao walinipongeza sana na kuniunga mkono kwamba nimewasilisha hoja nzuri, wanasubiri utekelezaji wake. Wakaniuliza kwa nini sasa Mheshimiwa Tundu Lissu anakupinga, mbona sisi tunamfahamu ni mwanamapinduzi? Nikawaambia, Tundu Lissu amedhihirisha ni namna gani yeye ni mnafiki. Kwa sababu ni Tundu Lissu huyuhuyu ambaye mwaka 2006 wakati nafanya kazi Hospitali ya Taifa ya Muhimbili...

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu uingilie kati kwa mara ya pili, kwa sababu mara ya kwanza umemuonya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla juu ya matumizi yake ya lugha. Sasa naomba uingilie kwa mara ya pili umfundishe matumizi ya lugha ya staha Bungeni. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangalla, endelea.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Tundu Lissu ni Kaka yangu

na ninakumbuka mwaka 2006 amewahi kuwa mgonjwa wangu nikimtibu na ninafahamu matatizo yake.

**NAIBU SPIKA:** Daktari usije ukatoa siri za wagonjwa, endelea lakini hebu kuwa makini kidogo. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Tundu Lissu namfahamu, ni Kaka yangu...

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(1) ikisomwa pamoja na Kanuni za 63(1) na 64(1)(a) ya Kanuni za Bunge hili. Naomba nirudie, Kanuni ya 68(1) inayozungumzia Kuhusu Utaratibu ikisomwa pamoja na Kanuni za 63(1) na 64(1)(a) zinazokataza Mbunge kusema uwongo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba iwe kwenye rekodi ya Bunge lako Tukufu kwamba mimi sijawahi kuwa mgonjwa wa Dokta Hamisi Kigwangalla, siyo mwaka 2006, wala si kipindi chochote katika maisha yangu, hajawahi kunitibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea mwaka 2006, Dokta Hamisi Kigwangalla na Madaktari wenzake wa Muhimbili, walikuwa wamefukuzwa kazi, wakashtakiwa katika Baraza la Madaktari, mimi niliwatetea bure, anachosema hapo ni uwongo na naomba aidha aithibitisha au aifute kauli yake kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba niseme tu kwamba mimi kama Daktari, kimaadili siruhusiwi sana kuongelea magonjwa ya wagonjwa wangu na kwa maana hiyo sitoweza kutoa taarifa za ugonjwa wa mgonjwa wangu Tundu Lissu...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu kuonyesha kutoridhishwa na maelezo anayotoa Mhe. Dkt. Hamisi A. Kigwangalla)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama hawezi kuthibitisha afute kauli yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, ungekuwa na subira tumsikilize kwanza.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Mheshimiwa Tundu Lissu yanajulikana, watu wa humu Bungeni mnayafahamu na watu wa kule nje wanayafahamu...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea kwa sauti za juu kuonyesha kutoridhishwa na maelezo ya Mhe. Dkt. Hamisi A. Kigwangalla)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangalla, naomba ukae kwanza, nimekuona Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge hili nimekusikia juzi ukisema Wabunge watumie lugha ya staha na kitu ambacho Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla anazungumza kuhusu Mbunge mwingine kwa kweli hakiruhusiwi. Kwa hiyo, naomba na ninamshauri ndugu yangu Dkt. Kigwangalla aondoe yale maneno aliyoyasema ambayo yanaleta taabu kwa Mbunge mwingine. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, ninakushauri sana na kukuomba uyatoe yale maneno ili uendelee kuchangia kwa vile kwa kweli unakula muda wako bila sababu wakati hoja yako ni nzito sana. Ningekuomba uyatoe yale maneno ili uweze kuendelea kuchangia. Ahsante.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuyatoa maneno yale, naomba niendelee na hadithi yangu niliyokuwa ninaitoa kuhusu historia ya mambo yaliyotokea mwaka 2006. Hii ninaeleza ili Watanzania waelewe kwamba katika

kesi ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu ana-*refer* na kweli alitutetea, nakubali, lakini tulijikuta katika mahusiano yale tumekuwa marafiki, tukawa kama Kaka na wadogo zake. Katika urafiki ule tulikuwa tukizungumza mambo mengi sana, mojawapo ya mambo ambayo tulikuwa tukizungumza, ni namna ambavyo sisi vijana tutalikomboa Taifa letu kutoka kwa viongozi wasaliti, kutoka kwa viongozi wafisadi, tulizungumza sana mambo haya. Katika kuzungumza mambo hayo, nikajifunza kitu kimoja, kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu ni mtu makini na kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu ni mtu *nationalist*, ni mtu anayelipenda Taifa letu kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hoja alizozitoa hapa Mheshimiwa Tundu Lissu siku ya Ijumaa, ni hoja ambazo zimenifanya nimwone ni mtu ambaye yupo *so inconsistent*, ni mtu ambaye anabadilikabadilika. Hoja zake hazikuonesha hata kidogo uzalendo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, nimekwishakuelekeza kwamba ujitahidi kuondoka huko ili usonge mbele.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshaondoka zamani kule, sasa hivi ninajenga hoja na hoja ninayojenga ninajibu hoja za kupinga kwa hoja alikokufanya Mheshimiwa Tundu Lissu kwa lugha ya matusi, akisema hoja yangu haina mantiki, akisema hoja yangu haina fikra.

## **T A A R I F A**



**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakae chini, Mheshimiwa Mwigulu alisema hapa Bungeni, wanaume wakiwa wanaongea, vijana wanyamaze. Sasa tunaongea wanaume, vijana wanyamaze. *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu kuonyesha kutoridhishwa na maelezo ya Mhe. Dkt. Hamisi A. Kigwangalla na baadhi walikuwa wamesimama kuomba Mwongozo wa Spika)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba umwambie huyo akae chini ili niendelee na hoja yangu.

## **T A A R I F A**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Mnyika. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ukae chini na Waheshimiwa wengine wote wakae chini. Mheshimiwa Mnyika ungejua mimi najaribu kuokoa muda ili wewe uweze kuongea, usingenipotezea tena muda.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitajielekeza kwenye lugha ya kuudhi, mimi napenda tu kumpa taarifa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, inaonesha

hakuelewa alichokuwa anazungumza Mheshimiwa Tundu Lissu. Mheshimiwa Tundu Lissu alichokisema na kwa kuwa yupo hapa, anaweza kupewa nafasi ya kusema alichokisema. Alichokisema Mheshimiwa Tundu Lissu na kumbukumbu za Bunge zipo, sisi hapa dhana ya fikra ya hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ni kwamba kuwe na utaratibu wa kuwa na mfuko na mikopo na utaratibu wa namna hiyo. Mheshimiwa Lissu amejenga hoja kwamba mfuko na mikopo siyo suluhisho pekee la matatizo ya ajira kwa vijana Tanzania na amesema...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa! Mheshimiwa Mnyika anapotosha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, malizia kwa kifupi sana tafadhali.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, amesema jambo ambalo kama mabadiliko yangu yangeletwa nimeeleza bayana kwamba ili tutatue tatizo la vijana kwa upana wake, ni lazima tutazame sekta zote, tuwe na mkakati mpana, tuunganishe kati ya ukuaji wa uchumi wa nchi na ongezeko la ajira. Sasa anaweza akawa amekerwa sana na maneno ya Mheshimiwa Lissu ya kwamba mpango huu ni wa kutongozea kura, lakini maneno haya ya kutongozea kura hayawezi kuondoa umaana wa dhana aliyokuwa akizungumza ya kupanua wigo wa suluhisho la tatizo la ajira kwa vijana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, taarifa hiyo Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, endelea, unaikubali au vipi?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna taarifa hapa, kuna maneno machache tu aliyoyaongea lakini siyo taarifa zinazo-*inform my argument, let me go back in line.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi kwenye mstari na hizi *interruption*, naomba unitunzie muda wangu maana hazina maana yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijenge hoja kwamba wakati tunazungumza tatizo la ukosefu wa ajira nchini, akatokea mtu ambaye anapinga wazo hili na hii ni changamoto ya Kitaifa ambayo ni lazima tuikabili kwa nguvu zote na changamoto hii ili tuweze kuikabili, Wabunge makini tumefanya tafiti za kutosha, tukabaini ni namna gani tunaweza kupendekeza na kuishauri Serikali yetu ili tuweze kuwakomboa vijana wa Kitanzania. Wabunge wote hapa siku ya Ijumaa nimewasikiliza na nimesoma michango yao, wali-*rise above party ideologist*, waliiangalia Tanzania kwanza, hawakuangalia vyama vyao, isipokuwa mtu mmoja tu na ndiyo maana nimeamua ku-*deal* naye kwa kuchambua hoja moja kadri alivyozieleza hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimeamua leo kumtaarifu Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba mimi ni Msomi wa Uchumi katika hatua ya *Masters* na sasa nafanya *PhD* kwenye mambo ya *policy* za uchumi, hii ni ili afahamu

kwamba ninapoongea mambo haya ya uchumi, ninayaelewa vizuri na kwamba hoja anazozijenga hapa kisheria, kuleta uanaharakati ndani ya Bunge, hazitoweza kupingana na hoja za kitaalam ambazo zimejengwa kwenye nadharia, kwenye *model* na kwenye fikra ambazo zimefanyiwa tafiti mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwelimishe mchangiaji huyu kwamba katika upungufu ambao alisema upo katika hoja yangu ni kwamba hakutakuwa na dhamana ya mikopo, hili ni tatizo la kiuielewa tu, mikopo itakuwa inatolewa kwa dhamana za Serikali. Kwa mfano, leo hii tunaongelea Bakhresa, Reginald Mengi wamekuwa ni matajiri wakubwa wanaotambulika katika nchi yetu, wapo kwenye *top five* kwenye *list* ya matajiri katika nchi yetu, lakini hawa watu haikutokea wakawa matajiri namna hii ghafla, haikutokea wakawa matajiri kwa kubahatisha tu, hapana! Kulikuwa kuna mfumo uliowawezesha kufika pale na ndiyo ninachokiongea hapa, ni lazima kuwe kuna uwezeshi wa namna fulani. Akina Bakhresa na akina Mengi walifaidika na mikopo ambayo ilikuwa inatoka *World Bank* kupitia Benki Kuu, wakapata mitaji, wakawekeza kwa sababu walikuwa na *discipline*, wakatajirika. Sasa leo hii tunawasifu ni matajiri wakubwa katika nchi hii lakini waliwezesha na mfumo. Nachokiongea hapa ni kwamba, ni lazima Serikali iingilie kati, iwawezeshe vijana wa Kitanzania leo ili waweze kushiriki katika kujenga uchumi wetu, ili waweze kushiriki katika kujitajirisha na kwa kufanya hivyo tutazalisha ajira, tutakuza uchumi wetu na tutakuza *GDP* yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huyu ndugu yangu yeye haelewi hilo, kwamba unaweza ukafanya...

## **T A A R I F A**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, nimekuona, kwa kifupi jamani!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisome ukurasa wa 35 wa hoja binafsi ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kuhusu dhamana, inasema kwamba, mikopo itakayotolewa katika mchakato huu itakuwa ni yenye masharti nafuu kama ifuatavyo, *item* ya mwisho inasema:-

*“isiwe na masharti ya dhamana/security za mali (maana vijana hawana assets zozote) bali iwe na ‘dhamana’ maalum kama cheti cha elimu/ujuzi kwenye fani husika...”*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa anasema kwamba sijamuelewa alisema kutakuwa na dhamana ya Serikali, maneno yake mwenyewe yanasema kusiwe na masharti ya dhamana za mali, unatoa fedha, mikopo benki kusiwe na dhamana ya mali!

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara amesema Mfuko wa Mikopo ya Vijana umekuwepo tangu mwaka 1994 na umekuwa unatoa pesa,

sasa hii hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ya kuanzisha Mfuko mpya wa Mikopo kwa Vijana unaonesha hakuna tafakuri, hakuna fikra. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge aliyetoka kuongea haelewi anachokisema na pengine ninaomba usimpe nafasi tena ya kutoa Taarifa maana anaweka hadharani ni namna gani haelewi ninachokiongea. Maana yake ni kwamba mchangiaji huyu anajielewa ni namna gani hajui uchumi.

**MBUNGE FULANI:** Mtaje jina!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Nimtaje jina, anajulikana ni huyu Tundu Lissu! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba taarifa yake siipokei na nitaelezea, angetulia kidogo tu ningeshafika kuelezea hicho anachokisema. Ninachokisema ni ukweli mtupu, kwamba vijana wa Kitanzania ni watoto wa maskini kama mimi, ukiwategemea watakuwa na jumba kama hili, ukiwategemea watakuwa na Ghorofa za kuweka amana ili wakope wakajenge viwanda, hawawezi mpaka tutakufa, mpaka na wao watakufa hawataweza kufika huko, watatoa wapi dhamana? Sasa tunaongelea tuwatoe vijana, watoto wa maskini kutoka pembezoni, tuwaweke katikati, tuwawezeshe, tuwatengenezee mfumo rahisi wa kupata

mikopo ili waweze kuwekeza, ndiyo tunachokiongea hapa.  
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata akina Ndugu Mengi nilikuwa nawaeleza walipata fedha kutoka kwenye *Commodity Import Support*, walipata mikopo nafuu, waliweka mali gani, walipata mabilioni ya pesa? Hawakuweka mali, walipewa dhamana za karatasi kutoka Benki Kuu. Hizi ndiyo dhamana ninazoziongelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtu huyu hajui, naomba nimtaarifu kwamba hapa tunaongelea mambo ya *Export Credit Guarantee Schemes*, hapa tunaongelea mambo ya *Central Government Guarantees* ambazo zinapatikana kutoka Benki Kuu, hizi ni karatasi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mfuko utanzishwa, Benki itanzishwa na ikawa na maelekezo hayo kwamba, wapate mikopo, dhamana atakuwa ni Serikali, kupitia hayo ma-*guarantee schemes* mbalimbali yaliyopo; hawa vijana watakopa, watapata mikopo, watawekeza, watatajirika. Kama tutaamua, njia nyingine ambayo nime-*suggest* pale ambayo ni rahisi sana kwamba, kwa kuwa, watakuwa wanasimamiwa na huu Mfuko ambao tunauongelea, basi hawa vijana sasa wanaweza vile vyeti vyao vya vya Shahada walivyopata kwenye chuo, vikachukuliwa, vikatunzwa mahali, tukatambua kama ni dhamana tukawapa pesa wakaenda kufanya kazi, hilo nalo linawezekana tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwani dhamana maana yake ni nini? Dhamana maana yake ni kitu

kisichohamishika, kinaweza kikawa ni karatasi, kinaweza kikawa ni nyumba. Yeye dhamana anayojua huyu mtu ni dhamana ya nyumba, mtoto wa maskini kama yeye kutoka kule kijijini ana nyumba gani? Nyumba ya nyasi ile anaweza akaweka dhamana ya kupata bilioni moja? Haiwezekani! Tunaongelea kuwasaidia watoto wa maskini, lakini huyu Mbunge, anatoka kwenye Jimbo maskini kabisa, lina watu maskini, tunaongelea hapa kujipanga namna ya kuwawezesha, lakini yeye anapinga; eti mikopo hii isitolewe mpaka kuwe na dhamana, sasa dhamana watazitoa wapi Watanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ni watu maskini. Mimi mwenyewe natokea kwenye nyumba ya maskini mpaka leo hii hatujaiwekea umeme, bado ni ya *biscuit*. Ile nyumba hata thamani ya shilingi milioni 10 haifikishi, labda kiwanja tu. Ndio nyumba ambayo ninatokea mimi, asili yangu; sasa ukisema nitaweka dhamana ile nyumba, nitapata shilingi ngapi? Kama nyumba ina thamani ya shilingi milioni 10, utapata shilingi ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukiweka hiyo...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu kuonyesha kutoafikiana na alichokuwa akieleza Mhe. Dkt. Hamisi Kigwangalla hapo juu)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilinde.



**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba uvumilivu, tumsikilize Mtoa Hoja.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimegundua kwamba hili darasa ninalolitoa hapa, lina wanafunzi wengi sana wanaohitaji. Naomba sasa niseme kwamba, mtu ambaye anapingana na Hoja hii na huyu si mwingine, ni Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, kuanzia leo nambandika lebo kuwa ni adui wa vijana wa Tanzania, kwa sababu, amejionesha waziwazi kupinga mkakati ambao utawawezesha vijana wa nchi hii.

*(Hapa Mhe. Tundu A.M. Lissu alikuwa amesimama kuomba nafasi ya kuongea)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Kwa sababu anaendelea kupinga na sasa anasimama tena kutaka kupinga kwamba, huu mpango usitekelezeke. Ninaomba vijana wa Kitanzania, walielewe hilo na ninaendelea mbele kwenye Hoja nyingine. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Tundu Lissu, atulie dawa iingie.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kafulila, nimekuona.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ananitukana, mimi nilitulia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kafulila!

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchungu kabisa, ajenda ambayo iko mbele yetu inahusu ajira, inahusu mikopo kwa vijana katika Taifa maskini. Ukweli, namna ambavyo mjadala unakwenda, pamoja na usomi ambao baadhi yetu tumekuwanao, busara ambazo baadhi yenu mmekuwa nazo, tunashusha heshima ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, pamoja na hasira ambazo anazo, atuhitimishie Hoja vizuri kwa sababu, jambo hili ni muhimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, hitimisha tafadhali kwa sababu, muda uliobaki ni mdogo sana kwa upande wako.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kutoa dawa kama ifuatavyo; nianze kwa kumnukuu Msomi mmoja ambaye anaitwa Albert Kemas ambaye aliwahi kusema kwamba:-

*“It is the job of thinking people not to be on the side of the executioners”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitarudia:-

*“It is the job of thinking people not to be on the side of the executioners”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vijana wa Kitanzania, wamjue *Executioner* ninayem-refeer hapa na wamshughulikie ipasavyo, wasiwe upande wake na hata kama atajitahidi kuwatongoza, wamkatalie. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nchi ni ya kwetu sote. Huwa tukishuhudia watu wakikosa heshima hapa hata kwa Rais wa Nchi hii, wengine roho inatuma kweli, lakini tunanyamaza tu, tumekuwa kwenye Bunge hilihili, lakini leo hii kumsema tu mtu mmoja kumwambia ukweli, tena kumwelimisha tu kistaarabu, inakuwa dhahama kubwa, Wabunge wanashindwa kuvumilia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwe tuna tabia ya kuvumiliana ili tuweze kuzilinda tunu za Taifa hili za umoja, amani, upendo na mshikamano. Tuvumiliane, tujenge hoja kwa heshima wenzetu wanapoongea na hiyo ndiyo heshima ya Kibunge, ndio heshima ya kisomi; Mheshimiwa Tundu Lissu, amesoma, anafahamu hilo. Huwa tunapingana kwa hoja, sio kwa matusi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kama ana vyeti bandia!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wamekuwa na tabia za kudanganya tu na kusema uwongo.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, kuna Mheshimiwa amesimama hapa.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa masikitiko makubwa, tena makubwa sana, sisi wengine hapa Wabunge, tuna hamu kubwa ya kusikiliza hoja inahitimishwa lakini badala yake hapa pamezuka malumbano. Kwa hivyo, tunawaomba, kama wana malumbano yao, waende nje huko, hapa pazungumzwe hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri sote humu ndani tunaona yale ambayo nimekuwa nikisisitiza mara kwa mara. Yale ambayo Mheshimiwa Spika amekuwa akisisitiza mara kwa mara kwamba, katika lugha zetu tujitahidi kadiri tunavyoweza, ili ujumbe uweze kufika. Kwa hiyo, ninawaomba kwa mara nyingine Waheshimiwa Wabunge wote kabisa, tujitahidi kusikiliza kwa umakini hoja hii muhimu sana, ambayo imeletwa mbele yetu na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, bila kusumbuliwa tena, hebu malizia tafadhali.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ninaomba niendeleee. Kuna Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, alichangia na akasema kwamba, kumekuwa kuna wingi wa Mifuko. Mimi sio wa kujibu hilo, lakini kwa kuwa, mimi nina Hoja tu ya kuanzishwa kwa Mfuko, ninaomba nikubaliane naye kwamba, kuna uwezekano mkubwa huko nyuma mifuko haikuwahi kuwa na tija sana katika kukuza ajira katika nchi yetu lakini

ninaomba nimtaarifu tu kwamba, Hoja hii ya kwangu ya kuanzisha Mfuko, inaitaka Serikali, ikaanzishe Mfuko ambao utaleta nguvu mpya na Hoja hii wala haikatai kuunganishwa kwa Mifuko hii yote ama kutafuta namna ya kui-*coordinate* hii Mifuko yote iliyopo na kuweza kutengeneza Mfuko mmoja wenye nguvu, ambao utaweza kutusaidia kupata ufumbuzi wa tatizo la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, katika mchango wake alisema kwamba, benki sio suluhu na akasema kwa sababu mpaka sasa hivi kuna utata mkubwa sana uliopo katika kupata mikopo ambayo inapatikana kwenye Benki ya Rasilimali. Mimi ninakubaliana na huu mchango na hoja yake lakini ninachokisema hapa ni kwamba, ugumu wa kupata mikopo ndio haswa tatizo ambalo katika Hoja yangu, ninapendekeza lipatiwe ufumbuzi, kwamba, tupate ufumbuzi wa kutatua tatizo la upatikanaji wa mikopo kiurahisi kwa Watanzania, hususan vijana, kwenye Hoja hii ambayo ninaiongelea hapa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kafulila, ninakubaliana na wewe kimsingi kwamba, benki inaweza isiwe *solution*, lakini mimi sikubaliani kwamba, sio *solution*; nakubaliana kwamba, benki ikiwepo, tukaweka utaratibu maalum wa kuwakopesha vijana, tukarahisisha mchakato mzima wa kupata mikopo, vijana wakapata mikopo, tutaweza kupata ile *impact* ambayo tunaitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na yeye alichangia kama Mheshimiwa Kafulila, kuhusiana na Mifuko na Wabunge wengi tu ambao pengine sitawataja. Lakini nipingane na yeye kusema kwamba, kilimo kipo *ICU* kwa sababu kilimo ndio uti wa

mgongo wa uchumi wa Taifa letu. Sisi sote tunaotokea huko Mikoani, Wilayani huko, tunafahamu ni namna gani ambavyo tulitumia kilimo kuweza ku-*generate income* ambayo ilituwezesha kupata ada ya kwenda kusomea shuleni. Sasa ni kilimo ambacho kweli hakipo katika hatua ambayo inapaswa kuwa, kwa sababu, ni kilimo cha jembe la mkono na ni kilimo ambacho hakitumii mbegu za kisasa, hakitumii teknolojia za kisasa, lakini ni kilimo hicho ambacho tunakiongelea hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachokiongelea kwenye Hoja yangu mimi ni kuleta pendekezo la kuamsha ari ya vijana kushiriki kwenye kilimo cha kisasa. Kwa hiyo, tunachokiongelea hapa ni mpango kabambe ambao umeletwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, ile Ibara ya 79 na ile ya 81, imeandikwa wazi kabisa, kuwepo na mpango kabambe. Sasa mimi niliyoleta hii ni kama kutia chachu ya kuanzishwa kwa huo mpango kabambe, ambao utatusababisha sasa kwenda kuwekeza kwa vijana wetu kupitia kilimo cha kisasa, ili waweze kukuza uchumi wetu kupitia sekta hiyo, lakini pia waweze ku-*generate* ajira za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nipingane na Wabunge wengine wote ambao walichangia wakidhani kwamba mpango huu unawahusu vijana wanaohusika na kilimo tu, hapana! Nafikiri kulikuwa kuna tatizo kidogo katika kuweka *titling* ya Hoja hii, lakini ukweli ni kwamba, ukizingatia mabadiliko ambayo yalikuja kufanywa baadaye na Mheshimiwa Ester Bulaya, akazitaja sasa zile sekta zote ambazo zinahusika. Ukweli ni kwamba, sekta zote zitahusika,

lakini tuliweka kilimo kama kipaumbele kwa sababu, kilimo kinaajiri watu zaidi ya 75% katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata Mheshimiwa Maryam Msabaha ambaye alikuwa na mashaka na uwepo wa Mfuko huu kwamba, utahusisha kilimo tu ni kwamba, sekta zote zitahusika. Hapa tunaongea yatengwe maeneo maalum, mahususi, kwenye kila Kijiji, kwenye kila Wilaya, kwenye kila Mji, kwa ajili ya vijana, ili vijana waweze ku-*access* mikopo katika Mfuko huu, waende kuwekeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ilivyo sasa hivi, mashamba kule Vijijini ni ya wazazi. Kijana akizaliwa anakuta ardhi yote ni mali ya familia, haiwi mali yake. Tunachokiongelea hapa ni kutengeneza mfumo wa kuwawezesha vijana nao waweze kumiliki ardhi, waweze kuwa na mali yao, tunaongelea *private property*. Katika mfumo ya kiuchumi, kule kuwa na uwezo tu wa kumiliki *property*, ni kianzio kikubwa sana cha wewe kupambana na umaskini na kujitajirisha. Kwa hiyo, tunaongelea hapa kuwawezesha vijana kupitia mfumo utakaowekwa, ambao utawawezesha kumiliki ardhi, utawawezesha kumiliki maeneo ya biashara wao wenyewe na sio wazazi wao. Kwa sababu, wakisubiria ile ya kurithi, haitaweza kuwasaidia wao kuanza ku-*generate income* wakiwa katika umri mdogo wa maisha yao, wakiwa katika kipindi ambacho wana nguvu zaidi, wanatubutu zaidi kuliko ilivyo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Hoja nzito kabisa katika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Toa Hoja, Mheshimiwa.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu la mwisho kwa kuomba Serikali, wakati inatekeleza mpango huu, ikubaliane na mimi, lakini pia na mapendekezo ya Mheshimiwa Mnyika, ambayo kweli mimi niliyapokea, yanayosema kwamba, kuwepo na ufuatiliaji wa utekelezaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili tayari, kwa hiyo, jitahidi utoe Hoja.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, Hoja iliyo mbele yetu ni ya kuitaka Serikali, ianzishe mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana kwa kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Vijana wanaowekeza kwenye kilimo na viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja na kilimo pamoja na marekebisho yale



yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Ester Bulaya. Sasa naomba kuwahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, kwa pendekezo hili ambalo Bunge hili limeliafiki. Sasa ni wajibu wa Serikali, kuona namna gani bora zaidi ya kulitekeleza jambo hili kwa ajili ya manufaa ya vijana wa Tanzania nzima. Katibu!

**Hoja Binafsi ya Mhe. John J. Mnyika juu ya Kuboresha  
Upatikanaji wa  
Maji Safi na Ushughulikiaji wa Maji Taka katika Jiji la Dar es  
Salaam**

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Ningeomba Miongozo iwe mwisho kabisa kwa sababu muda alionao Mheshimiwa Mnyika ni mdogo sana na ni vizuri tuutumie muda huu, hatuna muda mwingine tena. Mwishoni kabisa, nitaruhusu Miongozo.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea Hoja ya Mheshimiwa John Mnyika, akiwasilisha mabadiliko ya Hoja yake Binafsi ya mwanzo ya kupendekeza Bunge lijadili na kupitisha Maazimio ya hatua za haraka za kuboresha

upatikanaji wa maji safi na ushughulikiaji wa maji taka katika Jiji la Dar-es-Salaam. Katika Hoja yake ya Mabadiliko, Mheshimiwa Mnyika, anapendekeza mambo mapya yafuatayo:-

(a) Kwamba, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), afanye ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha, matumizi ya shilingi bilioni 96.4 za mradi wa maji safi na mazingira vijijini katika Jiji la Dar-es-Salaam na Halmashauri nyingine na kuwezesha hatua za ziada kuchukuliwa.

(b) Na kwamba, kufuatia Kauli iliyotolewa Bungeni, tarehe 7 Novemba, 2012 kuhusu mpango maalum wa kutatua tatizo la maji katika Jiji la Dar-es-Salaam, uliopitishwa mwezi Aprili, 2011, Serikali, izingatie makisio ya awali ya gharama za mpango huu na kuingiza mahitaji yaliyobaki kwenye mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014 na bajeti ya mwaka 2013/2014.

Wahehimiwa Wabunge, kwa kuingiza vipengele hivyo vipya viwili, vinakiuka Masharti ya Kanuni ya 55(12), kwa kuwa, yamebadilisha upeo wa Hoja yake ya awali ambayo inaitaka Serikali ichukue hatua za haraka kutatua matatizo ya maji safi na taka kwa Jiji la Dar-es-Salaam tu. Wakati Mapendekezo ya Mabadiliko ya Hoja, yanataka Serikali, itatue tatizo hilo katika Halmashauri zilizobaki. Kwa hatua hii, Hoja yake ya Mabadiliko ilikataliwa kuwasilishwa Bungeni kwa kuwa, mabadiliko hayo yanaongeza upeo wa Hoja yake ya awali, kinyume na Kanuni ya 55(12).

Hata hivyo, Mheshimiwa Mnyika, amewasilisha kusudio la kufanya mabadiliko ya Hoja yake kwa mujibu wa Kanuni

ya 55(10); haya ya ukurasa mmoja, natumaini mmeshapewa, kama bado yatagawiwa muda si mrefu. Anaomba kurekebisha Hoja yake ya Msingi kwa kurekebisha tarehe na kasoro ndogondogo za kiuchapaji na kuongeza Azimio Jipya ambalo liko ndani ya maudhui ya Hoja. Jambo hilo limekubaliwa ingawaje nimeona kwamba yale ambayo yamekataliwa, kwa namna moja au nyingine yanajitokeza tena kwenye Hoja za Mabadiliko za Wabunge wengine watatu, yaleyale ambayo yalikataliwa, lakini hayo baadaye mtayaamua Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hatua hiyo sasa, naomba nikuite Mheshimiwa Mnyika hapohapo ulipo; jitahidi sana utumie muda uliopo kuwasilisha Hoja yako.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba uniongeze muda kwa mujibu wa Kanuni, ili nipate ule muda unaostahili kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Spika, Hoja yangu inapatikana katika ukurasa wa 37 wa vitabu vya awali ambavyo Waheshimiwa Wabunge walipatiwa, vyenye Hoja zote za Wabunge zilizowasilishwa kwenye Mkutano uliopita wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa marekebisho ambayo umeniruhusu kuyawasilisha kwa mujibu wa Kanuni ya 55(11), yanatokana na kuwa maelezo ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayo pamoja na Hoja yenyewe, yaliwasilishwa kwa ajili ya Mkutano wa Bunge wa mwezi Novemba na niliyawasilisha na siku moja kabla ya mimi kuwasilisha Hoja yangu Serikali ilitoa Kauli Bungeni

tarehe 7 Novemba, 2012 kabla ya mimi kuwasilisha Hoja tarehe 8.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa muda umepita toka wakati huo mpaka sasa na Hoja ile haikujadiliwa wakati huo, naomba Waheshimiwa Wabunge, waelekee kwenye ukurasa wa 44 wa Kijitabu hiki cha Hoja, ambapo kuna mapendekezo sasa ya Maazimio ambayo, ninaliomba Bunge lako Tukufu liyapitishie na kufanya marekebisho yafuatayo:-

(i) Kwenye Azimio la pili, lile linaloanza na maneno, 'Serikali, iwasilishie Bungeni Mpango Maalum', maneno, '2012/2013' yaondoke, badala yake kuingizwe maneno, '2013/2014' kwa kuzingatia kupita huko kwa muda. Aidha, maneno, 'utakaopendekezwa na kuwasilishwa katika Mkutano wa Bunge wa mwezi Februari 2013' yabadilishwe, badala yake yaingizwe maneno, 'mwaka 2013/2014'.

(ii) Kwenye Azimio namba tatu linaloanzia na maneno, 'mpango wa dharura wa kupunguza kero ya maji ulioanza kutekelezwa na Wizara ya Maji kwa kushirikiana na DAWASA'. Maneno nambari '24' yabadilike badala yake yawekwe maneno, nambari '29' na maneno, 'Disemba 2012' yabadilike badala yake tuingize maneno, 'Desemba 2013'.

(iii) Kwenye Azimio namba sita na kwenye ukurasa wa 45 mabadiliko yafanyike ili badala ya maneno 'Mkutano wa Kumi' yaingizwe maneno 'kabla ya mwaka 2014'. Aidha, badala ya maneno 'Sheria ya Maji Safi, Maji Taka ama (*Water Supply and Sanitation Miscellaneous Amendment*

*Bill*) yasomeke maneno 'Sheria ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam yaani *Dar es Salaam Water and Sewerage Authority Act*. Vilevile kuondoa maneno 'nchini' badala yake kuingiza maneno 'Jiji la Dar es Salaam'.

(iv) Kwenye Azimio namba saba kufanyike marekebisho kwenye Azimio linalohusu Kamati ya Bunge kujadili taarifa, kuondoa maneno 'mara baada ya Mkutano wa Tisa wa Bunge' na baada ya maneno 'mpango wa taifa' yaongezwe maneno 'na bajeti ya nchi'.

(v) Sasa Azimio jipya ambalo naomba liongezwe pamoja na lile ambalo Mheshimiwa Naibu Spika umekwishalisoma ni kwamba Serikali itoe taarifa Bungeni sababu za *program* ya maji safi na mazingira yaani *RWSSP* ambayo ilipaswa kutekelezwa kwenye Manispaa za Temeke, Ilala na Kinondoni kati ya mwaka 2005/2006 mpaka 2010/2011 kutokamilika mpaka 2013 na kuwasilisha ratiba mpya ya utekelezaji wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ambao hawakuwa na hii karatasi, naamini karatasi hii itawasilishwa katika hatua za baadaye. Kwa hiyo, nitaendelea kusoma hoja yangu na kutoa maelezo ni kwa nini hasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge muweze kuipitisha hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile niwasilishe Mezani kwako *addendum* ya maelezo. Kama nilivyodokeza katika utangulizi wangu, maelezo yaliyoko kwenye kitabu cha Waheshimiwa Wabunge yalikuwa ni ya tarehe 8

Novemba na niliyawasilisha kabla ya mwezi Novemba na kabla ya Serikali kutoa Kauli yake Bungeni. Baada ya Kauli ya Serikali, maelezo haya naomba yote kwa ujumla wake yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge kama yalivyo, lakini yaongezwe maelezo ya ziada katika ukurasa wa 42 baada ya jedwali la mahitaji ya fedha ya Mpango Maalum wa Maji - Dar es Salaam, kuingizwe maelezo haya ambayo nitayasoma na kabla sijayasoma, naomba nakala ije kwako ili wakati nayasoma kama kuna jambo la angalizo liweze kutolewa angalizo lakini hii ni *addendum* na ni *addendum* ya mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuungana na wote wenye mapenzi mema katika kuomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu wakati huu tukitimiza wajibu wa Kikatiba, wa Kibunge kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwawakilisha wananchi na kuisimamia Serikali kuidhinisha mipango pamoja na kutunga sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa namna ya pekee, nikushukuru wewe binafsi, uongozi mzima wa Bunge kwa kunipa fursa hii adimu na adhimu ya kuwasilisha hoja binafsi kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1) ya kupendekeza Bunge lijadili na kupitisha Maazimio ya hatua za haraka za kuboresha upatikanaji wa maji safi na ushughulikiaji wa maji taka katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu ziwafikie Wabunge wenzangu wa Vyama vyote vya Upinzani na wa Chama Tawala, kwa maoni na mapendekezo yao yaliyoniwezesha kuirekebisha hoja hii pamoja na ushauri wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Maafisa na

Watendaji wa Ofisi ya Bunge, Kambi Rasmi ya Upinzani na Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Ubungo, mlioboresha Hoja hii kwa manufaa ya Jiji la Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii vilevile kuwashukuru Watanzania wenzangu wa kada, hadhi na ngazi mbalimbali katika Taasisi na maeneo mengi ndani na nje ya nchi, mnaoendelea kuniunga mkono kwa hali na mali katika kutimiza majukumu ya Kibunge na nafasi nyingine ninazowatumikia. Naomba sala zenu wakati wote tukitimiza majukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, pamoja na mjadala huu Bungeni, natarajia kupokea maoni na mapendekezo kuhusu Hoja hii kupitia mtandao wa '*Mnyika.co.com*' kwa hatua zaidi. Kauli mbiu yetu ni ileile 'Amua Maslahi ya Umma Kwanza'.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni mojawapo ya mahitaji ya msingi ya binadamu, maji ni uhai. Upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama, ni sehemu muhimu ya upatikanaji wa maendeleo ya nchi na maendeleo ya wananchi. Maji ni lazima kwa matumizi ya majumbani, maji ni malighafi muhimu katika ngazi za uzalishaji iwe ni viwanda, kilimo, mifugo na shughuli nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji safi na salama kwa urahisi, unachangia katika kupunguza gharama za maisha na upatikanaji wa maji safi na salama karibu na makazi, huisaidia jamii hususani wanawake kutumia nguvu na muda katika uzalishaji na hivyo

kuchangia katika kupunguza umaskini. Upatikanaji wa maji safi na salama, ni nyenzo ya kulinda utu na afya, kinyume chake ni kuenea kwa magonjwa na maisha duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Toleo la mwaka 2005 haijataja haki ya kupata maji safi na salama na huu ni moja ya upungufu ambao wananchi mijini na vijijini wanapaswa kuutolea maoni katika mchakato wa Katiba ili Katiba yetu iweke haki ya maji kama zilivyo Katiba za Ghana, Kenya na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya sasa, haki hii inapaswa kulindwa kupitia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (*The International Covenant on the Economic and Social and Cultural Rights*) wa mwaka 1966. Mkataba huu unataja haki za kijamii ikiwa ni pamoja na haki ya kupata maji safi na salama ambayo inapaswa kutiliwa mkazo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam ni letu sote, ni mahali ambapo Wabunge tunaishi kwa nyakati mbalimbali hususani wakati wa vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge, hivyo adha ya maji katika Jiji la Dar es Salaam kila mmoja wetu anaifahamu na ana wajibu wa kushiriki katika kulipatia ufumbuzi. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na jumla ya wakazi 2,497,940 huku ikikadiriwa kuwa na kasi ya ongezeko, naomba rekebisho, ya 6% kwa mwaka. Hadi kufikia mwaka 2011, Jiji la Dar es Salaam linakadiriwa kuwa na watu takribani 4,500,000 likiwa na takribani nusu ya waajiriwa wote wa viwanda nchini.



Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam miaka michache baada ya mwaka 1961, ulikuwa zaidi ya 68% hivi sasa baada ya uhuru tumerudi nyuma na upatikanaji wa maji Dar es Salaam ni wastani wa 55% tu tena kwa mgao. Katika mazingira haya, hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa kuhusu hali hii na ukizingatia kuwa idadi ya watu katika Jiji la Dar es Salaam inaendelea kukua kwa kasi na ni Jiji la tatu kwa ongezeko kubwa la watu barani Afrika na ni la tisa Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoieleza awali, nitaomba maelezo yote yanayofuata baada ya hapo, kutokana na muda, yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge na naomba niongeze maelezo kama ambavyo nilivyoieleza kwenye ukurasa wa 42 baada ya jedwali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ile *addendum* sijaipata bado.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilishanyoosha ije kwako muda mrefu sana.

**NAIBU SPIKA:** Endelea!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mabomba ya Mchina bila maji na miradi hewa kwa wananchi wa kipato cha chini Jijini Dar es Salaam. Kati ya mwaka 2003 mpaka mwaka 2010, Serikali ilitekeleza mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka jijini Dar es Salaam na maeneo ya Bagamoyo na Kibaha yaani *The Dar es Salaam Water Supply Sanitation*

*Project.* Mradi huu ulitumia dola milioni 164.6 yaani zaidi ya bilioni 260 hata hivyo mpaka sasa katika maeneo mengi mtandao wake maarufu kama 'mabomba ya Wachina' hautoi maji huku kukiwa na upungufu wa uzalishaji, upotevu wa maji, udhaifu katika usambazaji na tuhuma za ufisadi katika matumizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ni kati ya matatizo yanayokera wananchi wa Dar es Salaam kwa kuwa mabomba yasiyotoa maji kwa muda mrefu hata wakati wa mgao, yaani 'mabomba ya Wachina' ni sehemu ya kashfa katika Taifa letu. Serikali ilieleze Bunge hili sababu ya mabomba hayo kutokutoa maji mpaka hivi sasa, lini mabomba hayo yataanza kutoa maji katika maeneo ambayo maji hayatoki mpaka sasa na hatua gani zinachukuliwa kwa waliotekeleza mradi huo bila kuzingatia maandalizi ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kuwa hatua zikachukuliwa kwa wahusika kwa kuwa kitendo cha mabomba hayo kukaa muda mrefu bila kutoa maji, inafanya miundombinu hiyo kuanza kuharibika na kuharibiwa ambapo ni hasara kwa Taifa pamoja na fedha zilizotumika kuweka mabomba hayo kupotea. Fedha nyingine zitatumika katika hatua ya baadaye kufanya matengenezo kwa maeneo yaliyoharibika ambayo ni hasara mara mbili kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, yapo malamiko kwamba yapo maeneo ambayo yalitoa maji mara chache sana kati ya mwaka 2009/2010 lakini baada ya hapo maeneo hayo hayatoi maji tena mpaka sasa. Serikali itoe

maelezo ya kitaalam kwa Bunge na kwa wananchi kuhusu sababu za maji hayo kutokutoka wakati huo na kutokutoka mpaka sasa na ichukue hatua ya kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasoro katika mradi wa ukarabati wa upanuzi wa miundombinu wa maji safi na maji taka Dar es Salaam na maeneo ya Bagamoyo na Kibaha yaani Dar es Saalam *Water and Supply and Sanitation Project*, haielezwi na wananchi pekee bali hata watafiti mbalimbali. Ripoti ya hivi karibuni kabisa ya mwaka 2012 ya Shirika la Kimataifa la *Water Aid* ya utafiti uliofanywa kwa kuhusisha wataalam wa *Overseas Development Institute* na Chuo kimoja cha nchini Uingereza cha *Chaos* vilivyofuatilia uwekezaji wa miradi ya maji mijini katika nchi za Ghana, Burkina Faso na Tanzania yaani *The Strengthening for Poor Targeting of Investment by African Utilities in Urban Water Supply and Sanitation*, ikiwemo, imetaja miradi mbalimbali iliyoshindwa kufanya kazi ipasavyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Mnyika, nimemwona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naona hayo anayosoma wengine hatuna! Anasoma vitu vingine kuliko ile hoja aliyokiri kwamba anawasilisha.

**MBUNGE FULANI:** Iko Mezani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Suala sio kuweka Mezani lazima tuwe nayo wote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Mnyika unatupoteza kabisa sote na mimi nilikuwa natafuta hapa, tunapaswa twende wote kwa kitabu kile ambacho Wabunge wote wanacho.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwisha kueleza kwamba ni *addendum* na nimekwishaiwasilisha Mezani kwako. Utaratibu ufanyike wa kutolewa nakala na kama Mheshimiwa Waziri anataka nakala nitampa nakala ninayo nyingine hapa ili afuatilie.

**MBUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa Bunge lako na kwa desturi za Bunge hili, imekuwa ni kawaida kidesturi za hapa kama mtu anapendekeza marekebisho au ana maelezo ya nyongeza hapa mbele anayaleta hapa, yanaletwa Mezani na yanaendelea kusomwa wakati taratibu nyingine zinaendelea. Kwa hiyo, naomba ulinde muda wangu wakati naendelea kuwasilisha maelezo haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Mnyika, kwa kawaida hata kama ni *addendum* inakuwa imewasilishwa Ofisini na mimi hapa Mezani napata ambayo imegongwa muhuri wa Ofisi ambacho nimepata hapa ni kutoka tu kwako, sasa mnanichanganya kati ya wewe na Ofisi yangu pale kwamba kipi ni kipi, ni kipi ulikipeleka kikakataliwa, kipi kipo sawa na kitu muhimu sana hapa siyo maelezo haya ambayo ni muhimu katika kujenga hoja lakini kitu muhimu sana ni maelezo yako ya hoja hasa kuliko tukianza

kulumbana kwenye *addendum* ambazo ndiyo nazipata hapa kwa hapa. Hebu ningeomba unisaidie kidogo kwa sababu ya lil lile suala la muda wetu kwamba uweze kuutumia vizuri.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeleee na jambo la msingi, ni kwamba maelezo ninayoyasoma nilikwishayawasilisha kwenye Ofisi kwa nyakati mbalimbali, kwa hiyo, siyo jambo jipya sana. Kwa hiyo, naamini hata Spika angekuwepo hapo Mezani angekuwa na uelewa wa haya maelezo ambayo ninayowaelewesha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Mnyika, kaa chini kwanza, unaposema maneno hayo maana yake ni kwamba mimi sina uelewa, siyo? (*Kicheko/Makofi*)

Nimemsikia Mbunge wa Tunduma akiropoka huko, ningeomba tuheshimiane sana katika kazi za umma hizi, kuleta utoto humu ndani haisaidii sana na kudharauliana kirejareja haisaidii sana. (*Makofi*)

Tunakwenda kwa taratibu zilizopo, kile ambacho unakileta wewe hapa Mbunge iwe ni hoja ya mabadiliko, ni nini, ina utaratibu wake inakuwa na mhuri wa Ofisi kunithibitishia mimi kwamba kitu hiki ni *official* tayari. Vyote, hata mabadiliko ambayo yataletwa na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, ninayo hapa, mabadiliko yatakayoletwa na Mheshimiwa Susan Lyimo, ninayo hapa, mabadiliko yatakayoletwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura, ninayo hapa, kila kitu nakuwa nacho kwa utaratibu. Hamnipi tu hapa Mezani, ulipokaa hapo

unasema kama huna, chukua. Huo ndiyo uelewa unaouzungumza ambao mimi sina? Tufuate taratibu Bwana, hebu endelea na tusidharauliane. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba nikupe nakala ya maelezo ambayo yana mhuri wa Ofisi ili sasa niweze kuendelea kusoma maelezo haya ambayo yana mhuri wa Ofisi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nakuona umesimama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema, tunaongozwa na Kanuni kwa sababu kabla ya hapo ulishatuambia kwamba na ukasoma barua ambayo Mheshimiwa John Mnyika amejibiwa kuhusu baadhi ya hoja zake. Sasa tunavyofahamu kwamba tunaanza na Kanuni ya 55, fasili ya kwanza ambako kulitolewa taarifa ya hoja lakini pia Mheshimiwa Mbunge anaweza kufanya marekebisho au mabadiliko kwenye hoja yake fasili ya kumi ambayo inasema:-

*“Iwapo Mbunge anapenda kufanya mabadiliko ya maneno aliyoyatumia katika hoja anayokusudia kuitoa, anaweza kufanya hivyo kwa kutoa taarifa ya kutaka kufanya mabadiliko angalau siku moja kabla ya siku ile ambapo hoja hiyo imewekwa kwenye orodha ya shughuli ili ijadiliwe.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo fasili ya 11, inasema:-

*“Mbunge ambaye hakutoa taarifa ya kutaka kufanya marekebisho au mabadiliko katika hoja yake, anaweza kumwomba Spika afanye marekebisho au mabadiliko katika hoja hiyo wakati anawasilisha hoja yake bila ya kutoa taarifa”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, fasili ya 12 inasema:-

*“Pamoja na kuwa taarifa ya kutaka kufanya marekebisho au mabadiliko itakuwa imetolewa, marekebisho au mabadiliko yoyote hayatakubaliwa kama kwa maoni ya Spika mabadiliko hayo yanabadilisha mambo ya msingi yaliyomo katika hoja au yanabadilisha makusudio au upeo wa hoja hiyo”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tunacholalamika ni kwamba maneno anayosema Mheshimiwa John Mnyika sisi hatunayo na kwa ajili hiyo kwa upande wa Serikali itakuwa vigumu sana kufuatilia hicho anachozungumza kusudi Serikali itoe majibu sahihi kwa Mheshimiwa Mbunge, nafikiri tuongozwe na kanuni zaidi kuliko utashi.

**NAIBU SPIKA:** Nimewasiliana na Ofisi ya Katibu wa Bunge, wamenithibitishia hapa kwamba walikwishapokea hiyo kitu ya John Mnyika, Mheshimiwa John Mnyika endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Tutaongeza dakika chache, zile dakika tano ambazo zilikuwa zimepotea mwanzo ili Mheshimiwa John Mnyika aweze kwenda na muda wake ule.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya kuwa na mabomba yasiyotoa maji hayapo tu katika mabomba waliyofungiwa wananchi majumbani bali pia yapo kwenye visima na vioski vya maji vya jumuiya yaani magati ya maji. Kuna udhaifu katika kuendesha miradi ya jamii na kuacha kusimamia uendelevu yaani *sustainability* na hatimaye baada ya muda mfupi miradi hiyo iliyotumia fedha za umma imebaki kuwa miradi hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa vituo vya maji uliofanywa Juni 2009 na *Oversea Development Institute* chini ya udhamini wa *Water Aid*, umesema kuwa 54% ya miradi ya maji na vituo vya maji nchini vilivyofunguliwa havifanyi kazi, havina maji. Hivyo kwa wastani baada ya miaka miwili tu toka kujengwa, nusu ya visima na vioski huwa haviendelei kufanya kazi. Utaratibu wa kukimbia kutumia fedha za miradi ya maji mwaka mpya wa bajeti bila kuzingatia taarifa za utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya nyuma, ni hatari kwa uendelevu wa kuwepo kwa huduma ya maji kwa siku zijazo kama hatua za haraka hazitachukuliwa kuzingatia matatizo yaliyojitokeza katika miradi iliyopita na kuzingatia ubora na ufanisi katika miradi ya maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafafiti uliofanywa na *the Economic and Social Research Foundation* ubaini utofauti wa utekelezaji baina ya miradi ya Serikali na mashirika



binafsi katika kuhakiki matumizi ya fedha na huduma za jamii.

Utafiti ulibaini kuwa miradi inayofadhiliwa na mashirika ya maendeleo kwa wastani asilimia 67 ya *viosk* ilionekana kufanya kazi wakati miradi iliyofadhiliwa na Serikali ni wastani wa asilimia 45 tu ya *vioski* vya maji ndivyo vilikuwa vikifanya kazi katika maeneo mbalimbali nchini. Hali ni mbaya zaidi kwa upande wa Dar es Salaam ambapo kwa mujibu wa utafiti mwingine wa Shirika la *Water Aid*, umebainisha kuwa asilimia 85 ya *viosk* vilivyounganishwa jijini Dar es Salaam havitoi maji, asilimia 10 ndiyo vinatoa maji kwa kusuasua na asilimia tano tu ya *viosk* vya maji kwa Mkoa mzima wa Dar es Salaam ndiyo vinatoa maji kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasoro katika utendaji na uwajibikaji wa mamlaka na vyombo vinavyohusika na utoaji na udhibiti wa huduma ya maji, majukumu ya utoaji na huduma ya maji jijini Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Kibaha na Bagamoyo yanafanywa na Mamlaka ya Maji safi na Maji taka, yaani *DAWASCO*, ambao ni mmiliki, mkodishaji na wasimamizi wa utoaji wa huduma za maji safi na maji taka na inawajibu wa kupanga na kugharamia utekelezaji wa miradi ya miundombinu na kuiendeleza na kugharamia matengenezo ya dharura.

Mwaka 2005 *DAWASA* iliingia mkataba wa miaka kumi ya uendeshaji wa Shirika la Maji safi na Maji taka Dar es Salaam, yaani *DAWASCO*. Iliingia Mkataba na *DAWASCO* chini ya mkataba huo. Majukumu ya *DAWASCO* ni

kuendesha mitambo, kusimamia usambazaji wa maji na uendeshaji wa Maji taka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, Wasaidizi wako wananiambia kumbe hata hii ambayo ina muhuri ni wewe umeitoa, siyo Ofisi yangu ndiyo imeniletea. Hii ambayo unaisoma ndiyo Kumb. Na. OMU/BJMT/007/2013 ambayo umeshaandikiwa barua na Katibu wa Bunge na ulishapata nakala kabla ya hapa ambayo imekupa maelezo yote ya undani kuhusu *same document* na walishawasiliana na wewe.

Sasa ninachoshindwa kuelewa, kwanini unang'ang'ania jambo hilo badala ya kuchukua kitabu chako kile cha hoja yako ya mwanzo na kuisoma ukaturahisishia uelewa wa Wabunge wote walio humu ndani, kuliko utaratibu ambao unaamua kuuchukua wa kukaidi maelezo ambayo mlikwishawasiliana na Katibu wa Bunge, na tayari unayo na barua na bado unaendelea na *document* ile ile ambayo ulikuwa umekataliwa? Mimi nimeisoma hapa, maelezo ni kwamba ile ya mwanzo achana nayo, kinachokubalika ni mabadiliko haya ya ukurasa mmoja ambayo umeyaleta wewe mwenyewe. Haya yanakubalika, lakini hii *volume as a document*, hii tayari unayo maelezo na nakala za barua unazo, sasa unachokifanya ni nini?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naheshimu sana Kiti chako na naamini Kiti chako kinafanya kazi bila upendeleo. Maelezo ninayoyotoa siyo marekebisho ya maazimio haya na ni maelezo ambayo Ofisi yako inayo na Ofisi yako iliniandikia barua, sitafanyia

*reference* kwa sababu imegongwa muhuri wa siri. Barua hiyo nikaijibu na leo nimekuwa na majadiliano na Ofisi yako na ndiyo marekebisho haya yamekuja.

*(Hapa Mheshimiwa Tundu M. Lissu alisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu anapokuwa Mbunge wako anaongea na wewe mwenyewe umesimama, lengo lenu sasa nifanyeje?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba apewe nafasi kwa sababu amesimama, halafu na mimi nitaongea.

**NAIBU SPIKA:** Basi unakaa chini ili tumpe nafasi yeye.

*(Hapa Mheshimiwa John J. Mnyika alikaa)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nimeogopa sana maneno ambayo unayasema kuhusu mawasiliano aliyopatiwa Mheshimiwa Mnyika kwamba ameandikiwa barua na Katibu wa Bunge ikimkataza kufanya marekebisho katika hoja yake. Ninavyofahamu, utaratibu wa kanuni zetu za kudumu, utaratibu uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haumpi Katibu wa Bunge au Watumishi wa Bunge mamlaka yoyote ya kukataa hoja yoyote ya Mbunge. Mamlaka ya kuzuia hoja ya Mbunge ni Mamlaka ya Bunge hili na ni Mamlaka ya Kiti chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, barua kama imeandikwa na Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Mnyika

alikuwa na haki kabisa ya kuipuuza kwa sababu mwenye mamlaka ni wewe. Kama Mheshimiwa Mnyika anakatazwa, akatazwe na Kiti siyo na Katibu wa Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana na kwa hili ambalo umelisema ambao uko sahihi kabisa. Kabla ya Mheshimiwa Mnyika kusema chochote, mimi nilisoma maelezo ya kitu kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Mnyika. Kwa hiyo, nilichokifanya ndicho *exactly* unachokieleza kumkataza kwamba yale asiendelee nayo, aendelee kama alivyokuwa ameiwasilisha hapa ndani na marekebisho ya ukurasa mmoja yanayorekebisha hoja yake kwa maana ya zile tarehe ambazo zimepitwa na wakati na mambo mengine ambayo ninayo na natumaini Waheshimiwa Wabunge mnayo hii ya ukurasa mmoja.

Kwa hiyo, ni vitu viwili ambavyo nimeviruhusu, hoja kama ilivyo katika kitabu cha hoja kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wote, hata Mheshimiwa Nassari atakapokuja kesho au siku inayofuata atawasilisha kwa kadri ya kitabu hiki ambacho ninacho.

Mheshimiwa Mnyika anaruhusiwa na marekebisho aliyoyaeleza ukurasa mmoja. Hivi vitu viwili mwongozo huo nimekwishautoa. Mheshimiwa Tundu Lissu kwa hiyo, tuko *in order*. Mheshimiwa Mnyika endelea muda wako unazidi kuwa mdogo sana, naomba ufikie mahali pa kutoa hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba nijielekeze kwenye kutoa hoja, lakini kwa kuwa ninao muda kabla sijatoa hoja...

**NAIBU SPIKA:** Nadhani una dakika siyo zaidi ya tano.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba uamuzi wako ulioufanya nitaukatia rufaa kwa sababu sijaridhika nao kabisa, wa kuzuia nisitoe maelezo, nami nautafsiri ni uamuzi wa kuficha maelezo haya ambayo nilikuwa nataka kueleza kuhusu uozo ulioko kwenye Sekta ya Maji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nina dakika tano peke yake, naomba kwa unyenyekevu mkubwa niwaelekeze Wabunge wenzangu kwenye ukurasa wa 42 ili sasa niweze kutoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2003 mpaka 2010 Serikali ilitekeleza mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya Maji safi na Maji taka jijini Dar es Salaam na maeneo ya Bagamoyo na Kibaha, *Dar es Salaam Motor Supplier in Sanitation Project* umetumia dola milioni 164.

Hata hivyo, mpaka sasa katika maeneo mengi mtandao wake maarufu kama bomba ya wachina hautoi maji, kwa kuwa mwezi Februari, uliandaa waraka maalum wa kuiomba Serikali kutenga kiwango cha fedha Shilingi milioni 653.85, kwa ajili ya mpango maalum wa mwaka 2011/2013 wa kuboresha huduma za maji safi na uondoaji wa maji taka katika jiji la Dar es Salaam na kupitishwa na Baraza la Mawaziri. Lakini hata hivyo utekelezaji wake unakwenda taratibu kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2011/2013 na 2012/2013 Serikali haikutenga kiwango kamili cha fedha kwa kuzingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo ulioidhinishwa na Bunge na kwa kuzingatia

mgawanyo wa Mpango Maalum wa Maji safi na Maji taka katika jiji la Dar es Salaam.

NA KWA KUWA, majukumu ya utoaji wa maji jijini Dar es Salaam yanahusu pia Mamlaka ya Maji safi na Maji taka (*DAWASCO*) ambaye ni mmiliki, mkodishaji na msimamizi wa utoaji wa huduma ya maji safi na maji taka katika jiji la Dar es Salaam, wenye wajibu wa kupanga na kugharamia utekelezaji wa miradi ya miundombinu kuiendeleza na kugharamia matengenezo ya dharura na makubwa;

NA KWA KUWA, majukumu hayo yanahusu pia Mamlaka ya Maji safi na Maji taka (*DAWASCO*) ambaye ni mwendeshaji mwenyewe wajibu wa kuendesha shughuli za kutoa huduma za maji, kutoa ankra kwa wateja, kukusanya maduhuli, kutekeleza matengenezo makubwa yanayogharamiwa na *DAWASA* na kutekeleza uunganishaji wa maji na kutekeleza uunganishaji wa maji kwa wateja wapya kwa kutumia Mfuko wa Maji;

NA KWA KUWA, huduma ya utoaji wa huduma ya maji unamhusu pia Mdhhibiti ambaye ni Mamlaka ya Udhhibiti wa Maji yaani *EWURA*, yenye mamlaka ya kudhibiti utoaji wa huduma za maji, kuidhinisha bei ya huduma ya maji na uondoaji wa maji taka pamoja na kutoa leseni za uendeshaji;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Bunge ndicho chombo chenye madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake vyake katika utekelezaji wa majukumu.

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa ibara ya 63(3) Bunge katika utekelezaji wa madaraka yake laweza kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutunga sheria pale utekelezaji unapohitaji kuwapo sheria.

NA KWA KUWA malengo ya Kitaifa ya kuwapatia wakazi wa mijini maji kwa asilimia 90 ilipokuwa ifikapo 2010 na asilimia 100 ifikapo 2025 na Dar es Salaam iko nyuma sana ukilinganisha na kasi ya ukuaji wa jiji la ongezeko la watu.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ichukue hatua haraka zaidi za kuboresha upatikanaji wa maji safi na ushughulikiaji wa maji taka katika jiji la Dar es Salaam.

Pili, na kwamba Serikali iwasilishe Bunge mpango maalum wa kuboresha huduma ya maji safi na uondoaji maji taka katika jiji la Dar es Salaam uliopitishwa mwezi Machi, 2011 kwa ajili ya kuidhinishwa kutengewa bajeti ya kiutekelezaji ya haraka katika mwaka 2013, 2014 na vipaumbele vya mpango huo uzingatiwe katika Mpango wa Taifa wa mwaka 2013/2014; na kwamba mpango wa dharura wa kupunguza kero ya maji ulianza kutekelezwa na Wizara ya Maji kupitia DAWASA kuanzia Juni, 2010 unahusisha uchimbaji wa visima 29 uliopata kukamilika Oktoba, 2011 uwekewe muda wa ukomo wa kukamilika, kwani Desemba, 2013 katika maeneo ambayo miradi haijakamilika mpaka hivi sasa ikiwemo iliyozinduliwa mwaka 2012 yenye kuhitaji miundombinu ya ziada ya kuwafikia wananchi na kwamba Mkaguzi wa hesabu za Serikali CAG afanye ukaguzi wa thamani ikilinganisha na ufanisi yaani

*value for money audit* wa mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu wa maji safi na maji taka Dar es Salaam na maeneo ya Bagamoyo, yaani *Dar es Salaam Water Supply Sanitation project (WSSP)* kwa kurejea uchunguzi wa kiufundi (*technical audit*) uliofanywa na Kampuni ya *Holland Humphrey* na taarifa iwasilishwe na kujadiliwa Bungeni; na kwamba *EWURA* ifanye ukaguzi wa kiufanisi, yaani *performance audit* wa miradi ya visima vya maji ambavyo vilichimbwa na Serikali na kukabidhiwa kwa *DAWASCO*, Jumuiya za wananchi, Taasisi mbalimbali, lakini hazitoi huduma inayostahili kwa kadri ya malengo ya awali.

Aidha, *EWURA* iharakishe kukamilisha mchakato ulioanza wa kutunga kanuni za udhibiti wa ubora na bei ya huduma ya maji kwa upande wa sekta binafsi katika Jiji la Dar es Salaam na kwamba Serikali iwasilishe Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Dar es Saalam, yaani *The Dar es Salaam Water Sewage Authority Act*, na kwamba Kamati husika ya Bunge ijadili taarifa ya Ukaguzi na ufanisi kuhusu usimamizi wa usambazaji wa maji katika maeneo ya Miji, yaani *Performance Audit Report on the Management of the Water Distribution in Urban Areas* ya Januari mwaka 2012 mara baada ya Mkutano wa Kumi wa Bunge na kwamba Serikali itoe taarifa Bungeni ya sababu za Programu ya Maji safi na Mazingira yaani (*RWSSP*) ambayo ilipaswa kutekelezwa kwenye Manispaa za Temeke, Ilala na Kinondoni kati ya mwaka 2005/2006 mpaka 2010/2011 kutokamilika mpaka mwaka 2013 na kuwasilisha ratiba mpya ya utekelezaji wa haraka.



Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nawashukuruni sana.

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona, muda haupo upande wetu, nimalizie tu kwa kufafanua tena kwa ajili ya kuweka rekodi sawa sawa kwa ambaye anatusikiliza, kwanini hoja ya mabadiliko ya Mheshimiwa Mnyika yale niliyoyasemea hayakuwa yamekubalika. Nilisoma na narudia tena, ni kwa sababu ameingiza vipengele vipya ambavyo vinakiuka masharti ya kanuni namba 55(12), kwa kuwa imebadilisha upeo wa hoja yake ya awali ambayo inaitaka Serikali ichukue hatua za haraka kutatua matatizo ya maji safi na maji taka kwa jiji la Dar es Salaam tu. Wakati mapendekezo ya mabadiliko ya hoja yanaitaka Serikali itatue tatizo hilo katika Halmashauri zilizobaki nchi nzima. Kwa hiyo, kilichomgomea siyo Katibu wa Bunge wala siyo nani, ni kanuni tu na ni kanuni 55(12)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba nitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni. Muda hauturuhusu kabisa, tuko nje ya muda kabisa!

**MBUNGE FULANI:** Si mnatokaga Bungeni?

*(Saa 7.12 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tunaendelea na hoja binafsi ya Mheshimiwa John Mnyika, kuhusiana na kuboresha upatikanaji wa Maji safi na Ushughulikiaji wa Maji taka, katika Jijini la Dar es Salaam. Baada ya kuwa mtoa hoja amefanya kazi hiyo wakati wa kipindi cha asubuhi, tunaendelea na uchangiaji na mchangiaji wa kwanza atakuwa Waziri wa Maji - Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, Kanuni namba 57 (1) (c), naomba kupendekeza mabadiliko katika hoja binafsi iliyowasilishwa na Mheshimiwa John Mnyika - Mbunge wa Ubungo ya kulitaka Bunge lijadili na kupitisha Maazimio ya hatua za haraka za kuboresha upatikanaji wa maji safi na ushughulikiaji wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam, kwa kuongeza maneno mapya, baada ya *para* ya mwisho ya hoja hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu ni kuitaka Serikali kuchukua hatua za haraka, kuboresha huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam ambalo tayari unatekelezwa mpango maalum uliotengewa fedha nyingi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi na kuzingatia kwamba utekelezaji wa mpango huo unaendelea vizuri sana, hivyo basi, napendekeza hoja hiyo iondolewe.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba nusu dakika. Mheshimiwa John Mnyika, mbona unafanya fujo kwenye hoja yako mwenyewe? Wewe si umeshamaliza kutoa hoja, wenzako wanachangia?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna nakala ya mapendekezo ya mabadiliko ambayo Waziri anataka kuyafanya.

**NAIBU SPIKA:** *Okay!* Katibu Mezani endelea, nafikiri ndiyo hoja hiyo. Endelea Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Maelezo ya mabadiliko yanayopendekezwa hivi sasa Jiji la Dar es Salaam hupata maji yake kutoka mitambo mitatu ambayo ni Ruvu Juu, Ruvu Chini na Mtoni. Mtambo wa Mtoni uliopo kwenye Mto Kizinga ulijengwa mwaka 1947, na una uwezo wa kuzalisha maji lita milioni tisa kwa siku. Mtambo wa Ruvu Juu ulijengwa mwaka 1958 na una uwezo wa kuzalisha maji lita 82 kwa siku, na mtambo wa Ruvu Chini ulijengwa mwaka 1976 na uwezo wa kuzalisha lita milioni 182 kwa siku.

Pia vipo visima ambavyo vilichimbwa mwaka 1997 ambavyo vina uwezo wa kuzalisha milioni 27 kwa siku. Hivyo, maji yanayozalishwa kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam, hivi sasa ni lita milioni 300 ukilinganisha na mahitaji ya lita milioni 450 kwa siku. Hivyo, kuna upungufu wa lita milioni 150 kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uwezo wa miundombinu iliyopo, yaani *installed capacity*, inakadiriwa kuwa asilimia 68 ya wakazi wa Dar es Salaam, pamoja na

Miji ya Kibaha na Bagamoyo wanapata huduma ya Maji Safi. Upungufu huu wa maji, unaongezeka kila wakati kutokana na ongezeko kubwa la watu Jijini linalokadiriwa kuwa asilimia sita kila mwaka, ukilinganishwa na ongezeko la watu katika Miji mingine nchini Tanzania ya asilimia 4.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wakazi wa Dar es Salaam wanakadiriwa kuwa milioni nne ikilinganishwa na wakazi milioni mbili waliokuwa Dar es Salaam miaka kumi iliyopita. Aidha, uvujaji wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu na matumizi yasiyolipiwa, yanazalisha upotevu wa asilimia 42 ya maji hivi sasa. Hali hii pamoja na ongezeko kubwa la shughuli za kuchumi na kijamii, kupanuka kwa ujenzi na makazi, kupungua kwa maji kwenye vyanzo kutokana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, yote haya huongeza upungufu wa maji Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma ya Majitaka, miundo mbinu iliyopo haikidhi mahitaji ya sasa na ni changamoto kubwa kwa usafi na mazingira ya Jiji. Miundombinu hiyo inatoa huduma kwa asilimia 10 ya makazi na asilimia 90 iliyobaki wanatumia makaro na vyoo vya mashimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuanzia mwaka 2003 imechukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji Jijini Dar es Salaam. Kwa kuwa, kulikuwa hakuna uwekezaji mkubwa Dar es Salaam tangu mwaka 1976 na miundombinu ilikuwa inachakaa, Serikali ilibuni mradi wa ukarabati wa miundombinu uliotekelzwa kati ya mwaka 2003 - 2009 (*The Dar es Salaam Water Supply and*

*Sanitation Program*). Lengo la mradi huo ilikuwa kukarabati miundombinu ili iweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya mradi wa ukarabati uliofanyika ni pamoja na kuunganisha wateja wapya 67,662, kufunga dira za maji za wateja wapya 125,000, ulazaji wa mabomba mapya kilometa 1,550, kuimarisha uzalishaji katika mitambo yote mitatu, kuongeza ukusanyaji mapato kutoka Shilingi bilioni moja hadi bilioni mbili na nusu kwa mwezi, ukarabati wa mabwawa manne ya majitaka na ukarabati wa mabomba ya majitaka kilometa 66. Mradi huu pia ulihusu ujenzi wa miradi maji ya kijamii katika maeneo yasiyo na mfumo rasmi wa mabomba, na maeneo yaliyokuwa na historia ya milipuko ya magonjwa ya kuambukiza ambapo visima 38 vilichimbwa, vituo 440 vya kuchotea maji vilijengwa na wananchi laki 440,000 walipatiwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukarabati huo, Serikali ilifanya uchunguzi wa vyanzo vipya vya maji, na kuandaa mpango wa muda mrefu wa kuboresha huduma ya maji safi na uondoaji wa majitaka Jijini Dar es Salaam. Mpango huu ulibuniwa na kuridhiwa na Serikali mwaka 2010, ambapo kwa kipindi hicho Mbunge wa Jimbo la Ubungo alikuwa Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, ambaye alikuwa mstari wa mbele akishirikiana na Wabunge wengine wa Chama cha Mapinduzi, Waheshimiwa Mussa Z. Azzan - Mbunge wa Ilala, Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga - Mbunge wa Ukonga, Mheshimiwa Iddi M. Azzan - Mbunge wa Kinondoni, Mheshimiwa Rita L. Mlaki - Viti Maalum, na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Janeth

Masaburi katika kuhakikisha kwamba mpango huo maalum unaandaliwa na kupitishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuwaeleza ni kwamba, juhudi hizi zilikwishaanza hata kabla mtoa hoja hajawa Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo mengine Tanzania, lipo tatizo kubwa na sugu la upatikanaji wa majisafi na salama nchini kote. Hivyo, Serikali imekuwa ikitekeleza *Program* ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kukabiliana na tatizo hili kwa nchi nzima. Utekelezaji wa *program* hiyo, upo katika hatua mbalimbali. Kwa mfano, katika Majiji ya Tanga, Mwanza, Mbeya na Manispaa za Iringa Songea na Moshi, miradi hiyo imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia miradi ya majisafi inaendelea au inaanza kutekelezwa katika Manispaa za Bukoba, Musoma, Kigoma, Sumbawanga, Babati, Lindi, Mtwara, Morogoro, Dodoma, Singinda na Tabora. Aidha, utekelezaji wa miradi ya Vijiji vitano, katika kila Halmashauri, upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na katika maeneo machache miradi hiyo imekamilika. Vijiji vitano vilivyobaki katika Vijiji kumi, vitatekelezwa katika mwaka wa fedha 2013/2014. Changamoto iliyoko mbele ni kubwa, hivyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuungane na Serikali katika kupambana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji wa Mpango Maalum wa Dar es Salaam; Utekelezaji wa Mpango Maalum wa Maji kwa Jiji la Dar es

Salaam ambao ulianza mwaka wa fedha 2010/2011, unaendelea vizuri. Katika makisio ya awali, mpango ulikadiriwa kugharimu Shilingi bilioni 635.85. Hata hivyo, baada ya usanifu wa kina wa kila mradi gharama halisi ya utekelezaji wa miradi yote ni Shilingi trilioni 1,089.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa inaleta matumaini kwamba hivi karibuni shida ya maji ambayo inalikabili Jiji la Dar es Salaam kwa muda mrefu itakuwa historia. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayo nia ya dhati ya kuendelea kutekeleza mpango huu na kuitengea fedha za kutosha ili kuhakikisha kuwa mpango huu unatekelezwa kwa haraka na kukamilika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya mpango huu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa maji wa Ruvu Chini, umekamilika kwa asilimia 75. Matarajio ni kukamilika mradi huu mwezi Machi mwaka huu 2013. Aidha, Mkandarasi wa ulazaji wa bomba kuu la kipenyo cha milimeta 1,800 kutoka mtambo wa Ruvu chini hadi Jijini ameanza kazi mwezi Oktoba mwaka huu. Kazi hii inatarajiwa kukamilika miezi 15. Hivyo, mradi utakamilika na maji yatafika Dar es Salaam Januari mwaka 2014. Mradi huu utagharimu Shilingi bilioni 192.68 na utazalisha lita za maji milioni 270 kila siku, ukilinganisha na lita milioni 182 za sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Pili; Serikali ya Tanzania imepata fedha kutoka Serikali ya India dola za Kimarekani milioni 178.125 sawa na Shilingi bilioni 289.45 kwa ajili ya

upanuzi wa chanzo cha maji Ruvu Juu; ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara; na Ujenzi wa tanki kubwa katika eneo la Kimbamba; usanifu na ujenzi wa mabomba ya usambazaji katika maeneo ambayo hayana mtandao wa maji yakiwemo maeneo ya Mlandizi, Kibaha, Mbezi Luisi, Msumi, Makabe, Msakuzi, Malamba Mawili, Msigani, Kimara, Kibangu, Makaburi, Tabata na Segerea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 3 Desemba, 2012 lilitangazwa kusudio la kushiriki kwa ajili ya kumpata mtaalam mshauri atakayefanya mapitio ya usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Tarehe 15 Januari, 2013 yalipokelewa makusudio ya kushiriki zabuni hizo. Uchambuzi umekamilika na taarifa imepelekwa *Exim Bank of India* tarehe 30 Mwezi huu kwa ajili ya kupata kibali au *no objection* ili kugawa zabuni kwa kampuni ambazo zinataka kushiriki katika ujenzi wa mradi huo.

Aidha, zabuni za kuwatafuta Wakandarasi watakaoshindanishwa, yaani *pre-qualification* zilitangazwa tarehe 13 Januari, 2013 na zitapokelewa tarehe 28 Februari, 2013. Ujenzi wa mradi utanza mwezi Agosti, 2013 na kukamilika mwezi Machi, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu, kunatarajiwa kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 82 hadi kufikia lita milioni 196. Kukamilika kwa mradi wa Ruvu Juu na Ruvu Chini kutahakikisha kuwa jumla ya maji yanayofika Dar es Salaam ni lita milioni 502 kwa siku, ukilinganisha na mahitaji ya watu wa Dar es Salaam ya milioni 450. Kwa hiyo, tutakuwa



tumefikia utoshelevu wa maji Jijini Dar es salaam kwa watu wanaoishi hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, usanifu na utayarishaji wa vitabu vya zabuni kwa ajili wa ujenzi wa bwawa la Kidunda utakamilika mwezi Machi, 2013. Uthamini kwa ajili ya mali za wananchi watakaohamishwa kupisha ujenzi, umekamilika, na maeneo watakapohamishiwa yameshatambuliwa. Aidha, Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi hao zimetengwa kwenye bajeti ya mwaka 2012/2013. Ujenzi wa Bwawa utaanza mwezi Oktoba, 2013 na kukamilika mwezi Mei, 2015. Gharama za ujenzi huu zitakuwa Shilingi bilioni 179.7

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, usanifu pamoja na utayarishaji wa vitabu vya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 75 kutoka Ngerengere hadi Kidunda kwenye eneo la ujenzi wa Bwawa umekamilika. Ujenzi wa barabara hii unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2013, na kukamilika baada ya miezi 12. Gharama za ujenzi wa mradi huu zitakuwa Shilingi bilioni 37.5

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya kuchimba visima 20 vya mwanzo katika eneo la Kimbiji na Mpera unaendelea hivi sasa. Kibali cha Benki ya Dunia cha kuendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi kimetolewa tarehe 29 Januari, 2013. Hatua inayofuata, ni kufanya majadiliano na Mkandarasi kabla ya kusaini Mkataba wa Uchimbaji ili kuhakikisha kwamba anaweza kukidhi viwango vyote. Uchimbaji utaanza mwezi

Machi, 2013 na kukamilika mwezi Machi, 2014. Gharama za mradi huu ni Shilingi bilioni 103.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fedha kwa ajili ya fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi ambazo ni Shilingi bilioni 27 zinaombwa kwenye bajeti ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, hatua za kupunguza uvujaji wa maji na maji yasiyolipiwa *non-revenue water* kutoka asilimia 53 mwaka 2010 hadi asilimia 25 mwaka 2015 zinaendelea. Mradi huu unatarajia kugharimu Shilingi bilioni 17.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 23 Machi, 2012 kwa mwaliko wa *DAWASCO* Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam, akiwemo Mheshimiwa John Mnyika, walifanya ziara ya kukagua shughuli za *DAWASA* na *DAWASCO*, wakati wa ziara hiyo walipatiwa maelezo kuhusu mpango maalum wa kulipatia maji Jiji la Dar es Salaam, ambao utekelezaji wake ulianza mwaka 2010/2011.

Pia, Waheshimiwa Wabunge walitembelea Mtambo wa Maji wa Ruvu Juu, na baadaye chanzo cha maji cha Ruvu Chini na kujionea kazi ya upanuzi ya mtambo wa maji wa Ruvu Chini unaoendelea hivi sasa na kueleza kuridhika kwao na utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hiyo utakapokamilika mwezi Machi, 2015, utawezesha uzalishaji wa maji kufikia lita milioni 765 kwa siku, kutoka kwenye vyanzo kama ifuatavyo:-

Ruvu chini lita milioni 270, Ruvu juu lita milioni 196, Visima vya Kimbiji na Mpera lita milioni 260, Mtambo wa Mtoni lita milioni tisa na visima vingine lita milioni 30, maji hayo yanatosheleza mahitaji ya maji kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, viunga vyake na maeneo ya Bagamoyo na Kibaha, kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2032. Aidha, maeneo ambayo mabomba yalilazwa na kukarabatiwa ambayo hayapati maji na maeneo yote ambayo hayana mtandao wa maji kwa sasa yatapata maji ya kutosha baada ya miradi hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yatakayojengewa mtandao mpya wa mabomba ya majisafi ni pamoja na Kiluvya, Kibamba, Mbezi Luisi, Mbezi Msome, Msakuzi, Makabe, Mpiji, Magohe, Goba, Salanga, Malambamawili, King'ong'o, Matosa, Bonyokwa, Kibangu, Kinyerezi, Kipawa, Kiwalani, Vinguguti, Uwanja wa Ndege, Ukonga, Gongolamboto, Pugu, Chanika, Yombo, Tandika, Korogwe, Mbagala, Tuwangoma Kibada na Kigamboni.

Maeneo mengine ni Tegeta, Bahari *Beach*, Boko, Bunju, Salasala, Mbezi Juu, Goba, Kinzumbi, Madale, Kisonta, Mabwepande, Mpiji, Vikawe, Mapinga, Zinga, Kilombo, Bagamoyo na Vitongoji vyake.

Vilevile, maeneo mengine ya Jiji na yale ya Kibaha na Mlandizi ambayo hayakufikiwa na Mradi wa *Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Project*, nayo yatawekewa mtandao mpya. Gharama ya kazi ya kuongeza mtandao katika maeneo hayo ni Shilingi bilioni 138.85.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yatakayofikiwa na Mradi wa Upanuzi wa Mfumo wa Majitaka ni pamoja na Ilala, Buguruni, Keko, Chang'ombe, Kurasini, Tandika na Temeke.

Pia maeneo ya Magomeni, Mwananyamala, Kinondoni, Manzese, Masaki, Msasani, Kijitonyama na Mbezi *Beach*. Mitambo mitatu ya kisasa ya kusafisha majitaka itajengwa maeneo ya Jangwani, Kurasini na Mbezi *Beach* ili kupunguza matumizi ya mabwawa yaliyopo sasa na kuondoa au kutotumia bomba kubwa la maji ambalo linamwaga maji katika Bahari. Gharama ya Mradi huu ni Shilingi bilioni 109.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli kuwa utekelezaji wa Miradi hii mikubwa ya kuleta maji itakayotosheleza Jiji la Dar es Salaam, itakamilika mwezi Machi, 2015, Mheshimiwa Rais - Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 24 Mei, 2010, aliielekeza Wizara yangu ichimbe visima virefu katika maeneo mbalimbali ya Jiji ili kupunguza matatizo ya maji katika maeneo ambayo yana matatizo makubwa ya maji, wakati utekelezaji wa miradi mikubwa unaendelea.

Awali, vilikuwa vichimbwe visima 24 lakini kutokana na mahitaji kuwa makubwa, idadi ya visima imekuwa ikiongezeka, hadi hivi sasa, lengo ni kuchimba visima 34 ambapo 27 vimechimbwa kama ifuatavyo:-

Ubungo na Kimara tisa, Mburahati vitatu, Chang'ombe na Keko vitano, Tandale na Temeke vitatu, Kigamboni vinne, Mbagala na Mtoni viwili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri! Sekunde mbili, Mheshimiwa Tundu Lissu, ukae kidogo. Mheshimiwa Waziri!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena kwamba, hili Bunge linaendeshwa na Kanuni na Kanuni ninayotaka kuisema hapa ni ya 62(1) (a), inayohusu muda wa kuchangia hoja.

Nafahamu Mheshimiwa Waziri ni Waziri, lakini yeye sio mwenye hoja hapa. Kwa hiyo, hawezi akazungumza kwa muda uliowekwa kwenye Kanuni ya 62(1) (b), inayompa nusu saa, anachangia hapa kama mchangiaji mwingine yeyote na anatakiwa azungumze kwa dakika 15.

Amesimama hapa tangu saa 11.00, sasa hivi zimepita dakika 25. Anapewa upendeleo ambao haustahili, anapewa upendeleo ambao uko kinyume cha Kanuni. Naomba Waziri afuate Kanuni, acae chini, muda wake wa kuzungumza ulishakwisha.

**NAIBU SPIKA:** Makatibu walipitiwa tu kidogo. Mheshimiwa Waziri hitimisha hoja yako. Ninakupa dakika tatu za kumalizia.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii naitoa kwa faida ya Wabunge, ili waelezwe kazi hii ina...  
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu na uhitaji wa maji uliopo Jijini Dar es Salaam na kwamba fedha nyingi zimetengwa kwa ajili ya kulipatia Jiji la Dar es Salaam

majisafi na kuondoa majitaka, Serikali inatambua shida kubwa ya maji inayowakabili wananchi kutoka maeneo mbalimbali nchini. Kwa hiyo, kuendelea kuijadili hoja hii kama vile ni Dar es Salaam peke yake inayohitaji maji na hasa baada ya Serikali kuandaa na kutekeleza mpango mkubwa sana wa kutatua tatizo la maji Jijini Dar es Salaam, kunaweza kujenga hisia ya upendeleo kwa Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu!

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilishatoa maelezo kuhusu mpango wa utekelezaji wa mpango huo maalumu hapa Bungeni tarehe 7 Desemba, 2012 na nimeeleza hatua iliyofikiwa hadi sasa, naomba Bunge lako Tukufu liazimie kuiruhusu Serikali iendelee na utekelezaji.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Malizia Mheshimiwa Waziri. Ameshafika mwisho kabisa, niwape nafasi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu liazimie kuiruhusu Serikali iendelee na utekelezaji huo na kuwa Serikali iwe inatoa taarifa ya maendeleo ya utekelezaji huo kwenye Kamati ya Bunge linalohusika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu!

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweka msisitizo kwenye hoja yangu, naliomba Bunge lako Tukufu, kwa kuwa hoja iliyo mbele yetu...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu ni kuitaka Serikali kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka Jijini Dar es Salaam, ambalo tayari linatekelezwa na mpango maalumu uliotengewa fedha nyingi na Serikali, hivyo naomba kutoa hoja kwamba hoja hii iondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu!

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah! Ubabe, Ubabe!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba tuelewane.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hoja ijadiliwe!

**NAIBU SPIKA:** Naomba Mheshimiwa Halima Mdee ukae, nitakupa nafasi sasa hivi. Mheshimiwa John Mnyika, hoja ni ya kwako, unayeongoza vurugu ni wewe mwenyewe. Mheshimiwa John Mnyika, unasema hoja ijadiliwe siyo?

**WABUNGE FULANI:** *Aaaah!*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Naona umesimama.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, kwa kifupi sana nataka nimpe nafasi Mheshimiwa Halima Mdee aendelee. Nilikuwa nakugusa tu wewe kwa sababu nakuona hoja ni ya kwako, ukishakuwa wewe ndiye mwenye harusi yako, unanyamaza! Unawaachia wenzako! (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Tundu Lissu, tulikukubalia jambo lako tena tunataka kubishana nini tena! Aah!

Nataka kutoa mwongozo namna ya kuenenda au unataka kunitangulia tena. Nimempa nafasi Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ninachokiona hapa ni mwendelezo wa uvunjwaji wa Kanuni na sitarajii kama Kiti chako kitaruhusu yale makosa yaliyofanywa na Spika yafanywe tena. Kwa nini nasema hivyo?



Masuala ya hoja binafsi yanaratibiwa na Kifungu ama Kanuni namba 57 na 58. Kanuni namba 57(1) (a) mpaka (c) na (3), imetoa maelekezo kwa mtu ambaye anataka kuleta mabadiliko ya hoja. Mheshimiwa Waziri alichotakiwa kufanya, apendekeze katika yale mapendekezo ya Mheshimiwa Mnyika kitu gani kitoke na kitu gani kibaki, lakini asibadilishe hoja nzima ya Mheshimiwa Mnyika. Hiyo ni moja, lakini asiue *exactly*. Anachokifanya Mheshimiwa Waziri anaua hoja nzima ya Mheshimiwa Mnyika, ambayo hakuna Kifungu... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, kwa dakika mbili, tatu tu halafu utaendelea, nitakupa nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, tuelewane, ni vizuri kwenda kwa kuelewana. Mtoa hoja Mheshimiwa Mnyika amekwishatoa hoja yake asubuhi ya leo, Mheshimiwa Waziri ni mchangiaji wa kwanza katika hoja hiyo. Katika uchangiaji wake ana mambo ambayo ameyaweka mbele yetu, nilitaka niyaweke vizuri ili sote tuwe tunakwenda pamoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Waswahili walisema kuchamba kwingi, haya ni maneno ya Waswahili siyo ya kwangu haya.

**MBUNGE FULANI:** Utatoka na ...

**NAIBU SPIKA:** Tupeane nafasi tuzungumze kama watu wazima, tuelewane, lakini huku kujua ambako kunazidi kiasi ndiyo tatizo. Lazima twende kama nyumba moja, tusiende kikundi cha watu wawili, watatu wanaoelewa kinachoendelea humu ndani na wengine hawaelewi kinachoendelea humu ndani. Kwa hiyo, kinachoendelea ni nini kwa sababu mimi ndiye ninayeongoza kikao?

Ni kwamba, Mheshimiwa Waziri kama mchangiaji wa hoja, ametoa hoja kwa kutumia Kanuni ya 57(1) (c) kwa kusema kwamba, kwa kuwa hoja iliyo mbele ya Bunge ni kuitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kuboresha huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam, ambalo tayari linatekeleza Mpango Maalum uliotengewa fedha nyingi na Serikali ya CCM, kwa kuzingatia kwamba, utekelezaji wa Mpango huo unaendelea vizuri sana.

Hivyo basi, napendekeza hoja hiyo iondolewe. Hiyo ndiyo hoja ambayo ameitoa na imeungwa mkono.

Katika utaratibu wetu wa uendeshaji, hoja ya namna hiyo ikitolewa, baada ya kuwa mtoa hoja alikwishasema, inachangiwa na Wabunge. Kwa hiyo, katika uchangiaji wa Wabunge, wale Wabunge ambao wangependa kuichangia hoja hii iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, naomba wasimame pale walipo, nichukue majina ya baadhi yao. Sasa Mheshimiwa Halima utakuwa wa kwanza katika hao ili sasa kuchangia inakuwa ni vizuri zaidi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimeomba kuhusu utaratibu kutokana na maneno aliyoyazungumza Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU SPIKA:** Ngoja nichukue majina halafu tutaendelea.

Ahsante nadhani sasa nimepata majina ya kutosha, naomba Mheshimiwa Halima uwe mchangiaji wa kwanza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Sasa hakuna cha kuhusu utaratibu wala nini. Tunaendelea na hoja iliyoko kwenye Meza yetu. Mheshimiwa Halima endelea ulikuwa unazungumza nini?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wengine pia wameleta mapendekezo ya mabadiliko na yenyewe si yanatakiwa yasomwe halafu yajadiliwe yote kwa mujibu wa Kanuni?

**NAIBU SPIKA:** Umekuja juzi Mheshimiwa Nassari, unajua kuliko Wabunge waliotangulia?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni matusi, nimekuja juzi!

**NAIBU SPIKA:** Hoja huwa tunashughulikia moja baada ya nyingine. Hii ni ya kwanza kutolewa. Kama kuna mabadiliko mengine nayo yatashughulikiwa *accordingly*.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Si zinatolewa zote!

**NAIBU SPIKA:** Tunakwenda na hoja moja baada ya nyingine na ya kwanza kufuatana na Kanuni inakuwa ni upande wa Serikali kwa Hoja Binafsi za Wabunge.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, umebaka Kanuni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, nimekuheshimu sana tangu asubuhi, siyo vizuri kunivuruga bila sababu. Wewe ni *Chief Whip*, unajua Hoja Binafsi ya Mbunge, mtu wa kwanza ku-respond kwa kadiri ya Kanuni inakuwa ni upande wa Serikali, Wabunge wote mnajua. Upande wa Serikali wametoa hoja, ipo tunaijadili hiyo.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Iko wapi? Kuna vitu vingine vile vile visomwe kwa pamoja!

**MBUNGE FULANI:** Atoke nje huyo! Toka nje!

**NAIBU SPIKA:** Nadhani Mheshimiwa Halima kama hutumii hii nafasi, natoa kwa mtu mwingine.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Toa!

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuweza kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niishukuru sana Serikali pamoja na Wabunge wa Dar es Salaam wa kipindi kilichopita kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Sisi Wana-Dar es Salaam, tunajua matatizo ya maji... (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Hivi huyo Mbunge ameongea kitu gani cha kumpa taarifa wakati anaanza tu kuongea! Haya mpe taarifa Mheshimiwa Mnyika. Makatibu naomba ile nanii haraka sana.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ...

**MBUNGE FULANI:** Tokeni nje! Tulishawazoea haoooo!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba pawe na utulivu ndani ya Ukumbi wa Bunge. Naomba pawe na utulivu. Niliyempa nafasi ya kuongea...

**WABUNGE FULANI:** *Aaaah!*

**NAIBU SPIKA:** Tuwavumilie wapige kelele wakishamaliza tataendelea. Anayeongea ni Mbunge, Taifa zima linaona. Anayeongea ni Mbunge wenu wa CHADEMA, mnaofanya fujo ni ninyi wenyewe.

Mheshimiwa Mnyika, wanaokuzuia kuongea ni wenzako!

**WABUNGE FULANI:** *Aaaah!*

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo! Nipeni ile Kanuni. Hiyo Kanuni hamjaiona tu! Hawajaipata mpaka sasa hivi?

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya ya kisiasa....

**MBUNGE FULANI:** Hakuna cha kisiasa! Kanuni zifuatwe! Kama ni taarifa wote wapewe nafasi ya kuzungumza, siyo upande mmoja, wengine hapana.

**WABUNGE FULANI:** *Kanuni zifuatwe! Taarifa, taarifa, taarifa!*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mtaanza kuimba Mungu Ibariki Afrika hapa!

**NAIBU SPIKA:** Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unaweza ukaendelea. Unaongea na mimi.

**MBUNGE FULANI:** Tupewe fursa sawa ya kusema hapa Bungeni, hakuna cha nani wala nani!

**MBUNGE FULANI:** Taarifa! Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unaweza ukaendelea. Unaongea na mimi endelea.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili ambalo ...

**WABUNGE FULANI:** *CCM! CCM! CCM! CCM!*

**NAIBU SPIKA:** Labda uje, sikusikii! Leo nataka Watanzania mwone kinachoendelea na siahirishi Bunge mjionee wenyewe jinsi ambavyo kuna utovu wa nidhamu na muwe mnaona ni Wabunge wa aina gani wanaosababisha utovu huo. Siahirishi Bunge, lazima Watanzania leo waelewe mbivu na mbichi.

**WABUNGE FULANI:** *CCM! CCM! CCM! CCM!*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Yaani, wanatuburuza sisi! Tunaona tu watoke wao, sisi tubaki.

**MBUNGE FULANI:** Ya leo kali!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Hapana wanatuburuza sana, imekukwa *too much!*

**MBUNGE FULANI:** Inabidi tuheshimiwe wote!

**NAIBU SPIKA:** Vipi mmechoka kufanya fujo? Endeleeni!

**WABUNGE FULANI:** Hapana!

**NAIBU SPIKA:** Ninakaa hapa kusubiri fujo zenu tu!

**WABUNGE FULANI:** Hapana!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mnatuburuza sana humu ndani bwana!

**MBUNGE FULANI:** Tumeshachoka!

**MBUNGE FULANI:** Waziri amesema uongo, amedanganya!

**NAIBU SPIKA:** Sasa ninahoji wanaoafiki kwamba hoja hii iondolewe waseme ndiyo.

**WABUNGE FULANI:** Sasa utaihoji vipi wakati tuna majadiliano?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyoooooooooooo!

**NAIBU SPIKA:** Wanaokataa waseme siyo.

**WABUNGE FULANI:** Siyooo!

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeondolewa. Walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja Binafsi ya Mheshimiwa John Mnyika  
iliondolewa na Bunge)*

**MHE. TUNDU M. LISSU:** Aaaaaa! Aaaaaaaaaaaaah! Aibu!



**NAIBU SPIKA:** Hoja imeondolewa na Bunge linaahirishwa hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

Kamati ya Uongozi, mnatakiwa kukutana sasa hivi katika Ukumbi wa Spika.

**WABUNGE FULANI:** *CCM! CCM! CCM! CCM!*

*(Saa 11.45 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 5 Februari, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*